# Isaya

1 Maono kuhusu Yuda na Yerusalemu ambayo Isaya mwana wa Amozi aliyaona wakati wa utawala wa Uzia, Yothamu, Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda.

*Taifa asi*

2 Sikieni, enyi mbingu! Sikilizeni, enyi dunia!
Kwa maana Mwenyezi Mungu amesema:
“Nimewalisha watoto na kuwalea,
lakini wameniasi mimi.
3 Ng’ombe anamjua bwana wake,
naye punda anajua hori la mmiliki wake,
lakini Israeli hajui,
watu wangu hawaelewi.”

4 Ole wa taifa lenye dhambi,
watu waliolemewa na uovu,
uzao wa watenda mabaya,
watoto waliozoelea upotovu!
Wamemwacha Mwenyezi Mungu,
Wamemkataa kwa dharau
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli
na kumgeuzia kisogo.

5 Kwa nini mzidi kupigwa?
Kwa nini kudumu katika uasi?
Kichwa chako chote kimejeruhiwa,
moyo wako wote ni mgonjwa.

6 Kutoka wayo wako wa mguu hadi kwenye utosi
wa kichwa chako
hakuna uzima:
ni majeraha matupu na makovu
na vidonda vinavyotoa damu,
havikusafishwa au kufungwa
wala kulainishwa kwa mafuta.

7 Nchi yenu imekuwa ukiwa,
miji yenu imeteketezwa kwa moto;
mashamba yenu yameachwa tupu na wageni
mbele ya macho yenu,
yameharibiwa kama yaliyopinduliwa na wageni.
8 Binti Sayuni ameachwa kama kipenu
katika shamba la mizabibu,
kama kibanda katika shamba la matango,
kama mji uliozingirwa.
9 Kama Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni*
hakutuachia walionusurika,
tungekuwa kama Sodoma,
tungefanana na Gomora.

10 Sikieni neno la Mwenyezi Mungu,
ninyi watawala wa Sodoma;
sikilizeni Torati ya Mungu wetu,
enyi watu wa Gomora!
11 Mwenyezi Mungu anasema, “Wingi wa sadaka zenu,
ni kitu gani kwangu?

* **1:9** Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni hapa ni Yahweh Sabaoth; pia *Warumi 9:29* na *Yakobo 5:4*.

Nina sadaka za kuteketezwa nyingi kupita kiasi,
za kondoo dume na mafuta ya wanyama walionona.
Sipendezwi na damu za mafahali
wala za wana-kondoo na mbuzi.
12 Mnapokuja kujihudhurisha mbele zangu,
ni nani aliyewataka ninyi mfanye hivyo,
huku kuzikanyaga nyua zangu?
13 Acheni kuniletea sadaka zisizokuwa na maana!
Uvumba wenu ni chukizo kwangu.
Miandamo ya Mwezi, Sabato na makusanyiko ya ibada:
siwezi kuvumilia makusanyiko yenu maovu.
14 Sikukuu zenu za Miandamo ya Mwezi,
na sikukuu zenu zilizoamriwa:
moyo wangu unazichukia kabisa.
Zimekuwa mzigo kwangu,
nimechoka kuzivumilia.
15 Mnaponyoosha mikono yenu katika maombi,
nitaficha macho yangu nisiwaone;
hata mkiomba maombi mengi
sitasikiliza.

“Mikono yenu imejaa damu!

16 “Jiosheni na mkajitakase.
Yaondoeni matendo yenu maovu mbele zangu;
acheni kutenda mabaya.
17 Jifunzeni kutenda mema, tafuteni haki.
Wateteeni waliodhulumiwa.
Teteeni shauri la yatima,
wateteeni wajane.

18 “Njooni basi tujadiliane,”
asema Mwenyezi Mungu.
“Ingawa dhambi zenu ni kama rangi nyekundu,
zitakuwa nyeupe kama theluji;
ingawa ni nyekundu sana kama damu,
zitakuwa nyeupe kama sufu.
19 Mkikubali na kutii,
mtakula mema ya nchi,
20 lakini mkikataa na kuasi,
mtaangamizwa kwa upanga.”
Kwa kuwa kinywa cha Mwenyezi Mungu kimenena.

21 Tazama jinsi mji uliokuwa mwaminifu
umekuwa kahaba!
Mwanzoni ulikuwa umejaa unyofu,
haki ilikuwa inakaa ndani yake,
lakini sasa ni wauaji!
22 Fedha yenu imekuwa takataka,
divai yenu nzuri imechanganywa na maji.
23 Watawala wenu ni waasi,
rafiki wa wezi,
wote wanapenda rushwa
na kukimbilia hongo.
Hawatetei yatima;
shauri la mjane halileti mbele yao.

24 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
Mwenye Nguvu wa Israeli, asema hivi:
“Lo! Nitapata faraja kutoka kwa adui zangu,
na kujilipizia kisasi kwa watesi wangu.
25 Nitauelekeza mkono wangu dhidi yenu,

nitawasafisha takataka zenu zote
na kuwaondolea unajisi wenu wote.

26 Nitawarudishia waamuzi wenu kama ilivyokuwa siku za zamani,
nao washauri wenu kama ilivyokuwa mwanzoni.
Baadaye utaitwa,
Mji wa Haki,
Mji Mwaminifu."

27 Sayuni itakombolewa kwa haki,
wale walio ndani yake waliotubu, kwa uaminifu.
28 Lakini waasi na wenye dhambi wote wataangamizwa,
nao wanaomwacha Mwenyezi Mungu wataangamia.

29 "Mtaaibika kwa sababu ya hiyo mialoni
ambayo mlifurahia,
mtafadhaika kwa sababu ya bustani
mlizozichagua.
30 Mtakuwa kama mwaloni ulio na majani yanayonyauka,
kama bustani isiyokuwa na maji.
31 Mtu mwenye nguvu atatoweka kama majani makavu yanayowaka moto,
na kazi yake kama cheche ya moto;
vyote vitaungua pamoja,
wala hakuna wa kuuzima huo moto."

# 2

### *Mlima wa Mwenyezi Mungu*
### *(Mika 4:1-3)*

1 Hili ndilo aliloliona Isaya mwana wa Amozi
kuhusu Yuda na Yerusalemu:

2 Katika siku za mwisho
mlima wa Hekalu la Mwenyezi Mungu utaimarishwa
kama mlima mkuu miongoni mwa milima yote,
utainuliwa juu ya vilima,
na mataifa yote yatamiminika huko.
3 Mataifa mengi yatakuja na kusema,
"Njooni, twendeni kwenye mlima wa Mwenyezi Mungu,
kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo.
Atatufundisha njia zake,
ili tuweze kuenenda katika mapito yake."
Torati itatoka Sayuni,
neno la Mwenyezi Mungu litatoka Yerusalemu.
4 Atahukumu kati ya mataifa
na ataamua migogoro ya mataifa mengi.
Watafua panga zao ziwe majembe,
na mikuki yao kuwa miundu ya kukata matawi.
Taifa halitainua upanga dhidi ya taifa jingine,
wala hawatajifunza vita tena.

5 Njooni, enyi nyumba ya Yakobo,
tutembeeni katika nuru ya Mwenyezi Mungu.

### *Siku ya Mwenyezi Mungu*

6 Mwenyezi Mungu umewatelekeza watu wako,
nyumba ya Yakobo.
Wamejaa ushirikina unaotoka Mashariki,
wanapiga ramli kama Wafilisti
na wanashikana mikono na wapagani.
7 Nchi yao imejaa fedha na dhahabu,
hakuna mwisho wa hazina zao.
Nchi yao imejaa farasi,
hakuna mwisho wa magari yao ya vita.
8 Nchi yao imejaa sanamu;
wanasujudia kazi za mikono yao,
vitu vile vidole vyao vimevitengeneza.
9 Kwa hiyo mwanadamu atashushwa
na binadamu atanyenyekezwa:
usiwasamehe.

10 Ingieni kwenye miamba,
jificheni ardhini
kutokana na utisho wa Mwenyezi Mungu
na utukufu wa enzi yake!
11 Macho ya mtu mwenye majivuno yatanyenyekezwa
na kiburi cha wanadamu kitashushwa,
Mwenyezi Mungu peke yake ndiye atakayetukuzwa siku hiyo.

12 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni anayo siku aliyoiweka akiba
kwa wote wenye kujivuna na wenye kiburi,
kwa wote wanaojikweza
(nao watanyenyekezwa),

13 kwa mierezi yote ya Lebanoni iliyo mirefu sana,
na mialoni yote ya Bashani,
14 kwa milima yote mirefu
na vilima vyote vilivyoinuka,
15 kwa kila mnara ulio mrefu sana
na kila ukuta wenye ngome,
16 kwa kila meli ya biashara*,
na kila mashua ya kifahari.
17 Majivuno ya mwanadamu yatashushwa,
na kiburi cha wanadamu kitanyenyekezwa,
Mwenyezi Mungu peke yake ndiye atatukuzwa siku hiyo,
18 nazo sanamu zitatoweka kabisa.

19 Watu watakimbilia kwenye mapango ndani ya miamba,
na kwenye mahandaki ardhini
kutokana na utisho wa Mwenyezi Mungu
na utukufu wa enzi yake,
ainukapo kuitikisa dunia.
20 Siku ile, watu watawatupia
panya na popo
sanamu zao za fedha na za dhahabu,
walizozitengeneza ili waziabudu.
21 Watakimbilia kwenye mapango miambani
na kwenye nyufa za miamba
kutokana na utisho wa Mwenyezi Mungu
na utukufu wa enzi yake,
ainukapo kuitikisa dunia.

* **2:16** au *ya Tarshishi* (taz. 1 Wafalme 10:22; 22:48; 2 Nyakati 9:21; 20:36; Isaya 60:9).

22 Acheni kumtumainia mwanadamu,
ambaye hana kitu ila pumzi katika pua zake.
Yeye ana thamani gani?

# 3

*Hukumu kwa Yerusalemu na Yuda*

1 Tazama sasa, Bwana,
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
yu karibu kuwaondolea Yerusalemu na Yuda
upatikanaji wa mahitaji na misaada,
upatikanaji wote wa chakula na tegemeo lote la maji,
2 shujaa na mtu wa vita,
mwamuzi na nabii,
mwaguzi na mzee,
3 jemadari wa kikosi cha watu hamsini
na mtu mwenye cheo, mshauri,
fundi stadi na msihiri mjanja.

4 Nitawafanya wavulana wawe viongozi wao;
watoto ndio watakaowatawala.

5 Watu watadhulumiana:
mtu dhidi ya mtu, na jirani dhidi ya jirani yake.
Kijana atainuka dhidi ya mzee,
mtu mnyonge dhidi ya mtu mwenye heshima.

6 Mtu atamkamata mmoja wa ndugu zake
katika nyumba ya baba yake na kusema,
"Unalo joho, sasa uwe kiongozi wetu,

tawala lundo hili la magofu!”
7 Lakini siku hiyo atapiga kelele akisema,
“Sina msaada.
Sina chakula wala mavazi katika nyumba yangu,
msinifanye niwe kiongozi wa watu.”

8 Yerusalemu inapepesuka,
Yuda inaanguka;
maneno yao na matendo yao ni kinyume na Mwenyezi Mungu,
wakiudharau uwepo wake uliotukuka.
9 Nyuso zao zinavyoonekana zinashuhudia dhidi yao,
hujivunia dhambi yao kama Sodoma,
wala hawaifichi.
Ole wao!
Wamejiletea maafa juu yao wenyewe.

10 Waambie wanyofu itakuwa heri kwao,
kwa kuwa watafurahia tunda la matendo yao.
11 Ole kwa watu waovu! Maafa yapo juu yao!
Watalipwa kwa ajili ya yale mikono yao iliyotenda.

12 Vijana wanawatesa watu wangu,
wanawake wanawatawala.
Enyi watu wangu, viongozi wenu wanawapotosha,
wanawapoteza njia.

13 Mwenyezi Mungu anachukua nafasi yake mahakamani,
anasimama kuhukumu watu.

14 Mwenyezi Mungu anaingia katika hukumu
dhidi ya wazee na viongozi wa watu wake:
“Ninyi ndio mlioharibu shamba langu la mizabibu,
mali iliyonyang’anywa maskini imo nyumbani mwenu.
15 Mnamaanisha nini kuwaponda watu wangu
na kuzisaga nyuso za maskini?”
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

16 Mwenyezi Mungu asema,
“Wanawake wa Sayuni wana kiburi,
wanatembea na shingo ndefu,
wakikonyeza kwa macho yao,
wanatembea kwa hatua za madaha,
wakiwa na mapambo ya njuga kwenye vifundo vya miguu yao.
17 Kwa hiyo Bwana ataleta majipu kwenye vichwa vya wanawake wa Sayuni;
Mwenyezi Mungu atazifanya ngozi za vichwa vyao kuwa vipara.”

18 Katika siku ile Bwana atawanyang’anya
uzuri wao: bangili, tepe za kichwani, mikufu
yenye alama za mwezi mwandamo,
19 vipuli, vikuku, shela,
20 vilemba, mikufu ya vifundo vya miguu,
mshipi, chupa za manukato na hirizi,
21 pete zenye muhuri, pete za puani,
22 majoho mazuri, mitandio, mavazi, kifuko
cha kutilia fedha,
23 vioo, mavazi ya kitani, taji na shali.

24 Badala ya harufu ya manukato kutakuwa na uvundo;
badala ya mishipi, ni kamba;
badala ya nywele zilizotengenezwa vizuri, ni upara;
badala ya mavazi mazuri, ni magunia;
badala ya uzuri, ni alama ya aibu kwa chuma cha moto.
25 Wanaume wako watauawa kwa upanga,
nao mashujaa wako watauawa vitani.
26 Malango ya Sayuni yataomboleza na kulia,
ataketi mavumbini akiwa fukara.

# 4

1 Katika siku ile wanawake saba
watamshika mwanaume mmoja
wakisema, "Tutakula chakula chetu wenyewe
na kuvaa nguo zetu wenyewe,
ila wewe uturuhusu tu tuitwe kwa jina lako.
Utuondolee aibu yetu!"

*Tawi la Mwenyezi Mungu*

2 Katika siku ile Tawi la Mwenyezi Mungu
litakuwa zuri na lenye utukufu, nalo tunda la
nchi litakuwa fahari na utukufu wa wale Wais-
raeli watakaonusurika.
3 Wale watakaoachwa Sayuni, watakaobaki
Yerusalemu, wataitwa watakatifu, wale wote am-
bao wameorodheshwa miongoni mwa walio hai
huko Yerusalemu.
4 Bwana atausafisha uchafu wa wanawake
wa Sayuni, atatakasa madoa ya damu kutoka
Yerusalemu kwa Roho ya hukumu na Roho ya
moto.

5 Kisha Mwenyezi Mungu ataumba juu ya
Mlima wote wa Sayuni, na juu ya wale wote
wanaokusanyika hapo, wingu la moshi wakati
wa mchana, na kung'aa kwa miali ya moto
wakati wa usiku; nako juu ya huo utukufu wote
kutatanda kifuniko cha ulinzi.
6 Utakuwa sitara na kivuli kutokana na joto la
mchana, na kuwa mahali pa kujificha kutokana
na dhoruba na mvua.

# 5

*Wimbo wa shamba la mizabibu*

1 Nitaimba wimbo kwa mpenzi wangu,
wimbo kuhusu shamba lake la mizabibu:
Mpenzi wangu alikuwa na shamba la mizabibu
kwenye kilima chenye rutuba.
2 Alililima na kuondoa mawe
na akaliotesha mizabibu bora sana.
Akajenga mnara wa ulinzi ndani yake,
na kutengeneza shinikizo la kukamulia zabibu pia.
Kisha akatazamia kupata mazao ya zabibu nzuri,
lakini lilizaa matunda mabaya tu.

3 "Basi enyi wakazi wa Yerusalemu na watu wa Yuda,
hukumuni kati yangu na shamba langu la mizabibu.
4 Ni nini zaidi ambacho kingefanyika katika shamba langu la mizabibu
kuliko yale niliyofanya?
Nilipotazamia kupata zabibu nzuri,
kwa nini lilizaa zabibu mbaya tu?
5 Sasa nitawaambia lile nitakalolitendea

shamba langu la mizabibu:
Nitaondoa uzio wake,
nalo litaharibiwa,
nitabomoa ukuta wake,
nalo litakanyagwa.
6 Nitalifanya nchi ya ukiwa isiyokaliwa na watu,
halitakatiwa matawi wala kulimwa,
nayo michongoma na miiba itamea huko,
nitaamuru mawingu yasinyeshe mvua juu yake.”

7 Shamba la mzabibu la Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
ni nyumba ya Israeli,
na watu wa Yuda
ni bustani yake ya kumpendeza.
Alitazamia haki, lakini akaona umwagaji damu;
alitazamia uadilifu, lakini akasikia vilio vya taabu.

*Ole na hukumu*

8 Ole wenu mnaoongeza nyumba baada ya nyumba
na kuunganisha mashamba baada ya mashamba
hadi hakuna nafasi iliyobaki,
nanyi mnaishi peke yenu katika nchi.
9 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni amesema nikisikia:
“Hakika nyumba kubwa zitakuwa ukiwa,
nayo majumba ya fahari yatabaki bila kukaliwa.
10 Shamba la mizabibu la eka kumi

litatoa bathi moja* ya divai,
na homeri moja† ya mbegu zilizopandwa
itatoa efa moja‡ tu ya nafaka."

11 Ole wao wale waamkao asubuhi na mapema
wakikimbilia kunywa vileo,
wale wakawiao sana hadi usiku,
hata wamewaka kwa mvinyo.
12 Wana vinubi na zeze kwenye karamu zao,
matari, filimbi na mvinyo,
lakini hawayajali matendo ya Mwenyezi Mungu,
wala hawana heshima kwa ajili ya kazi ya mikono yake.
13 Kwa hiyo watu wangu wataenda uhamishoni
kwa sababu ya kukosa maarifa;
watu wao wenye vyeo watakufa kwa njaa,
nao watu wengi watakauka kwa kiu.
14 Kwa hiyo Kaburi§ limeongeza hamu yake
na kupanua mdomo wake bila kikomo,
ndani yake watashuka wakuu wao na wingi wa watu,
pamoja na wagomvi wao, na wafanyao sherehe wote.
15 Hivyo mwanadamu atashushwa,
na binadamu kunyenyekezwa,
macho ya wenye majivuno yatanyenyekezwa.
16 Lakini Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni atatukuzwa

* **5:10** Bathi moja ni sawa na lita 22. † **5:10** Homeri moja ni sawa na lita 220. ‡ **5:10** Efa moja ni sawa na lita 22. § **5:14** Kaburi hapa maana yake ni *Kuzimu*; kwa Kiebrania ni *Sheol.*

kwa ajili ya haki yake,
naye Mungu Mtakatifu atajionesha mwenyewe
kuwa mtakatifu kwa haki yake.
17 Kondoo watajilisha kwenye malisho yao wenyewe,
wana-kondoo watajilisha katika magofu ya matajiri.

18 Ole wao wanaovuta dhambi kwa kamba za udanganyifu
na uovu kama kwa kamba za mkokoteni,
19 kwa wale wanaosema, "Mungu na afanye haraka,
aharakishe kazi yake ili tupate kuiona.
Huo mpango wa Aliye Mtakatifu wa Israeli na ukamilike,
tena udhihirike ili tupate kuujua."

20 Ole wao wanaoita ubaya ni wema,
na wema ni ubaya,
wawekao giza badala ya nuru,
na nuru badala ya giza,
wawekao uchungu badala ya utamu,
na utamu badala ya uchungu.

21 Ole wao walio na hekima machoni pao wenyewe,
na kujiona wenye akili machoni pao wenyewe.

22 Ole wao walio mashujaa kwa kunywa mvinyo,
nao walio hodari katika kuchanganya vileo,

23 wale wanaoachilia wenye hatia kwa kupokea hongo,
lakini huwanyima haki wasio na hatia.
24 Kwa hiyo, kama ndimi za moto zinavyoteketeza nyasi,
na kama vile majani makavu yanavyozama katika miali ya moto,
ndivyo mizizi yao itakavyooza,
na maua yao yatakavyopeperushwa kama mavumbi;
kwa kuwa wameikataa Torati ya Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni
na kulisukumia mbali neno la
Aliye Mtakatifu wa Israeli.
25 Kwa hiyo hasira ya Mwenyezi Mungu
inawaka dhidi ya watu wake,
mkono wake umeinuliwa na anawapiga.
Milima inatetemeka,
maiti ni kama takataka kwenye barabara.

Hata kwa haya yote, hasira yake haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa juu.

26 Yeye anainua bendera kwa ajili ya mataifa yaliyo mbali,
anapiga filimbi kwa ajili ya wale walio kwenye miisho ya dunia.
Tazama wamekuja,
kwa kasi na kwa haraka!
27 Hakuna hata mmoja wao anayechoka wala kujikwaa,

hakuna hata mmoja anayesinzia wala kulala,
hakuna mkanda uliolegezwa kiunoni,
hakuna gidamu ya kiatu iliyokatika.
28 Mishale yao ni mikali,
pinde zao zote zimevutwa,
kwato za farasi wao ziko kama gumegume,
magurudumu ya magari yao ya vita ni kama upepo wa kisulisuli.
29 Ngurumo yao ni kama ile ya simba,
wananguruma kama wana simba,
wanakoroma wanapokamata mawindo yao,
na kuondoka nayo pasipo yeyote wa kuokoa.
30 Katika siku ile watanguruma juu yake
kama ngurumo za bahari.
Kama mtu akiitazama nchi,
ataona giza na dhiki;
hata nuru itatiwa giza kwa mawingu.

# 6

*Agizo kwa Isaya*

1 Katika mwaka ule Mfalme Uzia alikufa, nilimwona Bwana ameketi kwenye kiti cha enzi, kilicho juu na kilichotukuzwa sana, nalo pindo la joho lake likajaza Hekalu.
2 Juu yake walikuwa maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita: Kwa mabawa mawili walifunika nyuso zao, kwa mengine mawili walifunika miguu yao, na kwa mawili walikuwa wakiruka.
3 Nao walikuwa wakiitana kila mmoja na mwenzake:
“Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu

ni Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni;
dunia yote imejaa utukufu wake."
4 Kwa sauti zao, miimo ya milango na vizingiti
vilitikisika, nalo Hekalu likajaa moshi.

5 Ndipo nikalia, "Ole wangu! Nimeangamia!
Kwa kuwa mimi ni mtu mwenye midomo
michafu, nami ninaishi kati ya watu wenye
midomo michafu, nayo macho yangu yamem-
wona Mfalme, Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni."

6 Ndipo mmoja wa wale maserafi akaruka ku-
nijia akiwa na kaa la moto linalowaka mkononi
mwake, ambalo alikuwa amelichukua kwa koleo
kutoka madhabahuni.
7 Akanigusa nalo kinywa changu na kusema,
"Tazama, hili limegusa midomo yako, uovu
wako umeondolewa, nayo dhambi yako ime-
samehewa."
8 Kisha nikasikia sauti ya Bwana ikisema, "Nim-
tume nani? Ni nani atakayeenda kwa ajili yetu?"

Nami nikasema, "Mimi hapa. Nitume mimi!"

9 Akasema, "Nenda ukawaambie watu hawa:
" 'Mtaendelea daima kusikiliza,
lakini kamwe hamtaelewa;
mtaendelea daima kutazama,
lakini kamwe hamtatambua.'
10 Fanya mioyo ya watu hawa kuwa migumu,
fanya masikio yao yasisikie,
na upofushe macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
na wakasikiliza kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao,

nao wakageuka, wakaponywa."
11 Ndipo nikasema, "Hadi lini, Ee Bwana?"
Naye akanijibu:
"Hadi miji iwe imeachwa magofu
na bila wakazi,
hadi nyumba zitakapobaki bila watu,
na mashamba yatakapoharibiwa na kuangamizwa,
12 hadi Mwenyezi Mungu atakapokuwa amekwisha kumpeleka kila mmoja mbali sana,
na nchi itakapokuwa imeachwa kabisa.
13 Hata kama sehemu ya kumi ya watu watabaki katika nchi,
itaharibiwa tena.
Lakini kama vile mvinje au mwaloni
ubakizavyo visiki unapokatwa,
ndivyo mbegu takatifu
itakavyokuwa kisiki katika nchi."

# 7

## *Ishara ya Imanueli*

1 Ahazi mwana wa Yothamu, mwana wa Uzia,
alipokuwa mfalme wa Yuda, Mfalme Resini wa
Aramu*, na Peka mwana wa Remalia mfalme wa
Israeli walipanda kupigana dhidi ya Yerusalemu,
lakini hawakuweza kuushinda.
2 Wakati huu nyumba ya Daudi iliambiwa,
"Aramu wameungana na Efraimu." Kwa hiyo
mioyo ya Ahazi na watu wake ilitikiswa, kama
miti ya msituni inavyotikiswa na upepo.

* **7:1** yaani *Shamu*

3 Ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia Isaya,
“Toka uende, wewe na mwanao Shear-Yashubu†,
mkutane na Ahazi huko mwisho wa mfereji wa
Bwawa la Juu, kwenye barabara iendayo Shamba
la Dobi.
4 Mwambie, ‘Uwe mwangalifu, utulie na usio-
gope. Usife moyo kwa ajili ya watu hawa wawili
walio kama visiki vya kuni vifukavyo moshi, kwa
ajili ya hasira kali ya Resini na Aramu na ya
mwana wa Remalia.
5 Aramu, Efraimu na mwana wa Remalia
wamepanga njama ili wakuangamize, wakisema,
6 “Tuishambulie Yuda, naam, tuirarue vipande
vipande na kuigawa miongoni mwetu, na
kumtawaza mwana wa Tabeeli awe mfalme
juu yake.”
7 Lakini Bwana Mungu Mwenyezi asema hivi:
“ ‘Jambo hili halitatendeka,
halitatukia,
8 kwa kuwa kichwa cha Aramu ni Dameski,
na kichwa cha Dameski ni Resini peke yake.
Katika muda wa miaka sitini na tano,
Efraimu atakuwa ameharibiwa
kiasi kwamba hataweza tena kuwa taifa.
9 Kichwa cha Efraimu ni Samaria,
na kichwa cha Samaria
ni mwana wa Remalia peke yake.
Kama hamtasimama thabiti katika imani yenu,
hamtaimarika kamwe.’ ”
10 Mwenyezi Mungu akasema na Ahazi tena,
11 “Mwombe Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
ishara, iwe kwenye vina virefu sana, au kwenye
vimo virefu sana.”

† **7:3** maana yake *Mabaki Watarudi*

12 Lakini Ahazi akasema, “Sitaomba; sitam-
jaribu Mwenyezi Mungu.”
13 Ndipo Isaya akasema, “Sikia sasa, ewe
nyumba ya Daudi! Je, haitoshi kujaribu uvu-
milivu wa wanadamu? Je, mtaujaribu uvumilivu
wa Mungu wangu pia?
14 Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara:
Bikira atachukua mimba, naye atamzaa mwana,
na ataitwa Imanueli‡.
15 Atakula jibini na asali atakapokuwa
ameweza kukataa mabaya na kuchagua mema.
16 Lakini kabla mtoto hajajua kukataa mabaya
na kuchagua mema, nchi ya wafalme hao wawili
unaowaogopa itafanywa ukiwa.
17 Mwenyezi Mungu ataleta juu yako pamoja
na watu wako na juu ya nyumba ya baba
yako, nyakati ambazo hazijawahi kuwako tangu
Efraimu alipojitenga na Yuda: naye Mwenyezi
Mungu atawaleteeni mfalme wa Ashuru.”
18 Katika siku ile Mwenyezi Mungu atawapigia
filimbi inzi kutoka vijito vya mbali vya Misri, na
nyuki kutoka nchi ya Ashuru.
19 Wote watakuja na kukaa kwenye mabonde
yenye miteremko, na kwenye nyufa za miamba,
kwenye vichaka vyote vyenye miiba, na kwenye
mashimo yote ya maji.
20 Katika siku ile Bwana atatumia wembe ulioa-
jiriwa kutoka ng'ambo ya Mto§, yaani mfalme
wa Ashuru, kunyoa nywele za kichwa chako na
malaika ya miguu yako, na kuziondoa ndevu
zako pia.

‡ **7:14** maana yake *Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi* § **7:20** yaani *Mto Frati*

21 Katika siku ile, mtu atahifadhi hai mtamba
mmoja na kondoo wawili.
22 Kwa ajili ya wingi wa maziwa watakayotoa,
atapata jibini ya kula. Wote watakaobakia katika
nchi watakula jibini na asali.
23 Katika siku ile, kila mahali palipokuwa na
mizabibu elfu moja yenye thamani ya shekeli elfu
moja* za fedha, patakuwa na michongoma na
miiba tu.
24 Watu wataenda huko wakiwa na upinde na
mshale, kwa maana nchi itafunikwa na michon-
goma na miiba.
25 Kuhusu vilima vyote vilivyokuwa vikilimwa
kwa jembe, hamtaenda huko tena kwa ajili ya
hofu ya michongoma na miiba. Patakuwa mahali
ng'ombe wataachiwa huru, na kondoo kukimbia
kimbia.

# 8

## *Isaya na wanawe kama ishara*

1 Mwenyezi Mungu akaniambia, "Chukua
kitabu kikubwa, uandike kwa kalamu ya
kawaida jina: Maher-Shalal-Hash-Bazi*.
2 Nami nitawaita kuhani Uria, na Zekaria
mwana wa Yeberekia kama mashahidi wangu
waaminifu."
3 Kisha nikaenda kwa nabii mke, naye akapata
mimba, akazaa mwana. Kisha Mwenyezi Mungu
akaniambia, "Mwite huyo mtoto Maher-Shalal-
Hash-Bazi.

---

* **7:23** Shekeli 1,000 ni kama kilo 11.5. * **8:1** maana yake *Haraka kuteka nyara, upesi kwenye hizo nyara*

4 Kabla mtoto hajaweza kusema 'Baba yangu' au 'Mama yangu,' utajiri wa Dameski na nyara za Samaria zitachukuliwa na mfalme wa Ashuru."
5 Mwenyezi Mungu akasema nami tena:

6 "Kwa sababu watu hawa wamekataa maji ya Shilo yanayotiririka taratibu
wakamfurahia Resini na mwana wa Remalia;
7 kwa hiyo Bwana yu karibu kuleta dhidi yao
mafuriko makubwa ya Mto†:
yaani mfalme wa Ashuru na fahari yake yote.
Yatafurika juu ya mifereji yake yote,
yatamwagikia juu ya kingo zake zote,
8 na kufika hadi Yuda, yakizunguka kwa kasi juu yake,
yakipita katikati na yakifika hadi shingoni.
Mabawa yake yaliyokunjuliwa
yatafunika upana wa nchi yako,
Ee Imanueli‡!"

9 Inueni ukelele wa vita, enyi mataifa,
na mkavunjwevunjwe!
Sikilizeni, enyi nyote nchi za mbali.
Jiandaeni kwa vita, nanyi mkavunjwevunjwe!
Jiandaeni kwa vita, nanyi mkavunjwevunjwe!
10 Wekeni mikakati yenu, lakini itashindwa;
fanyeni mipango yenu, lakini haitafanikiwa,
kwa maana Mungu yu pamoja nasi§.

† **8:7** yaani *Mto Frati* ‡ **8:8** maana yake *Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi* § **8:10** Kiebrania ni *Imanueli*

11 Mwenyezi Mungu alisema nami mkono wake
wenye nguvu ukiwa juu yangu, akinionya nisifu-
ate njia za taifa hili. Akasema:

12 "Usiite fitina kila kitu ambacho watu hawa hukiita fitina,
usiogope kile wanachokiogopa,
wala usikihofu.
13 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ndiye peke yake
ikupasaye kumheshimu kuwa mtakatifu,
ndiye peke yake utakayemwogopa,
ndiye peke yake utakayemhofu,
14 naye atakuwa mahali patakatifu;
lakini kwa nyumba zote mbili za Israeli atakuwa
jiwe lile linalosababisha watu kujikwaa
na mwamba wa kuwaangusha.
Kwa watu wa Yerusalemu,
atakuwa mtego na tanzi.
15 Wengi wao watajikwaa;
wataanguka na kuvunjika,
watategwa na kunaswa."

16 Funga ushuhuda na kutia muhuri sheria
miongoni mwa wanafunzi wangu.
17 Nitamngojea Mwenyezi Mungu,
ambaye ameificha nyumba ya Yakobo uso wake.
Nitaliweka tumaini langu kwake.

18 Niko hapa, pamoja na watoto ambao
Mwenyezi Mungu amenipa. Sisi ni ishara na
mfano wake katika Israeli, kutoka kwa Mwenyezi

Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, anayeishi juu ya Mlima Sayuni.

19 Watu wanapowaambia ninyi kutafuta
ushauri kwa waaguzi na wenye kuongea na
mizimu, ambao hunong'ona na kunung'unika,
je, watu wasingeuliza kwa Mungu wao? Kwa
nini watake shauri kwa wafu kwa ajili ya walio
hai?
20 Kwa sheria na kwa ushuhuda! Kama
hawatasema sawasawa na neno hili, hawana
mwanga wa mapambazuko.
21 Watazunguka katika nchi yote, wakiwa na
dhiki na njaa. Watakapotaabika kwa njaa, wat-
apatwa na hasira kali, nao, wakiwa wanatazama
juu, watamlaani mfalme wao na Mungu wao.
22 Kisha wataangalia duniani na kuona tu dhiki
na giza, hofu na huzuni tupu, nao watasukumiwa
kwenye giza nene kabisa.

# 9

### *Mtoto amezaliwa kwa ajili yetu*

1 Hata hivyo, hakutakuwa huzuni tena kwa wale waliokuwa katika dhiki. Hapo awali aliidhili nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, lakini katika siku zijazo ataipa heshima Galilaya ya Mataifa, karibu na njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani:

2 Watu wanaotembea katika giza
wameona nuru kuu,
wale wanaoishi katika nchi ya uvuli wa mauti,
nuru imewazukia.
3 Umelikuza taifa,
na kuzidisha furaha yao,

wanafurahia mbele zako,
kama watu wanavyofurahia wakati wa mavuno,
kama mashujaa wanavyofurahia
wakigawanya nyara.
4 Kama vile siku ya kushindwa kwa Wamidiani,
umevunja nira iliyowalemea,
ile gongo mabegani mwao
na fimbo ya aliyewadhulumu.
5 Kila kiatu cha shujaa kilichotumiwa vitani,
na kila vazi lililovingirishwa katika damu
vitawekwa kwa ajili ya kuchomwa,
vitakuwa kuni za kuwasha moto.
6 Kwa maana, kwa ajili yetu mtoto amezaliwa,
tumepewa mtoto wa kiume,
nao utawala utakuwa begani mwake.
Naye ataitwa
Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye Nguvu,
Baba wa Milele, Mfalme wa Amani.
7 Kuongezeka kwa utawala wake na amani
hakutakuwa na mwisho.
Atatawala kwenye kiti cha utawala cha Daudi
na juu ya ufalme wake,
akiuthibitisha na kuutegemeza
kwa haki na kwa adili,
tangu wakati huo na hata milele.
Wivu wa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
utatimiza haya.

### *Hasira ya Mwenyezi Mungu dhidi ya Israeli*

8 Bwana ametuma ujumbe dhidi ya Yakobo,
utamwangukia Israeli.
9 Watu wote watajua hili:

Efraimu na wakazi wa Samaria,
wanaosema kwa kiburi
na majivuno ya mioyo,
10 “Matofali yameanguka chini,
lakini tutajenga tena kwa mawe yaliyochongwa,
mikuyu imekatwa,
na tutapanda mierezi badala yake.”
11 Lakini Mwenyezi Mungu amemtia nguvu adui wa Resini dhidi yao
na kuchochea watesi wao.
12 Waaramu kutoka upande wa mashariki
na Wafilisti kutoka upande wa magharibi
wameila Israeli kwa kinywa kilichopanuliwa.

Hata kwa haya yote, hasira yake haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa juu.

13 Lakini watu hawajamrudia yeye aliyewapiga,
wala hawajamtafuta Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni.
14 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu atakatilia mbali kutoka Israeli kichwa na mkia,
tawi la mtende na tete katika siku moja.
15 Wazee na watu mashuhuri ndio vichwa,
nao manabii wanaofundisha uongo ndio mkia.
16 Wale wanaowaongoza watu hawa wanawapotosha,
nao wale wanaoongozwa wamepotoka.
17 Kwa hiyo Bwana hatawafurahia vijana,
wala hatawahurumia yatima na wajane,

kwa kuwa kila mmoja wao hamchi Mungu, nao ni waovu,
na kila kinywa kinanena upumbavu.

Hata kwa haya yote, hasira yake haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa juu.

18 Hakika uovu huwaka kama moto;
huteketeza michongoma na miiba,
huwasha moto vichaka vya msituni,
hujiviringisha kuelekea juu kama nguzo ya moshi.
19 Kwa hasira ya Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
nchi itachomwa kwa moto,
nao watu watakuwa kuni za kuchochea moto.
Hakuna mtu atakayemhurumia ndugu yake.
20 Upande wa kuume watakuwa wakitafuna,
lakini bado wataona njaa;
upande wa kushoto watakuwa wakila,
lakini hawatashiba.
Kila mmoja atajilisha kwa nyama ya uzao wake mwenyewe:
21 Manase atamla Efraimu,
naye Efraimu atamla Manase;
nao pamoja watakuwa kinyume na Yuda.

Hata kwa haya yote, hasira yake haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa juu.

# 10

1 Ole wao wawekao sheria zisizo za haki,
kwa wale watoao amri za kuonea,
2 kuwanyima maskini haki zao
na kuzuilia haki za watu wangu waliodhulumiwa,
kuwafanya wajane mawindo yao
na kuwanyang'anya yatima.
3 Mtafanya nini siku ya hukumu,
wakati maafa yatakapokuja kutoka mbali?
Mtamkimbilia nani awape msaada?
Mtaacha wapi mali yenu?
4 Hakutasalia kitu chochote,
isipokuwa kujikunyata miongoni mwa mateka,
au kuanguka miongoni mwa waliouawa.

Hata kwa haya yote, hasira yake haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa juu.

### *Hukumu ya Mwenyezi Mungu juu ya Ashuru*

5 "Ole kwa Ashuru, fimbo ya hasira yangu,
ambaye mkononi mwake ana rungu ya ghadhabu yangu!
6 Ninamtuma dhidi ya taifa lisilomjua Mungu,
ninamtuma dhidi ya taifa linalonikasirisha,
kukamata mateka na kunyakua nyara,
pia kuwakanyaga chini kama matope ya barabarani.
7 Lakini hili silo analokusudia,
hili silo alilo nalo akilini;
kusudi lake ni kuangamiza,
kuyakomesha mataifa mengi.

8 Maana asema, 'Je, wafalme wote
si majemadari wangu?
9 Je, Kalno hakutendwa kama Karkemishi?
Hamathi si kama Arpadi,
nayo Samaria si kama Dameski?
10 Kama vile mkono wangu ulivyotwaa falme za sanamu,
falme ambazo vinyago vyao vilizidi vile vya Yerusalemu na Samaria:
11 je, nisiutendee Yerusalemu na sanamu zake
kama nilivyoutendea Samaria na vinyago vyake?' "

12 Bwana atakapokuwa amemaliza kazi yake
yote dhidi ya Mlima Sayuni na Yerusalemu,
atasema, "Nitamwadhibu mfalme wa Ashuru
kwa ajili ya majivuno ya ukaidi wa moyo wake
na kutazama kwa macho yenye dharau."

13 Kwa kuwa anasema:
" 'Kwa nguvu za mkono wangu nimefanya hili,
kwa hekima yangu, kwa sababu nina ufahamu.
Niliondoa mipaka ya mataifa,
niliteka nyara hazina zao,
kama yeye aliye shujaa
niliwatiisha wafalme wao.
14 Kama mtu atiavyo mkono kwenye kiota,
ndivyo mkono wangu ulivyochukua utajiri wa mataifa;
kama watu wakusanyavyo mayai yaliyoachwa,
ndivyo nilivyokusanya nchi zote;
wala hakuna hata mmoja aliyepiga bawa
au kufungua kinywa chake kutoa mlio.' "

15 Je, shoka laweza kujigamba kuwa na nguvu

kuliko yule anayelitumia,
au msumeno kujisifu
dhidi ya yule anayeutumia?
Ni kana kwamba fimbo ingeweza kumwinua yeye aichukuaye,
au mkongojo ungemwinua mwenye kuutumia!
16 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
atatuma ugonjwa wa kudhoofisha
kwa mashujaa wake wanene,
katika fahari yake moto utawaka
kama mwali wa moto.
17 Nuru ya Israeli itakuwa moto,
Aliye Mtakatifu wao mwali wa moto;
katika siku moja utaunguza na kuteketeza miiba
na michongoma yake.
18 Fahari ya misitu yake na mashamba yenye rutuba
utateketeza kabisa,
kama vile mtu mgonjwa adhoofikavyo.
19 Nayo miti inayobaki katika misitu yake itakuwa michache sana
hata mtoto mdogo angeweza kuihesabu.

### *Mabaki ya Israeli*

20 Katika siku ile, mabaki ya Israeli,
walionusurika wa nyumba ya Yakobo,
hawatamtegemea tena yeye aliyewapiga,
lakini watamtegemea kwa kweli
Mwenyezi Mungu Aliye Mtakatifu wa Israeli.
21 Mabaki watarudi*, mabaki wa Yakobo

* **10:21** Kiebrania ni *Shear-Yashubu*; pia 10:22.

watamrudia Mungu Mwenye Nguvu.
22 Ingawa watu wako, ee Israeli,
ni wengi kama mchanga wa pwani,
ni mabaki yao tu watakaorudi.
Maangamizi yamekwisha amriwa,
ni mengi tena ni haki.
23 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, atatekeleza
maangamizi yaliyoamriwa juu ya nchi yote.
24 Kwa hiyo, hili ndilo asemalo Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni:
"Enyi watu wangu mnaoishi Sayuni,
msiwaogope Waashuru,
wanaowapiga ninyi kwa fimbo
na kuinua rungu dhidi yenu, kama Misri ilivyofanya.
25 Bado kitambo kidogo sana hasira yangu dhidi yenu itakoma,
na ghadhabu yangu itaelekezwa kwenye maangamizi yao."

26 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni atawachapa kwa mjeledi,
kama alivyowapiga Wamidiani katika mwamba wa Orebu,
naye atainua fimbo yake juu ya maji,
kama alivyofanya huko Misri.
27 Katika siku hiyo mzigo wao utainuliwa kutoka mabegani mwenu,
na nira yao kutoka shingoni mwenu;
nira itavunjwa
kwa sababu ya kupakwa mafuta.

28 Wanaingia Ayathi,
wanapita katikati ya Migroni,
wanahifadhi mahitaji huko Mikmashi.
29 Wanavuka kivukoni, nao wanasema,
"Tutapiga kambi huko Geba usiku kucha."
Rama inatetemeka;
Gibea ya Sauli inakimbia.
30 Piga kelele, ee Binti Galimu!
Sikiliza, ee Laisha!
Maskini Anathothi!
31 Madmena inakimbia;
watu wa Gebimu wanajificha.
32 Siku hii ya leo watasimama Nobu;
watatikisa ngumi zao
kwa mlima wa Binti Sayuni,
kwa kilima cha Yerusalemu.

33 Tazama, Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
atayakata matawi kwa nguvu kuu.
Miti mirefu sana itaangushwa,
ile mirefu itashushwa chini.
34 Atakata vichaka vya msitu kwa shoka;
Lebanoni itaanguka mbele zake yeye Mwenye Nguvu.

# 11

*Tawi kutoka kwa Yese*

1 Chipukizi litatokea kutoka shina la Yese,
kutoka mizizi yake Tawi litazaa tunda.
2 Roho wa Mwenyezi Mungu atakaa juu yake,
Roho wa hekima na wa ufahamu,
Roho wa shauri na wa uweza,

Roho wa maarifa na wa kumcha Mwenyezi Mungu
3 naye atafurahia kumcha Mwenyezi Mungu.

Hatahukumu kwa yale ayaonayo kwa macho yake,
wala kuamua kwa yale ayasikiayo kwa masikio yake,
4 bali kwa uadilifu atahukumu wahitaji,
kwa haki ataamua wanyenyekevu wa dunia.
Ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake,
kwa pumzi ya midomo yake atawaua waovu.
5 Haki itakuwa mkanda wake
na uaminifu utakuwa mshipi kiunoni mwake.

6 Mbwa-mwitu ataishi pamoja na mwana-kondoo,
naye chui atalala pamoja na mbuzi,
ndama, mwana simba na ng'ombe wa mwaka mmoja
watakaa pamoja,
naye mtoto mdogo atawaongoza.
7 Ng'ombe na dubu watalisha pamoja,
watoto wao watalala pamoja,
na simba atakula majani makavu kama maksai.
8 Mtoto mchanga atacheza karibu na shimo la nyoka,
naye mtoto mdogo ataweka mkono wake
kwenye kiota cha fira.
9 Hawatadhuru wala kuharibu
juu ya mlima wangu mtakatifu wote,

kwa kuwa dunia itajawa na kumjua Mwenyezi Mungu
kama maji yajazavyo bahari.
10 Katika siku hiyo, Shina la Yese atasi-
mama kama bendera kwa ajili ya mataifa.
Mataifa yatakusanyika kwake, na mahali pake pa
kupumzikia patakuwa utukufu.
11 Katika siku hiyo Bwana atanyoosha mkono
wake mara ya pili kurudisha mabaki ya watu
wake waliosalia kutoka Ashuru, Misri, Pathrosi*,
Kushi, Elamu, Babeli, Hamathi, na kutoka visiwa
vya baharini.
12 Atainua bendera kwa mataifa
na kuwakusanya Waisraeli walio uhamishoni;
atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika
kutoka pembe nne za dunia.
13 Wivu wa Efraimu utatoweka,
na adui wa Yuda watakatiliwa mbali;
Efraimu hatamwonea Yuda wivu,
wala Yuda hatakuwa na uadui na Efraimu.
14 Watawashukia katika miteremko ya Wafilisti
hadi upande wa magharibi,
kwa pamoja watawateka watu nyara
hadi upande wa mashariki.
Watawapiga Edomu na Moabu,
na Waamoni watatawaliwa nao.
15 Mwenyezi Mungu atakausha
ghuba ya bahari ya Misri;
kwa upepo mkavu ataupeleka mkono wake
juu ya Mto Frati.
Ataugawanya katika vijito saba

* **11:11** yaani *Misri ya Juu*

ili watu waweze kuuvuka wakiwa wamevaa viatu.
16 Kutakuwa na njia kuu kwa mabaki ya watu wake
wale waliosalia kutoka Ashuru,
kama ilivyokuwa kwa Israeli
walipopanda kutoka Misri.

# 12

*Kushukuru na kusifu*

1 Katika siku ile utasema:
"Nitakusifu wewe, Ee Mwenyezi Mungu.
Ingawa ulinikasirikia,
hasira yako imegeukia mbali
nawe umenifariji.
2 Hakika Mungu ni wokovu wangu;
nitamtumaini wala sitaogopa.
Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu,
ni nguvu zangu na wimbo wangu;
amekuwa wokovu wangu."
3 Kwa furaha mtachota maji
kutoka visima vya wokovu.
4 Katika siku hiyo mtasema:
"Mshukuruni Mwenyezi Mungu, mliitie jina lake;
julisheni miongoni mwa mataifa yale aliyoyafanya,
tangazeni kuwa jina lake limetukuka.
5 Mwimbieni Mwenyezi Mungu, kwa kuwa ametenda mambo makuu,
hili na lijulikane duniani kote.
6 Pazeni sauti mwimbe kwa furaha, watu wa Sayuni,

kwa maana mkuu ni yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli miongoni mwenu."

# 13

### *Unabii dhidi ya Babeli*

1 Neno la unabii kuhusu Babeli ambalo Isaya mwana wa Amozi aliliona:
2 Twekeni bendera juu ya mlima usio na kitu,
wapazieni sauti,
wapungieni mkono waingie
katika malango ya wenye heshima.
3 Nimewaamuru watakatifu wangu;
nimewaita mashujaa wangu waitimize hasira yangu:
wale wanaoshangilia ushindi wangu.

4 Sikilizeni kelele juu ya milima,
kama ile ya umati mkubwa wa watu!
Sikilizeni, makelele katika falme,
kama mataifa yanayokusanyika pamoja!
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni anakusanya
jeshi kwa ajili ya vita.
5 Wanakuja kutoka nchi za mbali sana,
kutoka miisho ya mbingu,
Mwenyezi Mungu na silaha za ghadhabu yake,
kuangamiza nchi yote.

6 Ombolezeni, kwa maana siku ya Mwenyezi Mungu i karibu,

itakuja kama uharibifu kutoka kwa Mwenyezi*.
7 Kwa sababu ya hili, mikono yote italegea,
moyo wa kila mtu utayeyuka.
8 Hofu itawakamata,
uchungu na maumivu makali yatawashika,
watagaagaa kama mwanamke aliye na uchungu wa kuzaa.
Watatazamana kwa hofu kila mtu na mwenzake,
nyuso zao zikiwaka kama moto.

9 Tazameni, siku ya Mwenyezi Mungu inakuja,
siku katili, yenye ghadhabu na hasira kali,
kuifanya nchi kuwa ukiwa,
na kuwaangamiza wenye dhambi waliomo.
10 Nyota za mbinguni na makundi ya nyota havitatoa mwanga wake.
Jua linalochomoza litatiwa giza
na mwezi hautatoa nuru yake.
11 Nitauadhibu ulimwengu kwa ajili ya uovu wake,
waovu kwa ajili ya dhambi zao.
Nitakomesha majivuno ya wenye kiburi,
na nitakishusha kiburi cha watu wakatili.
12 Nitawafanya wanadamu kuwa adimu kuliko dhahabu safi,
watakuwa wachache sana kuliko dhahabu ya Ofiri.
13 Kwa hiyo nitazifanya mbingu zitetemeke,
nayo dunia itatikisika kutoka mahali pake
katika ghadhabu ya Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni,

* **13:6** Mwenyezi hapa ina maana ya *Shaddai* kwa Kiebrania.

katika siku ya hasira yake iwakayo.

14 Kama paa awindwaye,
kama kondoo wasio na mchungaji,
kila mmoja atarudi kwa watu wake mwenyewe,
kila mmoja atakimbilia nchi yake ya kuzaliwa.
15 Yeyote atakayetekwa atapasuliwa tumbo,
wote watakaokamatwa watauawa kwa upanga.
16 Watoto wao wachanga watavunjwa vipande vipande
mbele ya macho yao;
nyumba zao zitatekwa,
na wake zao watanajisiwa.

17 Tazama, nitawachochea Wamedi dhidi yao,
ambao hawajali fedha
wala hawafurahii dhahabu.
18 Mishale yao itawaangusha vijana,
hawatakuwa na huruma kwa watoto wachanga
wala hawataangalia watoto kwa huruma.
19 Babeli, johari ya falme,
utukufu wa kiburi cha Wababeli†,
utaangushwa na Mungu
kama Sodoma na Gomora.
20 Hautakaliwa na watu kamwe,
wala watu hawataishi humo kwa vizazi vyote.
Hakuna Mwarabu atakayepiga hema lake huko,
hakuna mchungaji atakayepumzisha makundi yake huko.

† **13:19** yaani Wakaldayo

21 Lakini viumbe wa jangwani watalala huko,
mbweha watajaza nyumba zake,
bundi wataishi humo
nao mbuzi-mwitu watarukaruka humo.
22 Fisi watalia ndani ya ngome zake,
mbweha ndani ya majumba yake ya kifahari.
Wakati wake umewadia,
na siku zake hazitaongezwa.

# 14

*Yuda kufanywa upya*

1 Mwenyezi Mungu atamhurumia Yakobo,
atamchagua Israeli tena,
na kuwakalisha katika nchi yao wenyewe.
Wageni wataungana nao
na kujiunga na nyumba ya Yakobo.
2 Mataifa watawachukua
na kuwaleta mahali pao wenyewe.
Nayo nyumba ya Israeli itamiliki mataifa
kama watumishi na wajakazi katika nchi ya
Mwenyezi Mungu.
Watawafanya watekaji wao kuwa mateka,
na kuwatawala waliowadhulumu.
3 Katika siku Mwenyezi Mungu atakapokuon-
dolea mateso, udhia na utumwa wa kikatili,
4 utaichukua dhihaka hii dhidi ya mfalme wa
Babeli:
Tazama jinsi mtesi alivyofikia mwisho!
Tazama jinsi ghadhabu yake kali ilivyokoma!
5 Mwenyezi Mungu amevunja fimbo ya mwovu,
fimbo ya utawala ya watawala,
6 ambayo kwa hasira waliyapiga mataifa
kwa mapigo yasiyo na kikomo,

nao kwa ghadhabu kali waliwatiisha mataifa
kwa jeuri pasipo huruma.
7 Nchi zote ziko kwenye mapumziko na kwenye amani,
wanabubujika kwa kuimba.
8 Hata misunobari na mierezi ya Lebanoni
inashangilia mbele yako na kusema,
“Basi kwa kuwa umeangushwa chini,
hakuna mkata miti atakayekuja kutukata.”

9 Kuzimu* kumetaharuki
kukulaki unapokuja,
kunaamsha roho za waliokufa ili kukupokea,
wote waliokuwa viongozi katika ulimwengu,
kunawafanya wainuke kwenye viti vyao vya kifalme:
wale wote waliokuwa wafalme juu ya mataifa.
10 Wote wataitikia,
watakuambia,
“Wewe pia umekuwa dhaifu, kama sisi tulivyo;
wewe umekuwa kama sisi.”
11 Majivuno yako yote yameshushwa hadi Kuzimu,
pamoja na kelele ya vinubi vyako,
mafunza yametanda chini yako,
na minyoo imekufunika.

12 Tazama jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni,
ewe nyota ya asubuhi, mwana wa mapambazuko!
Umetupwa chini duniani,

---

* **14:9** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

wewe uliyepata kuangusha mataifa!
13 Ulisema moyoni mwako,
“Nitapanda juu hadi mbinguni,
nitakiinua kiti changu cha utawala
juu ya nyota za Mungu;
nitaketi nimetawazwa juu ya mlima wa kusanyiko,
kwenye vimo vya juu sana vya Mlima Mtakatifu.
14 Nitapaa juu kupita mawingu,
nitajifanya kama Yeye Aliye Juu Sana.”
15 Lakini umeshushwa chini hadi Kuzimu,
hadi kwenye vina vya shimo.

16 Wale wanaokuona wanakukazia macho,
wanatafakari hatima yako:
“Je, huyu ndiye yule aliyetikisa dunia
na kufanya falme zitetemeke,
17 yule aliyeifanya dunia kuwa jangwa,
aliyeipindua miji yake,
na ambaye hakuwaachia mateka wake
waende nyumbani?”

18 Wafalme wote wa mataifa wamelala kwa heshima
kila mmoja katika kaburi lake.
19 Lakini wewe umetupwa nje ya kaburi lako
kama tawi lililokataliwa,
umefunikwa na waliouawa
pamoja na wale waliochomwa kwa upanga,
wale wanaoshuka hadi
kwenye mawe ya shimo.
Kama mzoga uliokanyagwa chini ya nyayo,
20 Hutajumuika nao kwenye mazishi,

kwa kuwa umeharibu nchi yako
na kuwaua watu wako.

Mzao wa mwovu
hatatajwa tena kamwe.
21 Andaa mahali pa kuwachinjia wanawe
kwa ajili ya dhambi za baba zao,
wasije wakainuka ili kuirithi nchi
na kuijaza dunia kwa miji yao.

22 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni asema,
"Nitainuka dhidi yao,
nitalikatilia mbali jina lake kutoka Babeli pamoja na watu wake walionusurika,
watoto wake na wazao wake,"
asema Mwenyezi Mungu.
23 "Nitaifanya kuwa mahali pa bundi,
na kuwa nchi ya matope;
nitaifagia kwa ufagio wa maangamizi,"
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

### *Unabii dhidi ya Ashuru*

24 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ameapa,
"Hakika, kama vile nilivyopanga, ndivyo itakavyokuwa,
nami kama nilivyokusudia, ndivyo itakavyosimama.
25 Nitamponda Mwashuru katika nchi yangu,
juu ya milima yangu nitawakanyagia chini.
Nira yake itaondolewa kutoka kwa watu wangu,

nao mzigo wake utaondolewa kutoka mabegani mwao.”

26 Huu ndio mpango uliokusudiwa kwa ajili ya ulimwengu wote,
huu ni mkono ulionyooshwa juu ya mataifa yote.
27 Kwa kuwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni amekusudia,
ni nani awezaye kumzuia?
Mkono wake umenyooshwa,
ni nani awezaye kuurudisha?

### *Unabii dhidi ya Wafilisti*

28 Neno hili lilikuja mwaka ule Mfalme Ahazi alipofariki:
29 Msifurahi, enyi Wafilisti wote,
kwamba fimbo iliyowapiga imevunjika;
kutoka mzizi wa huyo nyoka
atachipuka nyoka mwenye sumu kali,
uzao wake utakuwa joka lirukalo,
lenye sumu kali.
30 Maskini kuliko maskini wote watapata malisho,
nao wahitaji watalala salama.
Lakini mzizi wako nitauangamiza kwa njaa,
nayo njaa itawaua walionusurika.

31 Piga yowe, ee lango! Bweka, ee mji!
Yeyukeni, enyi Wafilisti wote!
Wingu la moshi linakuja toka kaskazini,
wala hakuna atakayechelewa katika safu zake.

32 Ni jibu gani litakalotolewa
kwa wajumbe wa taifa hilo?
"Mwenyezi Mungu ameifanya imara Sayuni,
na ndani yake watu wake walioonewa watapata kimbilio."

# 15

*Unabii dhidi ya Moabu*

1 Neno la unabii kuhusu Moabu:
Ari iliyo Moabu imeangamizwa:
imeharibiwa kwa usiku mmoja!
Kiri iliyo Moabu imeangamizwa,
imeharibiwa kwa usiku mmoja!
2 Diboni anakwea hadi kwenye hekalu lake,
hadi mahali pake pa juu pa kuabudia ili walie,
Moabu anaombolezea Nebo na Medeba.
Kila kichwa kimenyolewa
na kila ndevu limeondolewa.
3 Wamevaa magunia barabarani;
juu ya mapaa na kwenye viwanja
wote wanaomboleza,
wakilala kifudifudi na kulia.
4 Heshboni na Eleale wanalia,
sauti zao zinasikika hadi Yahazi.
Kwa hiyo watu wenye silaha wa Moabu wanapiga kelele,
nayo mioyo yao imezimia.

5 Moyo wangu unamlilia Moabu;
wakimbizi wake wanakimbilia Soari,
hadi Eglath-Shelishiya.
Wanapanda njia ya kwenda Luhithi,

wanaenda huku wanalia;
barabarani iendayo Horonaimu
wanaombolezea maangamizi yao.
6 Maji ya Nimrimu yamekauka
na majani yamenyauka;
mimea imekauka wala hakuna
kitu chochote kibichi kilichobaki.
7 Kwa hiyo mali waliyoipata na kujiwekea akiba
wamezichukua na kuvuka Bonde la Mierebi.
8 Mwangwi wa kilio chao umefika hadi mpakani
mwa Moabu,
kilio chao cha huzuni kimefika hadi Eglaimu,
maombolezo yao hadi Beer-Elimu.
9 Maji ya Dimoni yamejaa damu,
lakini bado nitaleta pigo jingine juu ya Dimoni:
simba juu ya wakimbizi wa Moabu
na juu ya wale wanaobaki katika nchi.

# 16

*Hali ya kukata tamaa ya Moabu*

1 Pelekeni wana-kondoo kama ushuru
kwa mtawala wa nchi,
Kutoka Sela, kupitia jangwani,
hadi mlima wa Binti Sayuni.
2 Kama ndege wanaopapatika
waliofukuzwa kutoka kiota,
ndivyo walivyo wanawake wa Moabu
kwenye vivuko vya Mto Arnoni.

3 “Tupeni shauri,
toeni uamuzi.
Wakati wa adhuhuri,
fanyeni kivuli chenu kama usiku.

Wafichení watoro,
msisaliti wakimbizi.
4 Waacheni watoro wa Moabu wakae pamoja nanyi;
kuweni mahali pao pa salama ili kuepuka mwangamizi."

Mtesi atafikia mwisho na maangamizi yatakoma,
aletaye vita atatoweka kutoka nchi.
5 Kwa upendo kiti cha utawala kitaimarishwa,
kwa uaminifu mtu ataketi juu yake,
yeye atokaye nyumba ya Daudi:
yeye ambaye katika kuhukumu hutafuta haki,
na huhimiza njia ya haki.

6 Tumesikia juu ya kiburi cha Moabu:
kiburi chake cha kujivuna na udanganyifu,
kiburi chake na ufidhuli wake,
lakini majivuno yake si kitu.
7 Kwa hiyo Wamoabu wanaomboleza,
wanaiombolezea Moabu kwa pamoja.
Wanaomboleza na kuhuzunika
kwa ajili ya watu wa Kir-Haresethi.
8 Mashamba ya Heshboni yananyauka,
pia na mizabibu ya Sibma.
Watawala wa mataifa
wamekanyaga mizabibu iliyo mizuri sana,
ambayo ilipata kufika Yazeri
na kuenea kuelekea jangwani.
Machipukizi yake yalienea
yakafika hadi baharini.
9 Hivyo ninalia kama Yazeri aliavyo,
kwa ajili ya mizabibu ya Sibma.

Ee Heshboni, ee Eleale,
ninakulowesha kwa machozi!
Shangwe za furaha kwa ajili ya tunda lako lililoiva
na kwa ajili ya mavuno zimekomeshwa.
10 Furaha na shangwe zimeondolewa
kutoka mashamba ya matunda;
hakuna yeyote aimbaye wala apazaye sauti
katika mashamba ya mizabibu;
hakuna yeyote akanyagaye zabibu shinikizoni,
kwa kuwa nimekomesha makelele.
11 Moyo wangu unaomboleza kwa ajili ya Moabu kama kinubi,
nafsi yangu yote kwa ajili ya Kir-Haresethi.
12 Moabu anapojitokeza mahali pake pa juu pa kuabudia,
anajichosha mwenyewe tu;
anapoenda mahali pake pa ibada za sanamu ili kuomba,
haitamfaidi lolote.
13 Hili ndilo neno ambalo Mwenyezi Mungu
ameshasema kuhusu Moabu.
14 Lakini sasa Mwenyezi Mungu anasema:
"Katika miaka mitatu, kama vile mtumishi aliye-
fungwa na mkataba angeihesabu, fahari ya Moabu na watu wake wengi watadharauliwa, nao walionusurika watakuwa wachache sana, tena wanyonge."

# 17

*Neno dhidi ya Dameski*

1 Neno la unabii kuhusu Dameski:
"Tazama, Dameski haitakuwa tena mji
bali itakuwa lundo la magofu.

2 Miji ya Aroeri itaachwa
na itaachiwa mifugo ambayo italala huko,
bila yeyote wa kuyaogopesha.
3 Mji wenye ngome utatoweka kutoka Efraimu,
nao uweza wa ufalme kutoka Dameski;
mabaki ya Aramu yatakuwa
kama utukufu wa Waisraeli,"
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

4 "Katika siku ile utukufu wa Yakobo utafifia,
unono wa mwili wake utadhoofika.
5 Itakuwa kama mvunaji akusanyavyo nafaka
na kuvuna nafaka kwa mikono yake,
kama wakati mtu aokotapo masazo ya masuke
katika Bonde la Warefai.
6 Hata hivyo baadhi ya masazo yatabaki,
kama vile mti wa mzeituni unavyopigwa,
kukiachwa zeituni mbili au tatu juu ya matawi kileleni,
nne au tano katika matawi yanayozaa sana,"
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli.

7 Katika siku ile watu watamwangalia Muumba wao,
na kuelekeza macho yao kwa yule Aliye Mtakatifu wa Israeli.
8 Hawataziangalia tena madhabahu,
kazi za mikono yao,
nao hawataheshimu nguzo za Ashera,
na madhabahu za kufukizia uvumba zilizofanywa kwa mikono yao.

9 Katika siku ile miji yao iliyo imara, ambayo
waliihama kwa sababu ya Waisraeli, itakuwa

kama mahali palipoachwa pa vichaka na magugu. Nayo yote itakuwa ukiwa.
10 Mmemsahau Mungu Mwokozi wenu,
hamkumkumbuka Mwamba aliye ngome yenu.
Kwa hiyo, hata ingawa mlipandikiza mimea iliyo mizuri sana
na kuotesha mizabibu ya kigeni,
11 hata kama siku ile unapoipandikiza, unaifanya iote
na asubuhi ile ile unayoipanda, unaifanya ichipue,
hata hivyo mavuno yatakuwa kama si kitu
katika siku ile ya ugonjwa na maumivu yasiyoponyeka.

12 Ole! Ghadhabu ya mataifa mengi:
wanaghadhibika kama bahari iliyochafuka!
Ole! Makelele ya mataifa wanaovuma:
wanavuma kama ngurumo za maji mengi!
13 Ingawa mataifa yanavuma kama ngurumo za maji yanayofanya mawimbi,
wakati anayakemea yanakimbia mbali,
yanafukuzwa mbele ya upepo kama makapi juu ya milima,
kama jani likivingirishwa na dhoruba.
14 Wakati wa jioni, hofu ya ghafula!
Kabla ya asubuhi, wametoweka!
Hili ndilo fungu la wale wanaotupora,
fungu la wale wanaotunyang'anya mali yetu.

# 18

*Unabii dhidi ya Kushi*

1 Ole kwa nchi ya mvumo wa mabawa*,
kando ya mito ya Kushi,
2 iwapelekayo wajumbe wake kupitia bahari
kwa mashua za mafunjo juu ya maji.

Nendeni, wajumbe wepesi,
kwa taifa la watu warefu wenye ngozi nyororo,
kwa taifa linaloogopwa mbali na karibu,
taifa gomvi lenye lugha ngeni,
ambalo nchi yao imegawanywa kwa mito.

3 Enyi mataifa yote ya ulimwengu,
ninyi mnaoishi duniani
wakati bendera itakapoinuliwa milimani,
mtaiona,
nayo tarumbeta itakapolia,
mtaisikia.
4 Hili ndilo Mwenyezi Mungu aliloniambia:
“Nitatulia kimya na kutazama
kutoka maskani yangu,
kama joto linalometameta katika mwanga wa jua,
kama wingu la umande
katika joto la wakati wa mavuno.”
5 Kwa maana, kabla ya mavuno,
wakati wa kuchanua ukishapita
na maua yakawa zabibu zinazoiva,
atayakata machipukizi kwa mundu wa kupogolea matawi,
naye atakata na kuyaondoa matawi yaliyopanuka.

* **18:1** au *wa nzige*

6 Yote yataachwa kwa ajili ya ndege wawindao wa mlimani
na wanyama pori,
ndege watajilisha juu yake wakati wote wa kiangazi,
nao wanyama pori wakati wote wa masika.
7 Wakati huo matoleo yataletwa kwa Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
kutoka kwa taifa la watu warefu wenye ngozi nyororo,
kutoka kwa taifa linaloogopwa mbali na karibu,
kutoka taifa gomvi lenye lugha ngeni,
ambalo nchi yao imegawanywa kwa mito,
matoleo yataletwa katika Mlima Sayuni, mahali
pa Jina la Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni.

# 19

### *Unabii kuhusu Misri*

1 Neno la unabii kuhusu Misri:
Tazama, Mwenyezi Mungu amepanda juu ya wingu liendalo kwa haraka
naye anakuja Misri.
Sanamu za Misri zinatetemeka mbele yake,
nayo mioyo ya Wamisri inayeyuka ndani yao.

2 “Nitamchochea Mmisri dhidi ya Mmisri,
ndugu atapigana dhidi ya ndugu,
jirani dhidi ya jirani,
mji dhidi ya mji,
ufalme dhidi ya ufalme.

3 Wamisri watakufa moyo,
na nitaibatilisha mipango yao.
Watatafuta ushauri kwa sanamu na kwa roho za waliokufa,
kwa waaguzi na kwa wale waongeao na mizimu.
4 Nitawatia Wamisri
mikononi mwa bwana mkatili
na mfalme mkali atawatawala,"
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

5 Maji ya mito yatakauka,
chini ya mto kutakauka kwa jua.
6 Mifereji itanuka;
vijito vya Misri vitapungua
na kukauka.
Matete na nyasi vitanyauka,
7 pia mimea iliyo kando ya Mto Naili,
pale mto unapomwaga maji baharini.
Kila shamba lililopandwa kando ya Mto Naili litakauka,
litapeperushwa na kutoweka kabisa.
8 Wavuvi watalia na kuomboleza,
wote watupao ndoana katika Mto Naili,
na watupao nyavu katika maji
watadhoofika kwa majonzi.
9 Wale watu wafanyao kazi ya kitani kilichochambuliwa watakata tamaa,
wafumaji wa kitani safi watavunjika moyo.
10 Wafanyao kazi ya kufuma nguo watahuzunishwa,
nao vibarua wataugua moyoni.

11 Maafisa wa Soani ni wapumbavu kabisa,
washauri wa Farao wenye busara wanatoa ushauri wa kijinga.
Unawezaje kumwambia Farao,
“Mimi ni mmoja wa watu wenye hekima,
mwanafunzi wa wafalme wa zamani”?

12 Wako wapi sasa watu wako wenye hekima?
Wao wakuoneshe na kukufahamisha
ni nini Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
amepanga dhidi ya Misri.
13 Maafisa wa Soani wamekuwa wapumbavu,
viongozi wa Memfisi* wamedanganyika,
walio mawe ya pembe ya taifa lake
wameipotosha Misri.
14 Mwenyezi Mungu amewamwagia
roho ya kizunguzungu;
wanaifanya Misri iyumbayumbe
katika yale yote inayoyafanya,
kama vile mlevi ayumbayumbavyo
katika kutapika kwake.
15 Misri haiwezi kufanya kitu chochote,
cha kichwa wala cha mkia,
cha tawi la mtende wala cha tete.
16 Katika siku ile Wamisri watakuwa kama
wanawake. Watatetemeka kwa hofu mbele ya
mkono wa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni anaoinua dhidi yao.
17 Nayo nchi ya Yuda itawatia hofu Wamisri,
kila mmoja atakayetajiwa Yuda ataingiwa na
hofu, kwa sababu ya kile ambacho Mwenyezi

* **19:13** au *Nofu*

Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni anapanga dhidi yao.

18 Katika siku hiyo miji mitano ya Misri,
itazungumza lugha ya Kanaani, na kuapa kumtii
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni. Mji mmoja utaitwa Mji wa Uharibifu†.

19 Katika siku hiyo patakuwa na madhabahu
ya Mwenyezi Mungu katikati ya Misri na mnara
wa kumbukumbu kwa Mwenyezi Mungu kwenye
mpaka wa Misri.
20 Itakuwa alama na ushahidi kwa ajili ya
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni katika nchi ya Misri. Watakapomlilia
Mwenyezi Mungu kwa sababu ya watesi wao,
Mungu atawapelekea mwokozi na mtetezi, naye
atawaokoa.
21 Hivyo Mwenyezi Mungu atajijulisha
mwenyewe kwa Wamisri, nao katika siku hiyo
watamkubali Mwenyezi Mungu. Wataabudu
kwa kumtolea dhabihu na sadaka za nafaka,
watamwekea Mwenyezi Mungu nadhiri na
kuzitimiza.
22 Mwenyezi Mungu ataipiga Misri kwa
tauni; atawapiga na kuwaponya. Watamgeukia
Mwenyezi Mungu, naye atayasikia maombi yao
na kuwaponya.

23 Katika siku hiyo kutakuwa na njia kuu kutoka Misri hadi Ashuru. Waashuru wataenda
Misri, na Wamisri wataenda Ashuru. Wamisri na
Waashuru wataabudu pamoja.

† **19:18** yaani *Heliopoli* (*Mji wa Jua*)

24 Katika siku hiyo Israeli itakuwa ya tatu,
pamoja na Misri na Ashuru, nao watakuwa
baraka kwa dunia.
25 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni atawabariki, akisema, “Baraka iwe
kwa Misri watu wangu, kwa Ashuru kazi ya
mikono yangu, na kwa Israeli urithi wangu.”

# 20

### *Unabii dhidi ya Misri na Kushi*

1 Mwaka ule jemadari mkuu alitumwa na
Mfalme Sargoni wa Ashuru, naye akaja Ashdodi,
akaushambulia na kuuteka,
2 wakati huo Mwenyezi Mungu alisema
kwa kinywa cha Isaya mwana wa Amozi.
Akamwambia, “Vua gunia kutoka mwilini
mwako na viatu kutoka miguuni mwako.” Naye
akafanya hivyo, akitembea uchi, bila viatu.
3 Kisha Mwenyezi Mungu akasema, “Kama
mtumishi wangu Isaya alivyotembea uchi na bila
viatu kwa miaka mitatu, kama ishara na dalili
mbaya dhidi ya nchi ya Misri na Kushi,
4 vivyo hivyo mfalme wa Ashuru atawaongoza
mateka wa Wamisri, na watu wa uhamisho wa
Kushi, uchi na bila viatu, vijana hata wazee,
wakiwa matako wazi, kwa aibu ya Wamisri.
5 Wale waliotegemea Kushi na kujivunia Misri
wataogopa na kuaibika.
6 Katika siku ile watu wanaoishi katika pwani
hii watasema, ‘Tazama lililowapata wale tuliowa-
tegemea, wale tuliowakimbilia kwa msaada na
wokovu kutoka mikononi mwa mfalme wa
Ashuru! Tutawezaje basi kupona?’ ”

# 21

*Unabii dhidi ya Babeli*

1 Neno la unabii kuhusu Jangwa kando ya Bahari:
Kama upepo wa kisulisuli unaopita katika nchi hadi kusini,
mshambuliaji anakuja kutoka jangwani,
kutoka nchi inayotisha.

2 Nimeoneshwa maono ya kutisha:
Msaliti anasaliti, mteka nyara anateka nyara.
Elamu, shambulia! Umedi, zingira kwa jeshi!
Nitakomesha huzuni zote alizosababisha.

3 Kwa sababu hii, mwili wangu umeteswa na maumivu,
maumivu makali ya ghafula yamenishika,
kama yale ya mwanamke mwenye uchungu wa kuzaa.
Nimeduwazwa na lile ninalolisikia,
nimeshangazwa na lile ninaloliona.
4 Moyo wangu unababaika,
woga unanifanya nitetemeke,
gizagiza la jioni nililolitamani sana,
limekuwa hofu kuu kwangu.

5 Wanaandaa meza,
wanatandaza mazulia,
wanakula, wanakunywa!
Amkeni, enyi maafisa,
zitieni ngao mafuta!
6 Hili ndilo Bwana analoniambia:
"Nenda, weka mlinzi,
na atoe taarifa ya kile anachokiona.

7 Anapoona magari ya vita
pamoja na kundi la farasi,
wapanda punda au wapanda ngamia,
na awe macho, awe macho kikamilifu."
8 Naye mlinzi alipaza sauti,
"Mchana baada ya mchana, bwana wangu,
ninasimama katika mnara wa ulinzi,
kila usiku ninakaa mahali pangu nilipoam-
riwa.
9 Tazama, yuaja mtu anayepanda gari la vita
pamoja na kundi la farasi.
Naye anajibu:
'Babeli umeanguka, umeanguka!
Vinyago vyote vya miungu yake
vimelala chini vikiwa vimevunjwa!' "

10 Ee watu wangu, mliopondwa kwenye sakafu ya
kupuria,
ninawaambia kile nilichokisikia
kutoka kwa Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni,
kutoka kwa Mungu wa Israeli.

### *Unabii dhidi ya Edomu*

11 Neno la unabii kuhusu Duma:
Mtu fulani ananiita kutoka Seiri,
"Mlinzi, usiku utaisha lini?
Mlinzi, usiku utaisha lini?"
12 Mlinzi anajibu,
"Asubuhi inakuja, lakini pia usiku.
Ukitaka kuuliza, basi uliza;
na urudi mara tena."

### *Unabii dhidi ya Arabia*

13 Neno la unabii kuhusu Arabia:

Enyi misafara ya Wadedani,
mnaopiga kambi katika vichaka vya Arabia,
14 leteni maji kwa wenye kiu,
ninyi mnaoishi Tema,
leteni chakula kwa ajili ya wakimbizi.
15 Wanaukimbia upanga,
upanga uliochomolewa alani,
kutoka upinde uliopindwa,
na kutoka kwa joto la vita.

16 Hili ndilo Bwana analoniambia: "Katika
muda wa mwaka mmoja, kama vile mtumishi
aliyefungwa na mkataba angeihesabu, majivuno
yote ya Kedari yatafikia mwisho.
17 Wanaume wavutao pinde walionusurika,
mashujaa wa Kedari, watakuwa wachache."
Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli, amesema.

# 22

*Unabii kuhusu Yerusalemu*

1 Neno la unabii kuhusu Bonde la Maono:
Nini kinachokutaabisha sasa,
kwamba ninyi nyote mmepanda juu ya mapaa?
2 Ewe mji uliojaa ghasia,
ewe mji wa makelele na sherehe!
Watu wenu waliokufa hawakuuawa kwa upanga,
wala hawakufa vitani.
3 Viongozi wako wote wamekimbia pamoja,
wamekamatwa bila kutumia upinde.
Ninyi nyote mliokamatwa mlichukuliwa wafungwa pamoja,
mlikimbia wakati adui alipokuwa bado mbali.

4 Kwa hiyo nilisema, “Geukia mbali nami,
niache nilie kwa uchungu.
Usijaribu kunifariji
juu ya maangamizi ya watu wangu.”

5 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, anayo siku
ya ghasia, ya kukanyaga, na ya kuogofya
katika Bonde la Maono,
siku ya kuangusha kuta
na ya kupiga kelele hadi milimani.
6 Elamu analichukua podo,
pamoja na waendesha magari ya vita na farasi.
Kiri anaifungua ngao.
7 Mabonde yako yaliyo mazuri sana yamejaa magari ya vita,
nao wapanda farasi wamewekwa kwenye malango ya mji.

8 Ulinzi wa Yuda umeondolewa.
Nawe ulitazama siku ile
silaha katika Jumba la Kifalme la Mwituni.
9 Mkaona kuwa Mji wa Daudi
una matundu mengi katika ulinzi wake,
mkaweka akiba ya maji
kwenye Bwawa la Chini.
10 Mlihesabu majengo katika Yerusalemu
nanyi mkabomoa nyumba ili kuimarisha ukuta.
11 Mlijenga bwawa la maji katikati ya kuta mbili
kwa ajili ya maji ya Bwawa la Zamani,
lakini hamkumtazama Yule aliyelitengeneza,

au kuwa na heshima kwa Yule aliyeubuni tangu zamani za kale.

12 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
aliwaita siku ile
ili kulia na kuomboleza,
kung'oa nywele zenu na kuvaa magunia.
13 Lakini tazama, kuna furaha na sherehe,
kuchinja ng'ombe na kuchinja kondoo,
kula nyama na kunywa mvinyo!
Mnasema, "Tuleni na kunywa,
kwa kuwa kesho tutakufa!"
14 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni amelifunua hili nikiwa ninasikia:
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, asema: "Hadi siku ya kufa kwenu, dhambi hii haitafanyiwa upatanisho."
15 Hili ndilo Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni, asemalo:
"Nenda ukamwambie huyu wakili Shebna,
ambaye ni msimamizi wa jumba la kifalme:
16 Unafanya nini hapa, na ni nani aliyekupa ruhusa
kujikatia kaburi lako mwenyewe,
ukichonga kaburi lako mahali palipo juu,
na kutoboa kwa patasi mahali pako pa kupumzikia katika mwamba?

17 "Jihadhari, Mwenyezi Mungu yu karibu kukukamata thabiti,
na kukutupa mbali, ewe mtu mwenye nguvu.
18 Atakuvingirisha uwe kama mpira

na kukutupa katika nchi kubwa.

Huko ndiko utakakofia,
na huko ndiko magari yako ya vita ya fahari yatabakia,
na kuwa fedheha kwa nyumba ya bwana wako!

19 Nitakuondoa kutoka kazi yako,
nawe utaondoshwa kutoka nafasi yako.

20 “Katika siku ile, nitamwita mtumishi wangu,
Eliakimu mwana wa Hilkia.
21 Nitamvika joho lako, nami nitamfunga
mshipi wako kiunoni mwake, na kumkabidhi
mamlaka yako. Yeye atakuwa baba kwa wale
wanaoishi Yerusalemu na kwa nyumba ya Yuda.
22 Nitaweka begani mwake ufunguo wa
nyumba ya Daudi. Kile afunguacho hakuna
awezaye kufunga, na kile afungacho hakuna
awezaye kufungua.
23 Nitampigilia kama kigingi kilicho mahali
palipo imara, naye atakuwa kiti cha heshima kwa
ajili ya nyumba ya baba yake.
24 Utukufu wote wa jamaa yake utakuwa juu
yake: Wazao wa jamaa hiyo na machipukizi yake,
vyombo vyake vyote vidogo, tangu bakuli hadi
magudulia yote.”

25 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni asema, “Katika siku ile, kigingi kili-
chopigiliwa mahali imara kitaachia njia. Ki-
takatwa, nacho kitaanguka na mzigo ulion-
ing’inia juu yake utaanguka chini.” Mwenyezi
Mungu amesema.

# 23

*Unabii kuhusu Tiro*

1 Neno la unabii kuhusu Tiro:
Ombolezeni, enyi meli za Tarshishi!
Kwa kuwa Tiro imeangamizwa,
imeachwa bila nyumba wala bandari.
Kuanzia nchi ya Kitimu*
neno limewajia.

2 Nyamazeni kimya, enyi watu wa kisiwani,
pia ninyi wafanyabiashara wa Sidoni,
ambao mabaharia wamewatajirisha.
3 Kwenye maji makuu
nafaka za Shihori zilikuja;
mavuno ya Mto Naili yalikuwa mapato ya Tiro,
naye akawa soko la mataifa.

4 Uaibishwe ee Sidoni, nawe ee ngome la bahari,
kwa kuwa bahari imesema:
“Sijapata kuwa na uchungu wa kuzaa wala sijapata kuzaa,
wala sijapata kulea wana wala kutunza binti.”
5 Habari ifikapo Misri,
watakuwa katika maumivu makuu kwa ajili ya taarifa kutoka Tiro.

6 Vukeni hadi Tarshishi,
ombolezeni, enyi watu wa kisiwani.
7 Je, huu ndio mji wenu uliojaa sherehe,
mji wa zamani, zamani kabisa

* **23:1** yaani *Kipro*, kisiwa katika Bahari ya Mediterania

ambao miguu yake imeuchukua
kufanya makao nchi za mbali sana?
8 Ni nani amepanga hili dhidi ya Tiro,
mji utoao mataji,
ambao wafanyabiashara wake ni wana wa mfalme
na wachuuzi wake ni watu mashuhuri wa dunia?
9 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ndiye alipanga jambo hili,
ili kukishusha kiburi cha utukufu wote
na kuwanyenyekeza wale wote
ambao ni mashuhuri duniani.

10 Ee Binti Tarshishi,
pita katika nchi yako kama vile Mto Naili
kwa kuwa huna tena bandari.
11 Mwenyezi Mungu amenyoosha mkono wake juu ya bahari
na kuzifanya falme zake zitetemeke.
Ametoa amri kuhusu Kanaani
kwamba ngome zake ziangamizwe.
12 Alisema, "Usizidi kufurahi,
ee Bikira Binti Sidoni, sasa umepondwa!

"Simama, vuka uende Kitimu;
hata huko hutapata pumziko."
13 Tazama katika nchi ya Wakaldayo,
watu hawa ambao sasa hawaonekani kama wapo!
Waashuru wameifanya nchi hiyo
kuwa mahali pa viumbe wa jangwani.
Wamesimamisha minara yao ya kuuzingira,
wameziteka ngome zake na kuziacha tupu

na kuufanya kuwa magofu.

14 Ombolezeni, enyi meli za Tarshishi;
ngome yenu imeangamizwa!
15 Wakati huo Tiro utasahauliwa kwa miaka
sabini, muda wa maisha ya mfalme. Lakini
mwisho wa miaka hiyo sabini, itakuwa kwa Tiro
kama ilivyo katika wimbo wa kahaba:
16 “Twaa kinubi, tembea mjini kote,
ewe kahaba uliyesahauliwa;
piga kinubi vizuri, imba nyimbo nyingi,
ili upate kukumbukwa.”
17 Mwishoni mwa miaka sabini, Mwenyezi
Mungu atatembelea Tiro. Naye Tiro atarudia
ajira yake ya ukahaba, na atafanya biashara yake
na falme zote duniani.
18 Lakini faida na mapato yake yatawekwa
wakfu kwa Mwenyezi Mungu; hayatahifadhiwa
wala kufichwa. Faida zake zitaenda kwa wale
wanaoishi mbele za Mwenyezi Mungu kwa ajili
ya chakula tele na mavazi mazuri.

# 24

*Dunia kuharibiwa*

1 Tazama, Mwenyezi Mungu ataifanya dunia
kuwa ukiwa
na kuiharibu,
naye atauharibu uso wake
na kutawanya wanaoishi ndani yake:
2 ndivyo itakavyokuwa
kwa makuhani na kwa watu,
kwa bwana na kwa mtumishi,
kwa bibi na kwa mjakazi wake,

kwa muuzaji na kwa mnunuzi,
kwa mkopaji na kwa mkopeshaji,
kwa mdaiwa na kwa mdai.
3 Dunia itaharibiwa kabisa
na kutekwa nyara kabisa.
Mwenyezi Mungu amesema neno hili.

4 Dunia inakauka na kunyauka,
dunia inanyong'onyea na kunyauka,
waliotukuzwa wa dunia wananyong'onyea.
5 Dunia imetiwa unajisi na watu wake;
wameacha kutii sheria,
wamevunja amri
na kuvunja agano la milele.
6 Kwa hiyo laana inaiteketeza dunia,
watu wake lazima waichukue hatia yao.
Kwa hiyo wakazi wa dunia wameteketezwa,
nao waliosalia ni wachache sana.
7 Divai mpya inakauka na mzabibu unanyauka,
watu wote wafurahishao wanalia kwa huzuni.
8 Furaha ya matoazi imekoma,
kelele za wenye furaha zimekoma,
shangwe za kinubi zimenyamaza.
9 Hawanywi tena mvinyo pamoja na wimbo,
kileo ni kichungu kwa wanywaji wake.
10 Mji ulioharibiwa umekuwa ukiwa,
mlango wa kila nyumba umefungwa.
11 Barabarani wanalilia kupata mvinyo,
furaha yote imegeuka kuwa majonzi,
furaha yote imefukuziwa mbali na dunia.
12 Mji umeachwa katika uharibifu,
lango lake limevunjwa vipande.

13 Ndivyo itakavyokuwa duniani
na miongoni mwa mataifa,
kama vile wakati mzeituni upigwavyo,
au kama vile wakati masazo yabakiavyo baada ya zabibu kuvunwa.

14 Wanapaza sauti zao, wanapiga kelele kwa furaha,
kutoka magharibi wanasifu kwa ukelele utukufu wa Mwenyezi Mungu.
15 Kwa hiyo upande wa mashariki mpeni Mwenyezi Mungu utukufu,
liadhimisheni jina la Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli,
katika visiwa vya bahari.
16 Kutoka miisho ya dunia tunasikia uimbaji:
"Utukufu kwa Yule Mwenye Haki."

Lakini nilisema, "Ninadhoofika, ninadhoofika!
Ole wangu!
Watenda hila wanasaliti!
Kwa hila watenda hila wanasaliti!"
17 Hofu, shimo na mtego vinakungojea,
ewe mtu ukaaye duniani.
18 Kila akimbiaye asikiapo sauti ya hofu
atatumbukia shimoni,
naye yeyote apandaye kutoka shimoni,
atanaswa kwenye mtego.

Malango ya gharika ya mbinguni yamefunguliwa,
misingi ya dunia inatikisika.
19 Dunia imepasuka,

dunia imechanika,
dunia imetikiswa kabisa.
20 Dunia inapepesuka kama mlevi,
inayumbayumba kama kibanda kwenye upepo;
imelemewa sana na mzigo wa hatia ya uasi wake
na ikianguka kamwe haitainuka tena.

21 Katika siku ile Mwenyezi Mungu ataadhibu
mamlaka zilizo juu mbinguni,
na wafalme walio chini duniani.
22 Watakusanywa pamoja
kama wafungwa waliofungwa gerezani;
watafungiwa gerezani
na kuadhibiwa baada ya siku nyingi.
23 Mwezi utatiwa haya, nalo jua litaaibishwa;
kwa maana Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni atatawala
juu ya Mlima Sayuni na katika Yerusalemu,
tena mbele ya wazee wake, kwa utukufu.

# 25

### *Sifa kwa Mwenyezi Mungu*

1 Ee Mwenyezi Mungu, wewe ni Mungu wangu,
nitakutukuza na kulisifu jina lako,
kwa maana katika ukamilifu wa uaminifu
umetenda mambo ya ajabu,
mambo yaliyokusudiwa tangu zamani.
2 Umeufanya mji kuwa lundo la kifusi,
mji wenye ngome kuwa magofu,
ngome imara ya wageni kuwa si mji tena,
wala hautajengwa tena kamwe.
3 Kwa hiyo mataifa yenye nguvu yatakuheshimu,

miji ya mataifa katili itakuogopa wewe.
4 Umekuwa kimbilio la watu maskini,
kimbilio la mhitaji katika taabu yake,
hifadhi wakati wa dhoruba
na kivuli wakati wa hari.
Kwa maana pumzi ya wakatili
ni kama dhoruba ipigayo ukuta
5 na kama joto la jangwani.
Wewe wanyamazisha kelele ya wageni;
kama vile hari ipunguzwavyo na kivuli cha wingu,
ndivyo wimbo wa wakatili unyamazishwavyo.

6 Juu ya mlima huu Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ataandaa
karamu ya vinono kwa mataifa yote,
karamu ya mvinyo wa zamani,
nyama nzuri sana na divai zilizo bora sana.
7 Juu ya mlima huu ataharibu
sitara ihifadhiyo mataifa yote,
kile kifuniko kifunikacho mataifa yote,
8 yeye atameza mauti milele.
Bwana Mungu Mwenyezi atafuta machozi katika nyuso zote;
ataondoa aibu ya watu wake duniani kote.
Mwenyezi Mungu amesema hili.
9 Katika siku ile watasema,
"Hakika huyu ndiye Mungu wetu;
tulimtumaini, naye akatuokoa.
Huyu ndiye Mwenyezi Mungu, tuliyemtumaini;
sisi tushangilie na kufurahia katika wokovu wake."

10 Mkono wa Mwenyezi Mungu utatulia juu ya mlima huu,
bali Moabu atakanyagwa chini
kama majani makavu yakanyagwavyo kwenye shimo la mbolea.
11 Watakunjua mikono yao katikati yake,
kama vile mwogeleaji akunjuavyo mikono yake ili aogelee.
Mungu atashusha kiburi chao
licha ya ujanja wa mikono yao.
12 Atabomoa kuta ndefu za ngome yako
na kuziangusha chini,
atazishusha chini ardhini,
hadi mavumbini kabisa.

# 26

*Wimbo wa ushindi*

1 Katika siku ile, wimbo huu utaimbwa katika nchi ya Yuda:
Tuna mji ulio na nguvu,
Mungu huufanya wokovu
kuwa kuta zake na maboma yake.
2 Fungua malango ili taifa lenye haki lipate kuingia,
taifa lidumishalo imani.
3 Utamlinda katika amani kamilifu
yeye ambaye moyo wake ni thabiti
kwa sababu anakutumaini wewe.
4 Mtumaini Mwenyezi Mungu milele,
kwa kuwa Mwenyezi Mungu,
Mwenyezi Mungu,
ni Mwamba wa milele.
5 Huwashusha wale wajikwezao,
huushusha chini mji wenye kiburi,

huushusha hadi ardhini
na kuutupa chini mavumbini.
6 Miguu huukanyagia chini:
miguu ya hao waliodhulumiwa,
hatua za hao maskini.

7 Mapito ya wenye haki ni nyoofu.
Ewe uliye Mwenye Haki,
waisawazisha njia ya mtu mnyofu.
8 Naam, Mwenyezi Mungu, tukienenda katika sheria zako,
twakungojea wewe,
jina lako na sifa zako
ndizo shauku za mioyo yetu.
9 Nafsi yangu yakutamani wakati wa usiku,
wakati wa asubuhi roho yangu yakuonea shauku.
Hukumu zako zinapokuja juu ya dunia,
watu wa ulimwengu hujifunza haki.
10 Ingawa neema yaoneshwa kwa waovu,
hawajifunzi haki;
hata katika nchi ya unyofu huendelea kutenda mabaya
wala hawazingatii utukufu wa Mwenyezi Mungu.
11 Ee Mwenyezi Mungu, mkono wako umeinuliwa juu,
lakini hawauoni.
Wao na waone wivu wako kwa ajili ya watu wako tena waaibishwe,
moto uliowekwa akiba kwa ajili ya adui zako na uwateketeze.

12 Mwenyezi Mungu, unaamuru amani kwa ajili yetu,
yale yote tuliyoweza kuyakamilisha ni wewe uliyetenda kwa ajili yetu.
13 Ee Mwenyezi Mungu, Mungu wetu, mabwana wengine zaidi ya wewe wametutawala,
lakini jina lako pekee ndilo tunaloliheshimu.
14 Wao sasa wamekufa, wala hawako tena hai,
roho za waliokufa hazitarudi tena.
Uliwaadhibu na kuwaangamiza,
umefuta kumbukumbu lao lote.
15 Umeliongeza hilo taifa, Ee Mwenyezi Mungu,
umeliongeza hilo taifa.
Umejipatia utukufu kwa ajili yako mwenyewe,
umepanua mipaka yote ya nchi.

16 Mwenyezi Mungu, walikujia katika taabu yao,
wewe ulipowarudi,
waliweza kuomba kwa kunong'ona tu.
17 Kama mwanamke mwenye mimba aliyekaribia kuzaa
anavyogaagaa na kulia kwa ajili ya maumivu yake,
ndivyo tulivyokuwa mbele zako, Ee Mwenyezi Mungu.
18 Tulikuwa na mimba, tuligaagaa kwa maumivu,
lakini tulizaa upepo.
Hatukuleta wokovu duniani,
hatujazaa watu katika ulimwengu huu.

19 Lakini wafu wenu wataishi,
nayo miili yao itafufuka.
Ninyi mnaokaa katika mavumbi,

amkeni mkashangilie kwa furaha.
Umande wenu ni kama umande wa asubuhi,
dunia itawazaa wafu wake.

20 Nendeni, watu wangu, ingieni vyumbani mwenu
na mfunge milango nyuma yenu,
jificheni kwa kitambo kidogo
hadi ghadhabu yake ipite.
21 Tazama, Mwenyezi Mungu anakuja kutoka makao yake
ili kuwaadhibu watu wa dunia kwa ajili ya dhambi zao.
Dunia itadhihirisha umwagaji damu juu yake,
wala haitaendelea kuwaficha watu wake waliouawa.

# 27

## *Wokovu kwa ajili ya Israeli*

1 Katika siku ile,
Mwenyezi Mungu ataadhibu kwa upanga wake,
upanga wake mkali, mkubwa na wenye nguvu;
ataadhibu Lewiathani* yule nyoka apitaye kwa mwendo laini,
Lewiathani yule nyoka mwenye kujipinda;
atamuua yule mnyama mkubwa wa baharini.
2 Katika siku ile:
"Imbeni kuhusu shamba la mizabibu lililozaa:
3 Mimi, Mwenyezi Mungu, ninalitunza,
ninalinywesha maji mfululizo.

---

* **27:1** Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.

Ninalichunga usiku na mchana
ili mtu yeyote asije akalidhuru.
4 Mimi sijakasirika.
Laiti michongoma na miiba ingenikabili!
Ningepambana dhidi yake katika vita,
ningeichoma moto yote.
5 Au niwaache waje kwangu kwa ajili ya kupata kimbilio,
wao na wafanye amani nami,
naam, wafanye amani nami.”

6 Katika siku zijazo, Yakobo atatia mizizi,
Israeli atatoa chipukizi na kuchanua maua,
naye atajaza ulimwengu wote kwa matunda.

7 Je, Mwenyezi Mungu amempiga
vile alivyowapiga wale waliompiga?
Je, yeye ameuawa
vile walivyouawa wale waliomuua yeye?
8 Kwa vita na kwa kumfukuza unapingana naye:
kwa mshindo wake mkali anamfukuza,
kama siku ile uvumapo upepo wa mashariki.
9 Kwa hili, basi, hatia ya Yakobo itafanyiwa upatanisho,
nalo hili litakuwa matunda ya utimilizo wa kuondolewa kwa dhambi yake:
Wakati atayafanya mawe yote ya madhabahu
kuwa kama mawe ya chokaa yaliyopondwa vipande vipande,
hakuna nguzo za Ashera au madhabahu za kufukizia uvumba
zitakazobaki zimesimama.
10 Mji wenye ngome umebaki ukiwa,

makazi yaliyotelekezwa, yaliyoachwa kama jangwa.
Huko ndama hulisha,
huko hujilaza,
wanakwanyua matawi yake.
11 Wakati vijiti vyake vimekauka, huvunjwa
nao wanawake huja na kuwasha navyo moto.
Kwa kuwa hili ni taifa lisilo na ufahamu,
kwa hiyo yeye aliyewafanya hana huruma juu yao,
Muumba wao hawaoneshi fadhili.
12 Katika siku ile Mwenyezi Mungu atapura
kutoka matiririko ya Mto Frati hadi Kijito cha
Misri, nanyi ee Waisraeli, mtakusanywa mmoja
mmoja.
13 Katika siku ile tarumbeta kubwa italia.
Wale waliokuwa wakiangamia katika nchi
ya Ashuru, nao wale waliokuwa uhamishoni
katika nchi ya Misri watakuja na kumwabudu
Mwenyezi Mungu katika mlima mtakatifu huko
Yerusalemu.

# 28

### *Ole wa Efraimu*

1 Ole kwa lile taji la maua, kiburi cha walevi wa Efraimu,
kwa ua linalosinyaa, uzuri wa utukufu wake,
uliowekwa kwenye kichwa cha bonde lenye rutuba:
kwa ule mji, kiburi cha wale walioshushwa na mvinyo!
2 Tazama, Bwana anaye mmoja aliye na uwezo na nguvu.

Kama dhoruba ya mvua ya mawe na upepo unaoharibu,
kama mvua inayonyesha kwa nguvu na mafuriko yanayoshuka,
atakiangusha chini kwa nguvu.
3 Lile taji la maua, kiburi cha walevi cha Efraimu,
kitakanyagwa chini ya nyayo.
4 Lile ua linalosinyaa, uzuri wa utukufu wake,
uliowekwa kwenye kichwa cha bonde lenye rutuba,
litakuwa kama tini iliyoiva kabla ya mavuno:
mara mtu aionapo, huichuma na kuila.

5 Katika siku ile, Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
atakuwa taji la utukufu,
taji zuri la maua
kwa mabaki ya watu wake.
6 Atakuwa roho ya haki
kwa yeye anayeketi kwenye kiti cha hukumu,
chanzo cha nguvu
kwa wale wazuiao vita langoni.

7 Hawa pia wanapepesuka kwa sababu ya mvinyo,
wanayumbayumba kwa sababu ya kileo:
Makuhani na manabii wanapepesuka kwa sababu ya kileo,
wanachanganyikiwa kwa sababu ya mvinyo;
wanapepesuka wanapoona maono,
wanajikwaa wanapotoa maamuzi.
8 Meza zote zimejawa na matapishi

wala hakuna sehemu hata ndogo
isiyokuwa na uchafu.

9 “Yeye anajaribu kumfundisha nani?
Yeye anamwelezea nani ujumbe wake?
Je, ni kwa watoto walioachishwa kunyonya?
Je, ni wale ambao ndipo tu wametolewa matitini?
10 Kwa maana ni:
Amri juu ya amri, amri juu ya amri,
kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni;
hapa kidogo, kule kidogo.”

11 Sawa kabisa, kwa midomo migeni
na kwa lugha ngeni,
Mungu atasema na watu hawa,
12 wale ambao aliwaambia,
“Hapa ni mahali pa kupumzika,
waliochoka na wapumzike,”
na, “Hapa ni mahali pa mapumziko,”
lakini hawakutaka kusikiliza.
13 Hivyo basi, neno la Mwenyezi Mungu kwao litakuwa:
Amri juu ya amri, amri juu ya amri,
kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni,
hapa kidogo, kule kidogo:
ili waende na kuanguka chali,
wakijeruhiwa, wakinaswa na kukamatwa.

14 Kwa hiyo sikieni neno la Mwenyezi Mungu, enyi watu wenye dharau
mnaotawala watu hawa wa Yerusalemu.
15 Ninyi mnajisifu, “Tumefanya agano na mauti,

tumefanya mapatano na Kuzimu*.
Pigo linalofurika litakapopita,
haliwezi kutugusa sisi,
kwa kuwa tumefanya uongo kuwa kimbilio letu
na miungu ya uongo kuwa mahali petu pa kujificha."
16 Kwa hiyo, hili ndilo asemalo Bwana Mungu
Mwenyezi:
"Tazama, ninaweka jiwe katika Sayuni,
jiwe lililojaribiwa,
jiwe la pembeni la thamani kwa ajili ya msingi thabiti.
Yeye atumainiye kamwe hatatiwa hofu.
17 Nitaifanya haki kuwa kamba ya kupimia
na uadilifu kuwa timazi;
mvua ya mawe itafagia kimbilio lenu, huo uongo,
nayo maji yatafurikia mahali penu pa kujificha.
18 Agano lenu na kifo litabatilishwa,
patano lenu na Kuzimu halitasimama.
Pigo linalofurika litakapowakumba,
litawaangusha chini.
19 Kila mara lijapo litawachukua,
asubuhi baada ya asubuhi,
wakati wa mchana na wakati wa usiku,
litawakumba tangu mwanzo hadi mwisho."

Kuuelewa ujumbe huu
utaleta hofu tupu.
20 Kitanda ni kifupi mno kujinyoosha juu yake,
nguo ya kujifunikia ni nyembamba mno

* **28:15** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

mtu hawezi kujifunikia.
21 Mwenyezi Mungu atainuka kama alivyofanya kwenye Mlima Perasimu,
ataghadhibika kama alivyofanya katika Bonde la Gibeoni:
ili kufanya kazi yake, kazi yake ya ajabu,
ili kutimiza kazi yake, kazi yake ngeni.
22 Sasa acheni dharau zenu,
la sivyo minyororo yenu itakuwa mizito zaidi.
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, ameniambia
habari za maangamizi yaliyoamriwa dhidi ya nchi yote.

23 Sikilizeni msikie sauti yangu,
tegeni masikio na msikie niyasemayo.
24 Mkulima anapolima ili apande,
je, hulima siku zote?
Je, huendelea kubomoa ardhi
na kusawazisha udongo?
25 Baada ya kusawazisha shamba,
je, hatapanyi mbegu za bizari na kutawanya jira?
Je, hapandi ngano katika sehemu yake,
shayiri katika eneo lake,
na nafaka nyingine katika shamba lake?
26 Mungu wake humwelekeza
na kumfundisha njia iliyo sahihi.

27 Iliki haipurwi kwa nyundo,
wala gurudumu la gari halivingirishwi juu ya jira;

iliki hupurwa kwa fimbo,
na jira kwa ufito.
28 Nafaka lazima isagwe ili kutengeneza mkate,
kwa hiyo mtu haendelei kuipura daima.
Ingawa huendesha magurudumu ya gari lake la kupuria juu yake,
farasi wake hawasagi.
29 Haya yote pia hutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
mwenye mashauri ya ajabu, na anayepita wote kwa hekima.

# 29

*Ole wa Mji wa Daudi*

1 Ole wako, wewe Arieli, Arieli,
mji alimokaa Daudi!
Ongezeni mwaka kwa mwaka,
na mzunguko wa sikukuu zenu uendelee.
2 Hata hivyo nitauzingira Arieli kwa jeshi,
utalia na kuomboleza,
utakuwa kwangu kama mahali
pa kuwashia moto madhabahuni.
3 Nitapiga kambi pande zote dhidi yako,
nitakuzunguka kwa minara
na kujenga ngome yakukuzingira.
4 Utakaposhushwa, utanena kutoka ardhini,
utamumunya maneno yako kutoka mavumbini.
Sauti yako itatoka katika nchi kama vile ya mzimu,
utanong'ona maneno yako toka mavumbini.

5 Lakini adui zako wengi watakuwa kama vumbi laini;
makundi ya watu wakatili watakuwa
kama makapi yanayopeperushwa.
Naam, ghafula, mara moja,
6 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni atakuja
na ngurumo, tetemeko la ardhi, na kwa sauti kuu,
atakuja na dhoruba, tufani na miali ya moto iteketezayo.
7 Kisha makundi ya mataifa yote yanayopigana dhidi ya Arieli,
yale yanayomshambulia yeye na ngome zake,
na kumzingira kwa jeshi,
watakuwa kama ilivyo ndoto,
kama maono wakati wa usiku:
8 kama vile mtu aliye na njaa aotavyo kuwa anakula,
lakini huamka, bado njaa yake ingalipo,
kama vile mtu mwenye kiu aotavyo kuwa anakunywa maji,
lakini huamka akiwa anazimia, akiwa bado angali ana kiu.
Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa makundi yote ya mataifa
yanayopigana dhidi ya Mlima Sayuni.

9 Pigweni na butwaa na mshangae;
jifanyeni vipofu wenyewe na msione;
leweni, lakini si kwa mvinyo,
pepesukeni lakini si kwa kileo.

10 Mwenyezi Mungu amewaleteeni usingizi mzito:
Ameziba macho yenu ninyi manabii;
amefunika vichwa vyenu ninyi waonaji.
11 Kwenu ninyi, maono haya yote si kitu ila ma-
neno yaliyotiwa muhuri katika kitabu. Mkimpa
mtu yeyote awezaye kusoma kitabu hiki, nanyi
mkamwambia, “Tafadhali kisome,” yeye atajibu,
“Mimi siwezi, kwa kuwa kimetiwa muhuri.”
12 Au mkimpa mtu yeyote kitabu hiki
asiyeweza kusoma na kumwambia, “Tafadhali
kisome,” atajibu, “Mimi sijui kusoma.”
13 Bwana asema:
“Watu hawa hunikaribia kwa vinywa vyao
na kuniheshimu kwa midomo yao,
lakini mioyo yao iko mbali nami.
Ibada yao kwangu inatokana na maagizo
waliyofundishwa na wanadamu.
14 Kwa hiyo mara nyingine tena nitawashangaza watu hawa,
kwa ajabu juu ya ajabu.
Hekima ya wenye hekima itapotea,
nayo akili ya wenye akili itatoweka.”
15 Ole kwa wale wanaoenda kwenye vilindi virefu
kumficha Mwenyezi Mungu mipango yao,
wafanyao kazi zao gizani na kufikiri,
“Ni nani anayetuona? Ni nani atakayejua?”
16 Mnapindua mambo juu chini,
kana kwamba mfinyanzi aweza kufikiriwa kuwa kama udongo wa mfinyanzi!
Je, kile kilichofinyangwa
chaweza kumwambia yule aliyekifinyanga,

“Wewe hukunifinyanga mimi”?
Je, chungu kinaweza kumwambia mfinyanzi,
“Wewe hujui chochote”?

17 Kwa muda mfupi sana, je, Lebanoni haitageuzwa
kuwa shamba lenye rutuba,
na shamba lenye rutuba
liwe kama msitu?
18 Katika siku ile viziwi watasikia maneno ya kitabu,
na katika utusitusi na giza
macho ya kipofu yataona.
19 Mara nyingine tena wanyenyekevu watafurahi katika Mwenyezi Mungu,
wahitaji watafurahi ndani yake Aliye Mtakatifu wa Israeli.
20 Wakatili watatoweka na wenye kudhihaki watatokomea,
nao wote wenye jicho la uovu watakatiliwa mbali,
21 wale ambao kwa neno humfanya mtu kuwa mwenye hatia,
wamtegeao mtego mtetezi katika mahakama,
na kwa ushuhuda wa uongo humnyima haki
yeye asiye na hatia.
22 Kwa hiyo hili ndilo Mwenyezi Mungu, aliyemkomboa Ibrahimu, analosema kwa nyumba ya Yakobo:
“Yakobo hataaibishwa tena,
wala nyuso zao hazitabadilika sura tena.
23 Watakapoona watoto wao miongoni mwao,

kazi ya mikono yangu,
watalitakasa Jina langu takatifu;
wataukubali utakatifu wa yeye Aliye Mtakatifu wa Yakobo,
nao watamcha Mungu wa Israeli.
24 Wale wanaopotoka rohoni watapata ufahamu,
nao wale wanaolalamika watayakubali mafundisho.”

# 30

*Ole wa taifa kaidi*

1 Mwenyezi Mungu asema,
“Ole kwa watoto wakaidi,
kwa wale wanaotimiza mipango ambayo si yangu,
wakifanya makubaliano, lakini si kwa Roho wangu Mtakatifu,
wakilundika dhambi juu ya dhambi,
2 wale wanaoshuka kwenda Misri
bila kutaka ushauri wangu,
wanaotafuta msaada wa ulinzi wa Farao,
wanaotafuta kivuli cha Misri kiwe kimbilio.
3 Lakini ulinzi wa Farao utakuwa kwa aibu yenu,
kivuli cha Misri kitawaletea fedheha.
4 Ingawa wana maafisa katika Soani
na wajumbe wamewasili katika Hanesi,
5 kila mmoja ataaibishwa
kwa sababu ya taifa lisilowafaa kitu,
ambalo haliwaletei msaada wala faida,
bali aibu tu na fedheha.”
6 Neno la unabii kuhusu wanyama wa Negebu:
Katika nchi ya taabu na shida,
ya simba za dume na jike,

ya nyoka mwenye sumu kali na nyoka warukao,
wajumbe huchukua utajiri wao juu ya migongo ya punda,
hazina zao juu ya nundu za ngamia,
kwa lile taifa lisilokuwa na faida,
7 kuvipeleka Misri,
ambaye msaada wake haufai kabisa.
Kwa hiyo nimemwita "Rahabu Asiyefanya Chochote."

8 Nenda sasa, liandike neno hili juu ya kibao kwa ajili yao,
liandike kwenye kitabu,
ili liweze kuwa shahidi milele
kwa ajili ya siku zijazo.
9 Hawa ni watu waasi, watoto wadanganyifu,
watoto ambao hawataki kusikiliza mafundisho ya Mwenyezi Mungu.
10 Wanawaambia waonaji,
"Msione maono tena!"
Nako kwa manabii wanasema,
"Msiendelee kutupatia maono
ambayo ni ya kweli!
Tuambieni mambo ya kupendeza,
tabirini mambo ya uongo.
11 Acheni njia hii,
ondokeni katika mapito haya,
nanyi acheni kutukabili pamoja
na yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli!"
12 Kwa hiyo, hili ndilo asemalo yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli:
"Kwa sababu mmekataa ujumbe huu,

mkategemea uonevu na kutumainia udanganyifu,
13 dhambi hii itakuwa kwenu
kama ukuta mrefu,
wenye ufa na wenye kubetuka,
ambao unaanguka ghafula,
mara moja.
14 Utavunjika vipande vipande kama chombo cha udongo
ukipasuka pasipo huruma
ambapo katika vipande vyake
hakuna kipande kitakachopatikana
kwa kuukulia makaa kutoka jikoni
au kuchotea maji kisimani."

15 Hili ndilo Bwana Mungu Mwenyezi, yeye
Aliye Mtakatifu wa Israeli, asemalo:

"Katika kutubu na kupumzika ndio wokovu wenu,
katika kutulia na kutumaini ndizo nguvu zenu,
lakini hamkutaka.
16 Mlisema, 'Hapana, tutakimbia kwa farasi.'
Kwa hiyo mtakimbia!
Mlisema, 'Tutakimbia kwa farasi wanaoenda kasi.'
Kwa hiyo wanaowafukuza wataenda kasi!
17 Watu elfu moja watakimbia
kwa ajili ya kitisho cha mtu mmoja,
kwa vitishio vya watu watano
wote mtakimbia,
hadi mtakapoachwa kama mlingoti wa bendera
juu ya kilele cha mlima,
kama bendera juu ya kilima."

18 Hata hivyo Mwenyezi Mungu anatamani kutupatia neema,
anainuka ili kuwaonesha huruma.
Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni Mungu wa haki.
Wamebarikiwa wote wanaomngojea yeye!

19 Enyi watu wa Sayuni, mnaoishi Yerusalemu,
hamtalia tena. Tazameni jinsi atakavyokuwa na
huruma mtakapolia kwa kumwomba msaada!
Mara asikiapo, atawajibu.
20 Ingawa Bwana huwapa chakula cha shida na
maji ya taabu, walimu wenu hawatafichwa tena,
kwa macho yenu wenyewe mtawaona.
21 Mkigeuka kuume au kushoto, masikio yenu
yatasikia sauti nyuma yenu ikisema, “Hii ndiyo
njia, ifuateni.”
22 Kisha mtanajisi sanamu zenu zilizofunikwa
kwa fedha, na vinyago vyenu vilivyofunikwa
kwa dhahabu. Mtazitupilia mbali kama vitambaa vya wakati wa hedhi na kuziambia, “Haya,
tokeni hapa!”

23 Pia atawapa mvua kwa ajili ya mbegu mnazootesha ardhini, chakula kinachotoka ardhini
kitakuwa kizuri sana, tena tele. Katika siku ile,
ng’ombe wenu watalisha katika shamba pana la
majani.
24 Maksai na punda walimao watakula majani
makavu na vyakula vilivyotengenezwa, vinavyotandazwa kwa uma na sepeto.
25 Katika siku ile ya mauaji makuu, wakati minara itakapoanguka, vijito vya maji vitatiririka
juu ya kila mlima mrefu na kila kilima kilichoinuka sana.

26 Mwezi utaangaza kama jua, nao mwanga wa
jua utang'aa mara saba zaidi, kama nuru ya siku
saba, wakati Mwenyezi Mungu atakapoyafunga
majeraha ya watu wake na kuwaponya vidonda
alivyowatia.
27 Tazama, Jina la Mwenyezi Mungu linakuja kutoka mbali,
likiwa na hasira kali inayowaka
pamoja na wingu zito la moshi,
midomo yake imejaa ghadhabu
na ulimi wake ni moto ulao.
28 Pumzi yake ni kama mkondo wa maji yaendayo kasi,
yakipanda hadi shingoni.
Hutikisa mataifa katika chujio ya uharibifu,
huweka lijamu katika mataya ya mataifa
ambayo huwaongoza upotevuni.
29 Nanyi mtaimba kama usiku ule mnaadhimisha sikukuu takatifu.
Mioyo yenu itashangilia
kama vile watu wanapokwea na filimbi
kwenye mlima wa Mwenyezi Mungu,
kwa Mwamba wa Israeli.
30 Mwenyezi Mungu atawasababisha watu waisikie sauti yake ya utukufu,
naye atawafanya wauone mkono wake ukishuka
pamoja na hasira yake kali na moto ulao,
kukiwa na tufani ya mvua,
ngurumo za radi na mvua ya mawe.
31 Sauti ya Mwenyezi Mungu itaivunjavunja Ashuru,
kwa fimbo yake ya utawala atawapiga.

32 Kila pigo Mwenyezi Mungu atakaloliweka juu yao
kwa fimbo yake ya kuadhibu,
litakuwa kwa wimbo wa matari na vinubi,
anapopigana nao katika vita
kwa mapigo ya mkono wake.
33 Tofethi pameandaliwa toka zamani,
pamewekwa tayari kwa ajili ya mfalme.
Shimo lake la moto limetengenezwa kwa kina kirefu
na kwa upana mkubwa,
likiwa na moto na kuni tele;
pumzi ya Mwenyezi Mungu,
kama kijito cha kiberiti,
huuwasha moto.

# 31

*Ole wa wale wanaotegemea Misri*

1 Ole wao wale wanaoshuka Misri kutafuta msaada,
wale wanaotegemea farasi,
wanaoweka tumaini katika wingi wa magari yao ya vita,
na katika nguvu nyingi za wapanda farasi,
lakini hawamwangalii yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli,
wala hawatafuti msaada kwa Mwenyezi Mungu.
2 Hata hivyo yeye pia ana hekima na anaweza kuleta maafa,
wala hayatangui maneno yake.
Yeye atainuka dhidi ya nyumba ya mwovu,
dhidi ya wale ambao huwasaidia watenda maovu.

3 Lakini Wamisri ni wanadamu, wala si Mungu,
farasi wao ni nyama, wala si roho.
Mwenyezi Mungu atakaponyoosha Mkono wake,
yeye anayesaidia atajikwaa,
naye anayesaidiwa ataanguka,
wote wawili wataangamia pamoja.
4 Hili ndilo Mwenyezi Mungu analoniambia:
“Kama vile simba angurumavyo,
simba mkubwa juu ya mawindo yake:
hata ingawa kundi lote la wafugaji
huitwa pamoja dhidi yake,
hatiwi hofu na kelele zao,
wala kusumbuliwa na ghasia zao;
ndivyo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni atakavyoshuka
kufanya vita juu ya Mlima Sayuni
na juu ya vilele vyake.
5 Kama ndege warukao,
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni
ataukinga Yerusalemu;
ataukinga na kuuokoa,
atapita juu yake na kuufanya salama.”
6 Mrudieni yeye ambaye nyumba ya Israeli
imemwasi sana.
7 Kwa kuwa katika siku ile kila mmoja wenu
atazikataa sanamu za fedha na za dhahabu zili-
zotengenezwa kwa mikono yenu yenye dhambi.
8 “Ashuru itaanguka kwa upanga ambao si wa mwanadamu;
upanga usio wa kibinadamu utawaangamiza.

Watakimbia mbele ya upanga
na vijana wao wa kiume watafanyizwa kazi kwa lazima.
9 Ngome zao zitaanguka kwa sababu ya hofu;
kwa kuona bendera ya vita,
majemadari wao watashikwa na hofu ya ghafula,"
asema Mwenyezi Mungu,
ambaye moto wake uko Sayuni,
nalo tanuru lake liko Yerusalemu.

# 32

*Ufalme wa haki*

1 Tazama, mfalme atatawala kwa uadilifu
na watawala watatawala kwa haki.
2 Kila mtu atakuwa kama kivuli cha kujificha kutokana na upepo
na kimbilio kutokana na dhoruba,
kama vijito vya maji jangwani
na kivuli cha mwamba mkubwa katika ardhi yenye kiu.

3 Ndipo macho ya wale wanaoona hayatafumbwa tena,
nayo masikio ya wale wanaosikia yatasikiliza.
4 Moyo wa mtu mwenye hamaki utafahamu na kuelewa,
nao ulimi wenye kigugumizi utanena kwa ufasaha.
5 Mpumbavu hataitwa tena muungwana,
wala mtu mbaya kabisa kupewa heshima ya juu.
6 Kwa kuwa mpumbavu hunena upumbavu,

moyo wake hushughulika na uovu:
Hutenda mambo yasiyo ya kumcha Mungu,
na hueneza habari za makosa kuhusu Mwenyezi Mungu;
yeye huwaacha wenye njaa bila kitu,
na wenye kiu huwanyima maji.
7 Taratibu za mtu mbaya kabisa ni ovu,
hufanya mipango miovu
ili kumwangamiza maskini kwa uongo,
hata wakati hoja za mhitaji ni za haki.
8 Lakini mtu muungwana hufanya mipango ya kiungwana,
na kwa matendo ya kiungwana yeye hufanikiwa.

### *Wanawake wa Yerusalemu*

9 Enyi wanawake wenye kuridhika sana,
amkeni na mnisikilize.
Enyi binti mnaojisikia kuwa salama,
sikieni lile ninalotaka kuwaambia!
10 Muda zaidi kidogo ya mwaka mmoja,
ninyi mnaojisikia salama mtatetemeka,
mavuno ya zabibu yatakoma,
na mavuno ya matunda hayatakuwepo.
11 Tetemekeni, enyi wanawake wenye kuridhika,
tetemekeni kwa hofu, enyi binti mnaojisikia salama!
Vueni nguo zenu,
vaeni magunia viunoni mwenu.
12 Pigeni vifua vyenu, mlilie mashamba yenu mazuri,
kwa ajili ya mizabibu iliyozaa vizuri
13 na kwa ajili ya nchi ya watu wangu,
nchi ambayo miiba na michongoma imemea:

naam, ombolezeni kwa ajili ya nyumba zote za furaha
na kwa ajili ya mji huu wenye kufanya sherehe.
14 Ngome itaachwa,
mji wenye kelele nyingi utahamwa,
ngome ndani ya mji na mnara wa ulinzi vitakuwa ukiwa milele,
mahali pazuri pa punda-mwitu na malisho ya makundi ya kondoo,
15 hadi Roho wa Mungu amwagwe juu yetu kutoka juu,
nalo jangwa kuwa shamba lenye rutuba,
na shamba lenye rutuba kuwa kama msitu.
16 Haki itakaa katika jangwa,
na uadilifu utakaa katika shamba lenye rutuba.
17 Matunda ya haki yatakuwa amani,
matokeo ya haki yatakuwa utulivu
na matumaini milele.
18 Watu wangu wataishi katika makao ya mahali pa amani,
katika nyumba zilizo salama,
katika mahali pa kupumzika pasipo na usumbufu.
19 Hata mvua ya mawe iangushe msitu
na mji ubomolewe kabisa,
20 tazama jinsi utakavyobarikiwa,
ukipanda mbegu yako katika kila kijito,
na kuwaacha ng'ombe wako
na punda wajilishe kwa uhuru.

# 33

*Taabu na msaada*

1 Ole wako wewe, ee mharibu,
wewe ambaye hukuharibiwa!
Ole wako, ee msaliti,
wewe ambaye hukusalitiwa!
Utakapokwisha kuharibu,
utaharibiwa;
utakapokwisha kusaliti,
utasalitiwa.

2 Ee Mwenyezi Mungu, uturehemu,
tunakutamani.
Uwe nguvu yetu kila asubuhi
na wokovu wetu wakati wa taabu.
3 Kwa ngurumo ya sauti yako, mataifa yanakimbia;
unapoinuka, mataifa hutawanyika.
4 Mateka yenu, enyi mataifa, yamevunwa
kama wafanyavyo madumadu,
watu huvamia juu yake
kama kundi la nzige.

5 Mwenyezi Mungu ametukuka, kwa kuwa anakaa mahali palipoinuka,
ataijaza Sayuni kwa haki na uadilifu.
6 Atakuwa msingi ulio imara kwa wakati wenu,
hazina ya wokovu tele, hekima na maarifa;
kumcha Mwenyezi Mungu ni ufunguo wa hazina hii.

7 Angalia, mashujaa wake wanapiga kelele barabarani,
wajumbe wa amani wanalia kwa uchungu.

8 Njia kuu zimeachwa,
hakuna wasafiri barabarani.
Mkataba umevunjika,
mashahidi wake wamedharauliwa*,
hakuna anayeheshimiwa.
9 Ardhi inaomboleza† na kuchakaa,
Lebanoni imeaibika na kunyauka;
Sharoni ni kama Araba,
nayo Bashani na Karmeli
wanapukutisha majani yao.

10 "Sasa nitainuka," asema Mwenyezi Mungu.
"Sasa nitatukuzwa;
sasa nitainuliwa juu.
11 Mlichukua mimba ya makapi,
mkazaa mabua;
pumzi yenu ni moto unaowateketeza.
12 Mataifa watachomwa wawe majivu;
kama vichaka vya miiba vilivyokatwa ndivyo watakavyochomwa."

13 Ninyi mlio mbali sana, sikieni lile nililofanya;
ninyi mlio karibu, tambueni uweza wangu!
14 Wenye dhambi katika Sayuni wametiwa hofu,
kutetemeka kumewakumba wasiomcha Mungu:
"Ni nani miongoni mwetu awezaye kuishi na moto ulao?
Ni nani miongoni mwetu awezaye kuishi na moto unaowaka milele?"
15 Yeye aendaye kwa uadilifu
na kusema lililo haki,

* **33:8** au *miji yake imedharauliwa* † **33:9** au *Ardhi inakauka*

yeye anayekataa faida ipatikanayo kwa dhuluma
na kuizuia mikono yake isipokee rushwa,
yeye azuiaye masikio yake dhidi ya mashauri ya mauaji,
na yeye afumbaye macho yake yasitazame uovu:
16 huyu ndiye mtu atakayeishi mahali pa juu,
ambaye kimbilio lake litakuwa ngome ya mlimani.
Atapewa mkate wake,
na maji yake hayatakoma.

17 Macho yenu yatamwona mfalme katika uzuri wake
na kuiona nchi inayoenea mbali.
18 Katika mawazo yenu mtaifikiria hofu iliyopita:
“Yuko wapi yule afisa mkuu?
Yuko wapi yule aliyechukua ushuru?
Yuko wapi afisa msimamizi wa minara?”
19 Hutawaona tena wale watu wenye kiburi,
wale watu wenye usemi wa mafumbo,
wenye lugha ngeni, isiyoeleweka.

20 Mtazame Sayuni, mji wa sikukuu zetu;
macho yenu yatauona Yerusalemu,
mahali pa amani pa kuishi, hema ambalo halitaondolewa,
nguzo zake hazitang’olewa kamwe,
wala hakuna kamba yake yoyote itakayokatika.
21 Huko Mwenyezi Mungu atakuwa Mwenye Nguvu wetu.

Patakuwa kama mahali pa mito mipana na vijito.
Hakuna jahazi lenye makasia litakalopita huko,
wala hakuna meli yenye nguvu itakayopita huko.
22 Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni mwamuzi wetu,
Mwenyezi Mungu ndiye mtoa sheria wetu,
Mwenyezi Mungu ni mfalme wetu,
yeye ndiye atakayetuokoa.

23 Kamba zenu za merikebu zimelegea:
Mlingoti haukusimama imara,
nalo tanga halikukunjuliwa.
Wingi wa mateka yatagawanywa,
hata yeye aliye mlemavu atachukua nyara.
24 Hakuna yeyote aishiye Sayuni atakayesema,
“Mimi ni mgonjwa”;
nazo dhambi za wale wanaoishi humo zitasamehewa.

# 34

*Hukumu dhidi ya mataifa*

1 Njooni karibu, enyi mataifa, nanyi msikilize;
sikilizeni kwa makini,
enyi makabila ya watu!
Dunia na isikie, navyo vyote vilivyo ndani yake,
ulimwengu na vyote vinavyotoka ndani yake!
2 Mwenyezi Mungu ameyakasirikia mataifa yote;
ghadhabu yake ni juu ya majeshi yao yote.
Atawaangamiza kabisa,
atawatia mikononi mwa wachinjaji.

3 Waliouawa watatupwa nje,
maiti zao zitatoa uvundo,
milima itatota kwa damu zao.
4 Nyota zote za mbinguni zitayeyuka
na mbingu itakunjwa kama kitabu,
jeshi lote la angani litaanguka
kama majani yaliyonyauka kwenye mzabibu,
kama tini iliyonyauka kwenye mtini.

5 Upanga wangu umekunywa na kushiba huko mbinguni,
tazama, unashuka katika hukumu juu ya Edomu,
wale watu ambao nimeshawahukumu,
kuwaangamiza kabisa.
6 Upanga wa Mwenyezi Mungu umeoga katika damu,
umefunikwa na mafuta ya nyama:
damu ya kondoo na mbuzi,
mafuta kutoka figo za kondoo dume.
Kwa maana Mwenyezi Mungu ana dhabihu huko Bosra,
na machinjo makuu huko Edomu.
7 Nyati wataanguka pamoja nao,
ndama dume na mafahali wakubwa.
Nchi yao italowana kwa damu,
nayo mavumbi yataloa mafuta ya nyama.

8 Kwa sababu Mwenyezi Mungu anayo siku ya kulipiza kisasi,
mwaka wa malipo,
siku ya kushindania shauri la Sayuni.

9 Vijito vya Edomu vitageuka kuwa lami,
mavumbi yake yatakuwa kiberiti kiunguza-cho,
nchi yake itakuwa lami iwakayo!
10 Haitazimishwa usiku wala mchana,
moshi wake utapaa juu milele.
Kizazi hadi kizazi itakuwa ukiwa;
hakuna mtu yeyote atakayepita huko tena.
11 Bundi wa jangwani na bundi mwenye sauti nyembamba wataimiliki,
bundi wakubwa na kunguru wataweka viota humo.
Mungu atanyoosha juu ya Edomu
kamba ya kupimia ya machafuko matupu,
na timazi ya ukiwa.
12 Watu wake wa kuheshimiwa hawatakuwa na chochote
kitakachoitwa ufalme huko,
nao wakuu wao wote watatoweka.
13 Miiba itaenea katika ngome za ndani,
viwawi na michongoma itaota
kwenye ngome zake.
Itakuwa maskani ya mbweha,
makao ya bundi.
14 Viumbe vya jangwani vitakutana na fisi,
nao mbuzi-mwitu watalia wakiitana;
huko viumbe vya usiku vitastarehe pia
na kujitafutia mahali pa kupumzika.
15 Bundi wataweka viota huko na kutaga mayai,
atayaangua na kutunza makinda yake
chini ya uvuli wa mabawa yake;
pia huko vipanga watakusanyika,
kila mmoja na mwenzi wake.

16 Angalieni katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na msome:
Hakuna hata mmoja katika hawa atakayekosekana,
hakuna hata mmoja atakayemkosa mwenzi wake.
Kwa kuwa ni kinywa chake Mungu kimeagiza,
na Roho wake Mtakatifu atawakusanya.
17 Huwagawia sehemu zao,
mkono wake huwagawanyia kwa kipimo.
Wataimiliki hata milele
na kuishi humo kizazi hadi kizazi.

# 35

### *Furaha ya waliokombolewa*

1 Jangwa na nchi kame vitafurahi;
nyika itashangilia na kuchanua maua.
Kama waridi,
2 litachanua maua,
litashangilia sana na kupaza sauti kwa furaha.
Litapewa utukufu wa Lebanoni,
fahari ya Karmeli na Sharoni;
wataona utukufu wa Mwenyezi Mungu,
fahari ya Mungu wetu.

3 Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu,
yafanyeni imara magoti yaliyolegea,
4 waambieni wale wenye mioyo ya hofu,
“Kuweni hodari, msiogope;
tazama, Mungu wenu atakuja kulipa kisasi,
pamoja na ujira wake,
atakuja na kuwaokoa.”

5 Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa
na masikio ya viziwi yatazibuliwa.
6 Ndipo kilema atarukaruka kama kulungu,
nao ulimi wa aliye bubu utapaza sauti kwa shangwe.
Maji yatatiririka kwa kasi katika nyika,
na vijito katika jangwa.
7 Mchanga wa moto utakuwa bwawa la maji,
ardhi yenye kiu itabubujika chemchemi.
Maskani ya mbweha walikolala hapo awali
patamea nyasi, matete na mafunjo.

8 Nako kutakuwa na njia kuu,
nayo itaitwa Njia ya Utakatifu.
Wasio safi hawatapita juu yake;
itakuwa ya wale wanaotembea katika Njia Ile;
yeye asafiriye juu yake,
ajapokuwa mjinga, hatapotea.
9 Huko hakutakuwa na simba,
wala mnyama mkali hatapita njia hiyo;
hawatapatikana humo.
Ila waliokombolewa tu ndio watakaopita huko,
10 waliokombolewa na Mwenyezi Mungu watarudi.
Wataingia Sayuni wakiimba;
furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao.
Watapata furaha na shangwe;
huzuni na majonzi vitakimbia.

# 36

*Senakeribu atishia Yerusalemu*
*(2 Wafalme 18:13-27; 2 Nyakati 32:1-19)*

1 Katika mwaka wa kumi na nne wa utawala
wa Mfalme Hezekia, Senakeribu mfalme wa Ashuru akaishambulia miji yote ya Yuda yenye ngome na kuiteka.

2 Kisha mfalme wa Ashuru akamtuma jemadari wa jeshi pamoja na jeshi kubwa kutoka Lakishi hadi kwa Mfalme Hezekia huko Yerusalemu. Jemadari wa jeshi akasimama kwenye mfereji wa Bwawa la Juu, lililojengwa katika barabara iendayo kwenye Uwanja wa Dobi.

3 Eliakimu mwana wa Hilkia aliyekuwa msimamizi wa jumba la kifalme, Shebna aliyekuwa katibu, na Yoa mwana wa Asafu mwandishi wakamwendea.

4 Jemadari wa jeshi akawaambia, “Mwambieni Hezekia,

“ ‘Hili ndilo asemalo mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru: Ni wapi unapoweka hili tumaini lako?

5 Unasema mnayo mikakati na nguvu za kijeshi, lakini unasema maneno matupu tu. Je, wewe unamtegemea nani, hata ukaniasi mimi?

6 Tazama sasa, unaitegemea Misri, fimbo ile ya mwanzi uliopasuka, ambayo huuchoma na kuujeruhi mkono wa mtu akiiegemea! Hivyo ndivyo alivyo Farao mfalme wa Misri, kwa wote wanaomtegemea.

7 Nawe ukiniambia, “Tunamtumainia Mwenyezi Mungu, Mungu wetu”: Je, si yeye ambaye Hezekia aliondoa mahali pake pa juu pa kuabudia na madhabahu zake, akiwaambia Yuda na Yerusalemu, “Ni lazima mwabudu mbele ya madhabahu haya”?

8 “ ‘Njooni sasa, fanyeni mapatano na bwana wangu, mfalme wa Ashuru: Nitakupa farasi elfu mbili, kama unaweza kuwapandisha waendesha farasi juu yao!
9 Utawezaje kumzuia hata afisa mmoja aliye mdogo kati ya maafisa wa bwana wangu, ijapo unategemea Misri kwa magari ya vita na wapanda farasi?
10 Zaidi ya hayo, je, nimekuja kushambulia na kuangamiza nchi hii bila Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye aliniambia niishambulie nchi hii na kuiangamiza.’ ”

11 Ndipo Eliakimu, Shebna na Yoa wakamwambia yule jemadari wa jeshi, “Tafadhali zungumza na watumishi wako kwa lugha ya Kiaramu, kwa kuwa tunaifahamu. Usiseme nasi kwa Kiebrania watu walio juu ya ukuta wakiwa wanasikia.”

12 Lakini yule jemadari wa jeshi akajibu, “Je, bwana wangu amenituma kutoa ujumbe huu kwa bwana wenu na kwenu tu? Je, hakunituma pia kwa watu walioketi ukutani, ambao, kama ninyi, itawabidi kula mavi yao na kunywa mkojo wao wenyewe?”

13 Kisha yule jemadari wa jeshi akasimama na kuita kwa lugha ya Kiebrania, akasema: “Sikieni maneno ya mfalme mkuu, mfalme wa Ashuru!
14 Hili ndilo asemalo mfalme: Msikubali Hezekia awadanganye. Hawezi kuwaokoa!
15 Msikubali Hezekia awashawishi kumtumaini Mwenyezi Mungu kwa kuwaambia, ‘Hakika Mwenyezi Mungu atatuokoa. Mji

huu hautaangukia mikononi mwa mfalme wa Ashuru.’

16 “Msimsikilize Hezekia. Hili ndilo mfalme wa Ashuru asemalo: Fanyeni amani nami na mje kwangu. Kisha kila mmoja wenu atakula kutoka kwa mzabibu wake na mtini wake mwenyewe, na kunywa maji kutoka kisima chake mwenyewe,
17 hadi nije nikawapeleke katika nchi iliyo kama nchi yenu wenyewe, nchi ya nafaka na divai mpya, nchi ya mkate na ya mashamba ya mizabibu.

18 “Msikubali Hezekia awapotoshe asemapo, ‘Mwenyezi Mungu atatuokoa.’ Je, yuko mungu wa taifa lolote aliyewahi kuokoa nchi yake kutoka mkononi mwa mfalme wa Ashuru?
19 Iko wapi miungu ya Hamathi na ya Arpadi? Iko wapi miungu ya Sefarvaimu? Je, imeokoa Samaria kutoka mkononi mwangu?
20 Ni yupi miongoni mwa miungu yote ya nchi hizi ameweza kuokoa nchi yake mkononi mwangu? Inawezekanaje basi Mwenyezi Mungu aiokoe Yerusalemu mkononi mwangu?”

21 Lakini wale watu wakakaa kimya, wala hawakujibu lolote, kwa kuwa mfalme alikuwa amewaamuru, “Msimjibu lolote.”

22 Kisha Eliakimu mwana wa Hilkia msimamizi wa jumba la kifalme, Shebna katibu, na Yoa mwana wa Asafu, mwandishi wakamwendea Hezekia, nguo zao zikiwa zimeraruliwa, na kumwambia vile jemadari wa jeshi alivyosema.

# 37

### *Hezekia autafuta msaada wa Mwenyezi Mungu (2 Wafalme 19:1-13)*

1 Mfalme Hezekia aliposikia haya, akararua
nguo zake na kuvaa gunia, na akaenda katika
Hekalu la Mwenyezi Mungu.
2 Akawatuma Eliakimu msimamizi wa nyumba
ya mfalme, Shebna mwandishi, na viongozi wa
makuhani, wote wakiwa wamevaa magunia,
waende kwa nabii Isaya mwana wa Amozi.
3 Wakamwambia, "Hili ndilo asemalo Hezekia:
Siku hii ni siku ya dhiki, ya kukaripiwa na ya
aibu, kama wakati watoto wanapofikia karibu
kuzaliwa na kumbe hakuna nguvu ya kuwazaa.
4 Yamkini Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
atayasikia maneno ya jemadari wa jeshi, ambaye bwana wake, mfalme wa Ashuru, amemtuma kumdhihaki Mungu aliye hai, tena kwamba
atamkemea kwa maneno ambayo Mwenyezi
Mungu, Mungu wako ameyasikia. Kwa hiyo
omba kwa ajili ya mabaki ambao bado wako."
5 Maafisa wa Mfalme Hezekia walipofika kwa
Isaya,
6 Isaya akawaambia, "Mwambieni bwana
wenu, 'Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
Usiogope kwa hayo uliyoyasikia, yale maneno
ambayo watumishi wa mfalme wa Ashuru
wamenitukana nayo.
7 Sikiliza! Nitatia roho fulani ndani yake ili
atakaposikia taarifa fulani, atarudi nchi yake
mwenyewe, nami huko nitafanya auawe kwa
upanga.' "

8 Jemadari wa jeshi aliposikia kwamba
mfalme wa Ashuru ameondoka Lakishi, alirudi,
akamkuta mfalme akipigana na Libna.
9 Basi Senakeribu akapata taarifa kwamba
Tirhaka, Mkushi mfalme wa Misri, alikuwa
anaenda kupigana naye. Aliposikia jambo hili
akatuma wajumbe kwa Hezekia na neno hili:
10 "Mwambieni Hezekia mfalme wa Yuda:
Usikubali huyo Mungu unayemtumainia akudan-
ganye wakati anaposema, 'Yerusalemu haitatiwa
mkononi mwa mfalme wa Ashuru.'
11 Hakika umesikia yale ambayo wafalme
wa Ashuru wametenda kwa nchi zote, waki-
waangamiza kabisa. Je, wewe utaokolewa?
12 Je, miungu ya mataifa ambayo
yaliangamizwa na baba zangu iliweza
kuwaokoa? Yaani miungu ya Gozani, Harani,
Resefu, na ya watu wa Edeni waliokuwa Telasari?
13 Yuko wapi mfalme wa Hamathi, mfalme wa
Arpadi, mfalme wa mji wa Sefarvaimu, au wa
Hena au wa Iva?"

### *Maombi ya Hezekia*

14 Hezekia akapokea barua kutoka kwa wale
wajumbe naye akaisoma. Kisha akapanda katika
Hekalu la Mwenyezi Mungu, akaikunjua mbele
za Mwenyezi Mungu.
15 Naye Hezekia akamwomba Mwenyezi
Mungu akisema:
16 "Ee Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni, Mungu wa Israeli, unayeketi kwenye
kiti cha enzi kati ya makerubi, wewe peke yako
ndiwe Mungu juu ya falme zote za dunia. Wewe
umeumba mbingu na nchi.

17 Tega sikio, Ee Mwenyezi Mungu, usikie;
fungua macho yako, Ee Mwenyezi Mungu, uone;
sikiliza maneno yote ambayo Senakeribu ame-
tuma kumtukana Mungu aliye hai.
18 “Ni kweli, Ee Mwenyezi Mungu, kwamba
wafalme wa Ashuru wameyaangamiza mataifa
haya yote pamoja na nchi zao.
19 Wameitupa miungu yao kwenye moto na
kuiangamiza, kwa kuwa haikuwa miungu, bali
miti na mawe tu, iliyotengenezwa kwa mikono
ya wanadamu.
20 Sasa basi, Ee Mwenyezi Mungu, Mungu wetu,
tuokoe kutoka mkononi mwake, ili falme zote
duniani zipate kujua kwamba wewe peke yako,
Ee Mwenyezi Mungu, ndiwe Mungu pekee.”

### *Kuanguka kwa Senakeribu (2 Wafalme 19:20-37)*

21 Kisha Isaya mwana wa Amozi akapeleka
ujumbe kwa Hezekia, akasema: “Hili ndilo ase-
malo Mwenyezi Mungu, Mungu wa Israeli: Kwa
sababu umeniomba kuhusu Senakeribu mfalme
wa Ashuru,
22 hili ndilo neno ambalo Mwenyezi Mungu
amelisema dhidi yake:
“Bikira Binti Sayuni
anakudharau na kukudhihaki.
Binti Yerusalemu
anatikisa kichwa chake unapokimbia.
23 Ni nani uliyemtukana na kumkufuru?
Ni nani uliyepaza sauti yako dhidi yake,
na kumwinulia macho yako kwa kiburi?
Ni dhidi ya yule Aliye Mtakatifu wa Israeli!
24 Kupitia kwa wajumbe wako

umelundika matukano juu ya Bwana.
Nawe umesema,
‘Kwa magari yangu mengi ya vita,
nimepanda juu ya vilele vya milima,
vilele vya juu sana katika Lebanoni.
Nami nimeiangusha mierezi yake mirefu,
misunobari yake iliyo bora sana.
Nimefikia sehemu zake zilizoinuka juu sana,
misitu yake iliyo mizuri sana.
25 Nimechimba visima katika nchi za kigeni
na kunywa maji yake.
Kwa nyayo za miguu yangu
nimekausha vijito vyote vya Misri.’

26 “Je, hujasikia?
Zamani sana niliamuru hili.
Siku za kale nilipanga hili;
sasa nimelifanya litokee,
kwamba umegeuza miji yenye ngome
kuwa malundo ya mawe.
27 Watu wa miji hiyo wameishiwa nguvu,
wanavunjika mioyo na kuaibishwa.
Wao ni kama mimea katika shamba,
kama machipukizi mororo ya kijani,
kama majani yachipuayo juu ya paa la nyumba,
ambayo hukauka kabla ya kukua.

28 “Lakini ninajua mahali ukaapo,
kutoka kwako na kuingia kwako,
na jinsi unavyoghadhibika dhidi yangu.
29 Kwa sababu unaghadhibika na ufidhuli dhidi yangu,

na kwa sababu ufidhuli wako umefika masikioni mwangu,
nitaweka ndoana yangu puani mwako
na hatamu yangu kinywani mwako,
nami nitakufanya urudi kwa njia ile uliyoijia.
30 “Hii ndiyo itakuwa ishara kwako, ee Hezekia:
“Mwaka huu utakula kile kinachoota chenyewe,
na mwaka wa pili utakula kutoka machipukizi yake.
Lakini katika mwaka wa tatu panda na uvune,
panda mashamba ya mizabibu na ule matunda yake.
31 Mara nyingine tena mabaki ya nyumba ya Yuda
wataeneza mizizi chini na kuzaa matunda juu.
32 Kwa kuwa kutoka Yerusalemu watakuja mabaki,
na kutoka Mlima Sayuni kundi la walionusurika.
Wivu wa Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni,
ndio utatimiza jambo hili.
33 “Kwa hiyo hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu kuhusu mfalme wa Ashuru:
“Hataingia katika mji huu
wala hatapiga mshale hapa.
Hatakuja mbele yake na ngao
wala kupanga majeshi kuuzingira.
34 Kwa njia ile aliyoijia ndiyo atakayorudi;
hataingia katika mji huu,”
asema Mwenyezi Mungu.
35 “Nitaulinda mji huu na kuuokoa,

kwa ajili yangu mwenyewe,
na kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu!”

36 Ndipo malaika wa Mwenyezi Mungu
akaenda, akawaua wanajeshi elfu mia moja na
themanini na tano katika kambi ya Waashuru.
Wenzao walipoamka asubuhi yake, walikuta
maiti kila mahali!
37 Basi Senakeribu mfalme wa Ashuru
akavunja kambi na kuondoka. Akarudi Ninawi
na kukaa huko.
38 Siku moja, alipokuwa akiabudu katika
hekalu la mungu wake Nisroki, wanawe
Adrameleki na Shareza wakamuua kwa upanga,
nao wakakimbilia nchi ya Ararati. Naye Esar-
Hadoni mwanawe akawa mfalme baada yake.

# 38

### *Ugonjwa wa Hezekia*
### *(2 Wafalme 20:1-11; 2 Nyakati 32:24-26)*

1 Katika siku hizo Hezekia akaugua, naye
akawa karibu kufa. Nabii Isaya mwana wa
Amozi akaenda kwake na kumwambia, “Hili
ndilo asemalo Mwenyezi Mungu: Tengeneza
mambo ya nyumba yako, kwa sababu utakufa,
hutapona.”

2 Hezekia akaelekeza uso wake ukutani, akam-
womba Mwenyezi Mungu:

3 “Ee Mwenyezi Mungu, kumbuka jinsi nilivy-
oenenda mbele zako kwa uaminifu na kuji-
toa kwa moyo wangu wote, na kufanya yaliyo
mema machoni pako.” Naye Hezekia akalia kwa
uchungu.

4 Ndipo neno la Mwenyezi Mungu likamjia
Isaya, kusema:
5 “Nenda ukamwambie Hezekia, ‘Hili ndilo ase-
malo Mwenyezi Mungu, Mungu wa baba yako
Daudi: Nimeyasikia maombi yako na nimeona
machozi yako. Nitakuongezea miaka kumi na
tano katika maisha yako.
6 Nami nitakuokoa wewe pamoja na mji huu
kutoka mkononi mwa mfalme wa Ashuru. Ni-
taulinda mji huu.
7 “ ‘Hii ndiyo ishara ya Mwenyezi Mungu kwako
kwamba Mwenyezi Mungu atafanya kile ali-
choahidi:
8 Nitafanya kivuli cha jua kwenye ngazi iliyo-
jengwa na Ahazi kirudi nyuma madaraja kumi.’ ”
Hivyo jua likarudi nyuma madaraja kumi am-
bayo lilikuwa limeshuka.
9 Maandiko ya Hezekia mfalme wa Yuda baada
ya kuugua kwake na kupona:

10 Nilisema, “Katika ustawi wa maisha yangu,
je, ni lazima nipite katika malango ya mauti*,
na kupokonywa miaka yangu iliyobaki?”
11 Nilisema, “Sitamwona tena Mwenyezi Mungu,
Mwenyezi Mungu katika nchi ya walio hai,
wala sitamtazama tena mwanadamu,
wala kuwa na wale ambao sasa wanakaa katika ulimwengu huu.
12 Kama hema la mchunga mifugo,
nyumba yangu imebomolewa na kutwaliwa kutoka kwangu.
Kama mfumaji nimevingirisha maisha yangu,

* **38:10** yaani *Kuzimu*

naye amenikatilia mbali kutoka kitanda cha mfumi.
Mchana na usiku uliyakomesha maisha yangu.
13 Nilingoja kwa uvumilivu hadi mapambazuko,
lakini alivunja mifupa yangu yote kama simba.
Mchana na usiku uliyakomesha maisha yangu.
14 Nililia kama mbayuwayu au korongo,
niliomboleza kama hua aombolezaye.
Macho yangu yalififia nilipotazama mbinguni.
Ee Bwana, ninataabika, njoo unisaidie!"

15 Lakini niseme nini?
Amesema nami, naye yeye mwenyewe amelitenda hili.
Nitatembea kwa unyenyekevu
katika miaka yangu yote
kwa sababu ya haya maumivu makali
ya nafsi yangu.
16 Bwana, kwa mambo kama haya watu huishi,
nayo roho yangu hupata uzima katika hayo pia.
Uliniponya
na kuniacha niishi.
17 Hakika ilikuwa ya faida yangu
ndiyo maana nikapata maumivu makali.
Katika upendo wako ukaniokoa
kutoka shimo la uharibifu;
umeziweka dhambi zangu zote
nyuma yako.

18 Kwa maana kaburi[†] haliwezi kukusifu,
mauti haiwezi kuimba sifa zako;
wale wanaoshuka shimoni
hawawezi kuutarajia uaminifu wako.
19 Walio hai, walio hai: hao wanakusifu,
kama ninavyofanya leo.
Baba huwaambia watoto wao
habari za uaminifu wako.

20 Mwenyezi Mungu ataniokoa,
nasi tutaimba kwa vyombo vya nyuzi
siku zote za maisha yetu
katika Hekalu la Mwenyezi Mungu.
21 Isaya alikuwa amesema, "Tengenezeni dawa
ya kubandika ya tini, mweke juu ya jipu, naye
atapona."
22 Hezekia alikuwa ameuliza, "Kutakuwa na
ishara gani kwamba nitapanda kwenda Hekalu
la Mwenyezi Mungu?"

# 39

### *Wajumbe kutoka Babeli (2 Wafalme 20:12-19)*

1 Wakati huo Merodaki-Baladani, mwana wa
Baladani mfalme wa Babeli, akamtumia Hezekia
barua na zawadi, kwa sababu alikuwa amesikia
habari za kuugua na kupona kwake.
2 Hezekia akawapokea wale wajumbe kwa fu-
raha na kuwaonesha vitu vile vilivyokuwa katika
ghala zake: yaani fedha, dhahabu, vikolezo na
mafuta safi, ghala la silaha lote, na kila kitu kili-
chokuwa katika hazina yake. Hapakuwa na kitu

[†] **38:18** Kaburi hapa maana yake ni *Kuzimu*; kwa Kiebrania ni *Sheol.*

katika jumba lake la kifalme au katika ufalme wake wote ambacho Hezekia hakuwaonesha.
3 Ndipo nabii Isaya akaenda kwa Mfalme Hezekia na kumuuliza, “Watu hao walisema nini, na wametoka wapi?”

Hezekia akamjibu, “Wametoka nchi ya mbali. Walikuja kwangu kutoka Babeli.”

4 Nabii akauliza, “Waliona nini katika jumba lako la kifalme?”

Hezekia akajibu, “Waliona kila kitu katika jumba langu. Hakuna kitu katika hazina yangu ambacho sikuwaonesha.”
5 Ndipo Isaya akamwambia Hezekia, “Sikia neno la Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni:
6 Hakika wakati unakuja ambapo vitu vyote katika jumba lako la kifalme, na vyote ambavyo baba zako waliweka akiba hadi siku hii, vitachukuliwa kwenda Babeli. Hakuna chochote kitakachosalia, asema Mwenyezi Mungu.
7 Nao baadhi ya wazao wako, mwili wako na damu yako mwenyewe watakaozaliwa kwako, watachukuliwa mbali, nao watakuwa matowashi katika jumba la mfalme wa Babeli.”
8 Hezekia akamjibu Isaya, “Neno la Mwenyezi Mungu ulilosema ni jema.” Kwa kuwa alifikiri, “Kutakuwa amani na usalama wakati wa uhai wangu.”

# 40

*Faraja kwa watu wa Mwenyezi Mungu*

1 Wafarijini, wafarijini watu wangu,
asema Mungu wenu.

2 Sema na Yerusalemu kwa upole,
umtangazie
kwamba kazi yake ngumu imekamilika,
kwamba dhambi yake imelipiwa fidia,
kwamba amepokea kutoka mkononi mwa Mwenyezi Mungu
maradufu kwa ajili ya dhambi zake zote.

3 Sauti ya mtu aliaye nyikani:
"Itengenezeni njia ya Mwenyezi Mungu jangwani,
yanyoosheni mapito nyikani
kwa ajili ya Mungu wetu.
4 Kila bonde litainuliwa,
kila mlima na kilima kitashushwa;
penye mabonde patanyooshwa,
napo palipoparuza patasawazishwa.
5 Utukufu wa Mwenyezi Mungu utafunuliwa,
nao wanadamu wote watauona pamoja.
Kwa maana kinywa cha Mwenyezi Mungu kimenena."

6 Sauti husema, "Piga kelele."
Nami nikasema, "Nipige kelele gani?"

"Wanadamu wote ni kama majani,
nao utukufu wao wote
ni kama maua ya kondeni.
7 Majani hunyauka na maua huanguka,
kwa sababu pumzi ya Mwenyezi Mungu huyapuliza.
Hakika wanadamu ni majani.
8 Majani hunyauka na maua huanguka,

lakini neno la Mungu wetu ladumu milele."

9 Wewe uletaye habari njema Sayuni,
panda juu ya mlima mrefu.
Wewe uletaye habari njema Yerusalemu,
paza sauti yako, piga kelele kwa nguvu,
paza sauti, usiogope;
iambie miji ya Yuda,
"Yuko hapa Mungu wenu!"
10 Tazameni, Bwana Mungu Mwenyezi anakuja na nguvu,
nao mkono wake ndio utawalao kwa ajili yake.
Tazameni, ujira wake u pamoja naye,
nayo malipo yake yanafuatana naye.
11 Huchunga kundi lake kama mchungaji wa mifugo:
Hukusanya wana-kondoo katika mikono yake
na kuwachukua karibu na moyo wake,
huwaongoza taratibu wale wanaonyonyesha.

12 Ni nani aliyepima maji ya bahari
kwenye konzi ya mkono wake,
au kuzipima mbingu kwa shibiri yake?
Ni nani aliyeyashika mavumbi ya dunia katika kikapu,
au kupima milima kwenye kipimio
na vilima kwenye mizani?
13 Ni nani aliyeyafahamu mawazo ya Mwenyezi Mungu,
au kumfundisha akiwa kama mshauri wake?

14 Ni nani ambaye Mwenyezi Mungu ametaka shauri kwake ili kumwelimisha,
naye ni nani aliyemfundisha njia iliyo sawa?
Ni nani aliyemfundisha maarifa
au kumwonesha mapito ya ufahamu?

15 Hakika mataifa ni kama tone ndani ya ndoo,
ni kama vumbi jembamba juu ya mizani,
huvipima visiwa kana kwamba vilikuwa vumbi laini.
16 Lebanoni hautoshi kwa moto wa madhabahuni,
wala wanyama wake hawatoshi kwa sadaka za kuteketezwa.
17 Mbele yake mataifa yote ni kama si kitu,
yanaonekana yasio na thamani
na zaidi ya bure kabisa.

18 Basi, utamlinganisha Mungu na nani?
Utamlinganisha na kitu gani?
19 Kwa habari ya sanamu, fundi huisubu,
naye mfua dhahabu huifunika kwa dhahabu
na kuitengenezea mikufu ya fedha.
20 Mtu aliye maskini sana asiyeweza kuleta sadaka kama hii
huuchagua mti usiooza.
Humtafuta fundi stadi
wa kusimamisha sanamu ambayo haitatikisika.

21 Je, hujui?
Je, hujasikia?
Je, hujaambiwa tangu mwanzo?
Je, hujafahamu tangu kuumbwa kwa dunia?

22 Anakaa kwenye kiti cha utawala juu ya duara
ya dunia,
nao watu wanaoishi humo ni kama panzi.
Huzitandaza mbingu kama chandarua,
na kuzitandaza kama hema la kuishi.
23 Huwafanya wakuu kuwa si kitu,
na kuwashusha watawala wa dunia hii kuwa
kitu bure.
24 Mara baada ya kupandwa,
mara baada ya kutiwa ardhini,
mara baada ya kutoa mizizi yao ardhini,
ndipo huwapulizia nao wakanyauka,
nao upepo wa kisulisuli
huwapeperusha kama makapi.

25 “Utanilinganisha mimi na nani?
Au ni nani anayelingana nami?” asema yeye
Aliye Mtakatifu.
26 Inueni macho yenu mtazame mbinguni:
Ni nani aliyeumba hivi vyote?
Ni yeye aletaye nje jeshi la nyota moja baada ya
nyingine
na kuziita kila moja kwa jina lake.
Kwa sababu ya uweza wake mkuu na nguvu zake
kuu,
hakuna hata mojawapo inayokosekana.

27 Kwa nini unasema, ee Yakobo,
nanyi ee Israeli, kulalamika,
“Njia yangu imefichwa Mwenyezi Mungu asiione,
Mungu wangu hajali shauri langu?”
28 Je wewe, hufahamu?
Je wewe, hujasikia?

Mwenyezi Mungu ni Mungu wa milele,
Muumba wa miisho ya dunia.
Hatachoka wala kulegea,
wala hakuna hata mmoja
awezaye kuupima ufahamu wake.
29 Huwapa nguvu waliolegea
na huongeza nguvu za wadhaifu.
30 Hata vijana huchoka na kulegea,
nao vijana wanaume hujikwaa na kuanguka,
31 bali wale wamtumainio Mwenyezi Mungu
atafanya upya nguvu zao.
Watapaa juu kwa mabawa kama tai;
watapiga mbio wala hawatachoka,
watatembea kwa miguu wala hawatazimia.

# 41

*Msaidizi wa Israeli*

1 "Nyamazeni kimya mbele zangu, enyi visiwa!
Mataifa na wafanye upya nguvu zao!
Wao na wajitokeze, kisha waseme,
tukutane pamoja mahali pa hukumu.

2 "Ni nani aliyemchochea mmoja kutoka mashariki,
akimwita katika haki kwa utumishi wake?
Huyatia mataifa mkononi mwake,
na kuwatiisha wafalme mbele zake.
Huwafanya kuwa mavumbi kwa upanga wake,
huwafanya makapi yapeperushwayo na upepo kwa upinde wake.
3 Huwafuatia na kuendelea salama,
katika njia ambayo miguu yake haijawahi kupita.

4 Ni nani aliyefanya jambo hili na kulitimiliza,
akiita vizazi tangu mwanzo?
Mimi, Mwenyezi Mungu, ni wa kwanza,
nami nitakuwa pamoja na wa mwisho:
Mimi ndiye."

5 Visiwa vimeliona na kuogopa,
miisho ya dunia inatetemeka.
Wanakaribia na kuja mbele,
6 kila mmoja humsaidia mwingine
na kusema kwa ndugu yake, "Uwe hodari!"
7 Fundi humtia moyo sonara,
yeye alainishaye kwa nyundo
humhimiza yeye agongeaye kwenye fuawe.
Humwambia yeye aunganishaye, "Ni kazi njema."
Naye huikaza sanamu kwa misumari ili isitikisike.

8 "Lakini wewe, ee Israeli, mtumishi wangu,
Yakobo, niliyemchagua,
ninyi wazao wa Ibrahimu rafiki yangu,
9 nilikuchukua toka miisho ya dunia,
nilikuita kutoka pembe zake za mbali.
Nilisema, 'Wewe ni mtumishi wangu';
nimekuchagua, wala sikukukataa.
10 Hivyo usiogope, kwa maana niko pamoja nawe;
usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako.
Nitakutia nguvu na kukusaidia;
nitakutegemeza kwa mkono wa kuume wa haki yangu.

11 “Wote walioona hasira dhidi yako
hakika wataaibika na kutahayarika,
wale wakupingao
watakuwa kama vile si kitu, na kuangamia.
12 Ingawa utawatafuta adui zako,
hutawaona.
Wale wanaopigana vita dhidi yako
watakuwa kama vile si kitu kabisa.
13 Kwa maana Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
Mungu wako,
nikushikaye mkono wako wa kuume
na kukuambia, Usiwe na hofu,
nitakusaidia.
14 Usiogope, ee Yakobo uliye mdudu,
ee Israeli uliye mdogo,
kwa kuwa Mimi mwenyewe nitakusaidia,”
asema Mwenyezi Mungu,
Mkombozi wako, yeye Aliye Mtakatifu wa
Israeli.
15 “Tazama, nitakufanya chombo cha kupuria,
kipya na chenye makali, chenye meno mengi.
Utaipura milima na kuiponda
na kuvifanya vilima kuwa kama makapi.
16 Utaipepeta, nao upepo utaichukua,
dhoruba itaipeperushia mbali.
Bali wewe utajifurahisha katika Mwenyezi
Mungu
na katika utukufu wa yeye Aliye Mtakatifu
wa Israeli.

17 “Maskini na wahitaji wanatafuta maji,
lakini hayapo,
ndimi zao zimekauka kwa kiu.
Lakini Mimi Mwenyezi Mungu nitawajibu,

Mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha.
18 Nitaifanya mito itiririke juu ya vilima vilivyo kame,
nazo chemchemi ndani ya mabonde.
Nitaligeuza jangwa liwe mabwawa ya maji,
nayo ardhi iliyokauka kuwa chemchemi za maji.
19 Katika jangwa nitaotesha
mwerezi, mshita, mhadasi na mzeituni.
Nitaweka misunobari, mivinje na misanduku
pamoja huko nyikani,
20 ili watu wapate kuona na kujua,
wapate kufikiri na kuelewa,
kwamba mkono wa Mwenyezi Mungu umetenda hili,
kwamba yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli ndiye alilifanya."

21 Mwenyezi Mungu asema, "Leta shauri lako.
Toa hoja yako," asema Mfalme wa Yakobo.
22 "Leteni sanamu zenu zituambie
ni nini kitakachotokea.
Tuambieni mambo ya zamani yalikuwa nini,
ili tupate kuyatafakari
na kujua matokeo yake ya mwisho.
Au tutangazieni mambo yatakayokuja,
23 tuambieni ni nini kitakachotokea baadaye,
ili tupate kujua kuwa ninyi ni miungu.
Fanyeni jambo lolote zuri au baya,
ili tupate kutishika na kujazwa na hofu.
24 Lakini ninyi ni zaidi ya bure kabisa,
na kazi zenu hazifai kitu kabisa;
yeye awachaguaye ni chukizo sana.

25 “Nimemchochea mtu mmoja kutoka kaskazini,
naye yuaja, mmoja toka mawio ya jua aliitaye Jina langu.
Huwakanyaga watawala kana kwamba ni matope,
kama mfinyanzi akanyagavyo udongo wa kufinyangia.
26 Ni nani aliyenena hili tokea mwanzoni, ili tupate kujua,
au kabla, ili tuweze kusema, ‘Alikuwa mwenye haki’?
Hakuna aliyenena hili,
hakuna aliyetangulia kusema hili,
hakuna yeyote aliyesikia maneno kutoka kwenu.
27 Nilikuwa wa kwanza kumwambia Sayuni,
‘Tazama, wako hapa!’
Nilimpa Yerusalemu mjumbe wa habari njema.
28 Ninatazama, lakini hakuna yeyote:
hakuna yeyote miongoni mwao awezaye kutoa shauri,
hakuna yeyote wa kutoa jibu wakati ninapowauliza.
29 Tazama, wote ni ubatili!
Matendo yao ni bure;
vinyago vyao ni upepo mtupu na machafuko.

# 42

*Mtumishi wa Mwenyezi Mungu*

1 “Huyu hapa mtumishi wangu, ninayemtegemeza,
mteule wangu, ninayependezwa naye;

nitaweka Roho yangu juu yake,
naye ataleta haki kwa mataifa.
2 Hatapaza sauti wala kupiga kelele,
wala hataipaza sauti yake barabarani.
3 Mwanzi uliopondeka hatauvunja,
na utambi unaofuka moshi hatauzima.
Kwa uaminifu ataleta haki,
4 hatazimia roho wala kukata tamaa,
hadi atakaposimamisha haki juu ya dunia.
Visiwa vitaweka tumaini lao katika sheria yake.”

5 Hili ndilo asemalo Mungu, Mwenyezi Mungu,
yeye aliyeziumba mbingu na kuzitanda,
aliyeitandaza dunia na vyote vinavyotoka humo,
awapaye watu wake pumzi,
na uzima kwa wale wanaoenda humo:
6 “Mimi, Mwenyezi Mungu, nimekuita katika haki;
nitakushika mkono wako.
Nitakulinda na kukufanya kuwa agano
kwa ajili ya watu
na nuru kwa Mataifa,
7 kuwafungua macho wale wasioona,
kuwaacha huru kutoka kifungoni wale waliofungwa,
na kuwafungua kutoka gerezani
wale wanaokaa gizani.

8 “Mimi ndimi Mwenyezi Mungu; hilo ndilo Jina langu!
Sitampa mwingine utukufu wangu
wala sanamu sifa zangu.
9 Tazama, mambo ya kwanza yametokea,

nami natangaza mambo mapya;
kabla hayajatokea
nawatangazia habari zake.”

*Wimbo wa kumsifu Mwenyezi Mungu*

10 Mwimbieni Mwenyezi Mungu wimbo mpya,
sifa zake toka miisho ya dunia,
ninyi mshukao chini baharini,
na vyote vilivyomo,
enyi visiwa na wote wanaoishi humo.
11 Jangwa na miji yake na vipaze sauti zao;
makazi anamoishi Kedari na yashangilie.
Watu wa Sela waimbe kwa furaha,
na wapige kelele kutoka vilele vya milima.
12 Wampe Mwenyezi Mungu utukufu,
na kutangaza sifa zake katika visiwa.
13 Mwenyezi Mungu ataenda kama mtu mwenye nguvu,
kama shujaa atachochea shauku yake,
kwa kishindo ataamsha ukelele wa vita,
naye atashinda adui zake.

14 “Kwa muda mrefu nimenyamaza;
nimekaa kimya na kujizuia.
Lakini sasa, kama mwanamke wakati wa kujifungua,
ninapiga kelele, ninatweta na kushusha pumzi.
15 Nitaharibu milima na vilima
na kukausha mimea yako yote;
nitafanya mito kuwa visiwa
na kukausha mabwawa.
16 Nitawaongoza vipofu kwenye njia ambayo hawajaijua,

kwenye mapito wasiyoyazoea nitawaongoza;
nitafanya giza kuwa nuru mbele yao,
na kufanya mahali palipoparuza kuwa laini.
Haya ndio mambo nitakayofanya;
mimi sitawaacha.
17 Lakini wale wanaotumaini sanamu,
wanaoviambia vinyago, 'Ninyi ndio miungu yetu,'
watarudishwa nyuma kwa aibu kubwa.

*Israeli ni kipofu na kiziwi*

18 "Sikieni, enyi viziwi;
tazameni, enyi vipofu, mpate kuona!
19 Ni nani aliye kipofu isipokuwa mtumishi wangu,
na kiziwi kama mjumbe ninayemtuma?
Ni nani aliye kipofu kama yeye aliyejitoa kwangu,
aliye kipofu kama mtumishi wa Mwenyezi Mungu?
20 Mmeona vitu vingi, lakini hamkuzingatia;
masikio yenu yako wazi, lakini hamsikii chochote."
21 Ilimpendeza Mwenyezi Mungu
kwa ajili ya haki yake
kufanya sheria yake kuwa kuu na tukufu.
22 Lakini hili ni taifa lililoibwa na kutekwa nyara,
wote wamenaswa katika mashimo,
au wamefichwa katika magereza.
Wamekuwa nyara,
wala hapana yeyote awaokoaye.
Wamefanywa mateka,
wala hapana yeyote asemaye, "Warudishe."

23 Ni nani miongoni mwenu atakayesikiliza hili,
au atakayezingatia kwa makini katika wakati ujao?
24 Ni nani aliyemtoa Yakobo kuwa mateka,
na Israeli kwa wateka nyara?
Je, hakuwa yeye, Mwenyezi Mungu,
ambaye tumetenda dhambi dhidi yake?
Kwa kuwa hawakufuata njia zake,
hawakutii sheria zake.
25 Hivyo akawamwagia hasira yake inayowaka,
ukali wa vita.
Iliwazunguka kwa miali ya moto,
lakini hata hivyo hawakuelewa;
iliwateketeza, lakini hawakuyatia moyoni.

# 43

*Mwokozi pekee wa Israeli*

1 Lakini sasa hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
yeye aliyekuumba, ee Yakobo,
yeye aliyekuhuluku, ee Israeli:
"Usiogope kwa maana nimekukomboa,
nimekuita wewe kwa jina lako, wewe u wangu.
2 Unapopita kwenye maji makuu,
nitakuwa pamoja nawe,
unapopita katika mito ya maji,
hayatakugharikisha.
Utakapopita katika moto,
hutaungua,
miali ya moto haitakuunguza.
3 Kwa kuwa Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako,

yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli, Mwokozi wako.
Ninaitoa Misri kuwa fidia yako,
Kushi na Seba badala yako.
4 Kwa kuwa wewe ni wa thamani na wa kuheshimiwa machoni pangu,
nami kwa kuwa ninakupenda,
nitatoa watu badala yako
na mataifa badala ya maisha yako.
5 Usiogope, kwa kuwa mimi nipo pamoja nawe,
nitawaleta watoto wako kutoka mashariki,
na kukukusanya kutoka magharibi.
6 Nitaiambia kaskazini, ‘Watoe!’
nayo kusini, ‘Usiwazuie.’
Walete wana wangu kutoka mbali,
na binti zangu kutoka miisho ya dunia:
7 kila mmoja ambaye ameitwa kwa Jina langu,
niliyemuumba kwa utukufu wangu,
niliyemhuluku na kumfanya.”
8 Uwaongoze wale wenye macho lakini hawaoni,
wenye masikio lakini hawasikii.
9 Mataifa yote yanakutanika pamoja,
na makabila yanakusanyika.
Ni nani miongoni mwao aliyetangulia kutuambia haya,
na kututangazia mambo yaliyopita?
Walete mashahidi wao ili kuwathibitisha kuwa walikuwa sahihi,
ili wengine waweze kusikia, waseme, “Ni kweli.”

10 “Ninyi ni mashahidi wangu,” asema Mwenyezi Mungu,
“na mtumishi wangu niliyemchagua,

ili mpate kunijua na kuniamini,
na kutambua kwamba Mimi ndiye.
Kabla yangu hakuna mungu aliyefanyizwa,
wala hatakuwepo mwingine baada yangu.
11 Mimi, naam mimi, ndimi Mwenyezi Mungu,
zaidi yangu hakuna mwokozi.
12 Nimedhihirisha, kuokoa na kutangaza:
Mimi mwenyewe, bali si mungu mgeni kati yenu.
Ninyi ni mashahidi wangu," asema Mwenyezi Mungu,
"kwamba Mimi ndimi Mungu.
13 Naam, tangu siku za kale, Mimi ndiye.
Hakuna hata mmoja awezaye kuokoa
kutoka mkononi wangu.
Mimi ninapotenda,
ni nani awezaye kutangua?"

### *Huruma za Mwenyezi Mungu, na kutoaminika kwa Israeli*

14 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mkombozi wako, yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli:
"Kwa ajili yenu nitatumana Babeli
na kuwaleta Wakaldayo wote kama wakimbizi,
katika meli walizozionea fahari.
15 Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, yeye Aliye Mtakatifu wako,
Muumba wa Israeli, Mfalme wako."

16 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
yeye aliyefanya njia baharini,
mahali pa kupita kwenye maji mengi,

17 aliyeyakokota magari ya vita na farasi,
jeshi pamoja na askari wa msaada,
nao wakalala huko, wala hawatainuka tena kamwe,
wakakomeshwa, na wakazimika kama utambi:
18 "Msiyakumbuke mambo yaliyopita,
wala msiyatafakari mambo ya zamani.
19 Tazama, nitafanya jambo jipya!
Sasa litachipuka, je, hamtalitambua?
Nitafanya njia jangwani
na vijito vya maji katika nchi kame.
20 Wanyama pori wataniheshimu,
mbweha na bundi,
kwa sababu ninawapatia maji jangwani,
na vijito katika nchi kame,
ili kuwapa watu wangu maji, wale niliowachagua,
21 watu wale niliowaumba kwa ajili yangu,
ili wapate kutangaza sifa zangu.

22 "Hata hivyo hukuniita mimi, ee Yakobo,
hujajitaabisha kwa ajili yangu, ee Israeli.
23 Hujaniletea kondoo kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa,
wala kuniheshimu kwa dhabihu zako.
Sikukulemea kwa sadaka za nafaka
wala kukuchosha kwa kuhitaji uvumba.
24 Hukuninunulia uvumba wowote wenye manukato,
wala hukunipa kwa ukarimu
mafuta ya wanyama wa dhabihu zako.
Lakini umenilemea kwa dhambi zako,
na kunitaabisha kwa makosa yako.

25 “Mimi, naam mimi, ndimi nizifutaye dhambi zako,
kwa ajili yangu mwenyewe,
wala sizikumbuki dhambi zako tena.
26 Tafakari mambo yaliyopita,
njoo na tuhojiane,
jitetee uweze kupewa haki yako.
27 Baba yako wa kwanza alitenda dhambi,
wasemaji wako wameasi dhidi yangu.
28 Kwa hiyo nitawaaibisha wakuu wa Hekalu lako,
nami nitamtoa Yakobo aangamizwe,
na Israeli adhihakiwe.

# 44

## *Israeli aliyechaguliwa*

1 “Lakini sasa sikiliza, ee Yakobo, mtumishi wangu,
Israeli, niliyemchagua.
2 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
yeye aliyekuhuluku, aliyekuumba tumboni,
yeye atakayekusaidia:
Usiogope, ee Yakobo, mtumishi wangu,
Yeshuruni*, niliyekuchagua.
3 Kwa maana nitamimina maji juu ya nchi yenye kiu,
na vijito vya maji juu ya ardhi iliyokauka;
nitamimina Roho wangu Mtakatifu juu ya watoto wako,
nayo baraka yangu juu ya wazao wako.

---

* **44:2** maana yake *Yeye aliye mnyofu*, yaani Israeli

4 Nao watachipua kama nyasi katika shamba la majani,
kama mierezi kando ya vijito vya maji yanayotiririka.
5 Mmoja atasema, 'Mimi ni wa Mwenyezi Mungu';
mwingine atajiita kwa jina la Yakobo;
vilevile mwingine ataandika juu ya mkono wake,
'Wa Mwenyezi Mungu,'
na kujiita kwa jina la Israeli.

### *Ni Mwenyezi Mungu, siyo sanamu*

6 "Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mfalme wa Israeli na Mkombozi,
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni:
Mimi ni wa kwanza na Mimi ni wa mwisho;
zaidi yangu hakuna Mungu.
7 Ni nani basi aliye kama mimi? Yeye na atangaze.
Yeye atangaze na kuweka mbele yangu
ni kitu gani kilichotokea tangu nilipoumba watu wangu wa kale,
tena ni nini kitakachotokea:
naam, yeye na atoe unabii ni nini kitakachokuja.
8 Msitetemeke, msiogope.
Je, sikutangaza hili, na kutoa unabii tangu zamani?
Ninyi ni mashahidi wangu.
Je, yuko Mungu zaidi yangu mimi?
Hasha, hakuna Mwamba mwingine;
mimi simjui mwingine."

9 Wote wachongao sanamu ni ubatili,

navyo vitu wanavyovithamini havifai kitu.
Wale ambao wanazitetea ni vipofu,
ni wajinga, nao waaibika.
10 Ni nani atengenezaye mungu na kusubu sanamu,
ambayo haiwezi kumfaidia kitu chochote?
11 Yeye pamoja na wenziwe wa aina yake wataaibishwa,
mafundi wao si kitu ila ni wanadamu tu.
Wote wakusanyike pamoja na kuwa na msimamo wao,
watashushwa chini kwa hofu na kwa fedheha.

12 Muhunzi huchukua kifaa
na kukifanyia kazi kwenye makaa ya moto,
hutengeneza sanamu kwa nyundo,
huifanyiza kwa nguvu za mkono wake.
Huona njaa na kupoteza nguvu zake,
asipokunywa maji huzimia.
13 Seremala hupima kwa kutumia kamba,
na huuchora mstari kwa kalamu;
huchonga kwa patasi
na kutia alama kwa bikari.
Huitengeneza katika umbo la binadamu,
umbo la binadamu katika utukufu wake wote,
ili iweze kukaa katika mahali pake pa ibada za sanamu.
14 Hukata miti ya mierezi,
huchukua mtiriza au mwaloni.
Huuacha ukue miongoni mwa miti ya msituni,
au hupanda msunobari, nayo mvua huufanya ukue.
15 Ni kuni ya binadamu:

yeye huchukua baadhi yake na kuota moto,
huwasha moto na kuoka mkate.
Lakini pia huutumia kumtengeneza mungu na akamwabudu,
huitengeneza sanamu na kuisujudia.
16 Sehemu ya kuni huziweka motoni,
akapikia chakula chake,
hubanika nyama na kula hadi ashibe.
Huota moto na kusema,
“Aha! Ninahisi joto, ninaona moto.”
17 Mabaki yake hutengeneza mungu, sanamu yake;
yeye huisujudia na kuiabudu.
Huiomba na kusema,
“Niokoe; wewe ni mungu wangu.”
18 Hawajui chochote, hawaelewi chochote,
macho yao yamefungwa hata hawawezi kuona,
akili zao zimefungwa hata hawawezi kufahamu.
19 Hakuna anayefikiri,
hakuna mwenye maarifa wala ufahamu wa kusema,
“Sehemu yake nilitumia kwa kuni;
hata pia nilioka mkate juu ya makaa yake,
nikabanika nyama na kuila.
Je, nifanye machukizo kwa kile kilichobaki?
Je, nisujudie gogo la mti?”
20 Hujilisha kwa majivu, moyo uliodanganyika humpotosha;
hawezi kujiokoa mwenyewe, au kusema,
“Je, kitu hiki kilicho mkononi wangu wa kuume
si ni uongo?”

21 “Ee Yakobo, kumbuka mambo haya,
ee Israeli, kwa kuwa wewe ni mtumishi wangu.
Nimekuumba wewe, wewe ni mtumishi wangu.
Ee Israeli, sitakusahau.
22 Nimeyafuta makosa yako kama wingu,
dhambi zako kama ukungu wa asubuhi.
Nirudie mimi,
kwa kuwa nimekukomboa wewe.”

23 Enyi mbingu, imbeni kwa furaha,
kwa maana Mwenyezi Mungu amefanya jambo hili.
Ee vilindi vya dunia, piga kelele.
Enyi milima, pazeni sauti kwa nyimbo,
enyi misitu na miti yenu yote,
kwa maana Mwenyezi Mungu amemkomboa Yakobo,
ameuonesha utukufu wake katika Israeli.

### *Yerusalemu itakaliwa*

24 “Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mkombozi wako, aliyekuumba tumboni:

“Mimi ni Mwenyezi Mungu,
niliyeumba vitu vyote,
niliyezitanda mbingu peke yangu,
niliyeitandaza nchi mwenyewe.

25 “Mimi huzipinga ishara za manabii wa uongo,
na kuwatia upumbavu waaguzi,
niyapinduaye maarifa ya wenye hekima,
na kuyafanya kuwa upuzi.

26 Mimi ndimi niyathibitishaye maneno ya watumishi wake,
na kutimiza utabiri wa wajumbe wake.

"Mimi ndiye niiambiaye Yerusalemu, 'Itakaliwa na watu,'
niiambiaye miji ya Yuda kuwa, 'Itajengwa,'
na kuhusu magofu yake, 'Mimi nitayatengeneza,'
27 niiambiaye kilindi cha maji, 'Kauka,
nami nitakausha vijito vyako,'
28 nisemaye kuhusu Koreshi, 'Yeye ni mchungaji wangu,
naye atatimiza yote yanipendezayo;
atauambia Yerusalemu, "Ukajengwe tena,"
na kuhusu Hekalu, "Misingi yake na iwekwe." '

# 45

### *Koreshi ni chombo cha Mwenyezi Mungu*

1 "Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu kwa mpakwa mafuta wake,
Koreshi, ambaye nimemshika mkono wake wa kuume
kutiisha mataifa mbele yake
na kuwavua wafalme silaha zao,
kufungua milango mbele yake
ili malango yasije yakafungwa:
2 Nitaenda mbele yako
na kusawazisha milima;
nitavunjavunja malango ya shaba
na kukatakata mapingo ya chuma.
3 Nitakupa hazina za gizani,

mali iliyofichwa mahali pa siri,
ili upate kujua kwamba Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
Mungu wa Israeli, akuitaye kwa jina lako.
4 Kwa ajili ya Yakobo mtumishi wangu,
Israeli niliyemchagua,
nimekuita wewe kwa jina lako,
na kukupa jina la heshima,
ingawa wewe hunitambui.
5 Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, wala hakuna mwingine,
zaidi yangu hakuna Mungu.
Nitakutia nguvu,
ingawa wewe hujanitambua,
6 ili kutoka mawio ya jua
hadi machweo yake,
watu wapate kujua kwamba hakuna Mungu mwingine ila Mimi.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu wala hakuna mwingine.
7 Mimi ninaumba nuru na kuhuluku giza,
ninaleta mafanikio na kusababisha maafa.
Mimi, Mwenyezi Mungu, huyatenda haya yote.

8 “Enyi mbingu juu, nyesheni haki,
mawingu na yaidondoshe.
Dunia na ifunguke sana,
wokovu na uchipuke,
haki na ikue pamoja nao.
Mimi, Mwenyezi Mungu, ndiye niliyeiumba.

9 “Ole wake yeye ashindanaye na Muumba wake,

yeye ambaye ni kigae tu kati ya vigae juu ya ardhi.
Je, udongo wa kufinyangia humwambia mfinyanzi,
'Unatengeneza nini wewe?'
Je, kazi yako husema,
'Hana mikono'?
10 Ole wake amwambiaye baba yake,
'Umezaa nini?'
Au kumwambia mama yake,
'Umezaa kitu gani?'

11 "Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli na Muumba wake:
Kuhusu mambo yatakayokuja,
je, unaniuliza habari za watoto wangu,
au kunipa amri kuhusu kazi za mikono yangu?
12 Mimi ndiye niliyeumba dunia
na kumuumba mwanadamu juu yake.
Mikono yangu mwenyewe ndiyo iliyozitanda mbingu,
nikayapanga majeshi yake yote ya angani.
13 Mimi nitamwinua Koreshi katika haki yangu:
nitazinyoosha njia zake zote.
Yeye atajenga mji wangu upya,
na kuwaweka huru watu wangu walio uhamishoni,
lakini si kwa kulipiwa fedha wala kupewa zawadi,
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni."

14 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Mazao ya Misri na bidhaa za Kushi,
nao wale Waseba warefu,
watakujia na kuwa wako,
watakujia wakijikokota nyuma yako,
watakujia wamefungwa minyororo.
Watasujudu mbele yako,
wakikusihi na kusema,
‘Hakika Mungu yu pamoja nawe,
wala hakuna mwingine;
hakuna Mungu mwingine.’ ”

15 Hakika wewe u Mungu unayejificha,
Ee Mungu na Mwokozi wa Israeli.
16 Wote watengenezao sanamu wataaibika na kutahayarika;
wataenda kutahayarika pamoja.
17 Lakini Israeli ataokolewa na Mwenyezi Mungu
kwa wokovu wa milele;
kamwe hutaaibika wala kutatahayarika,
milele yote.

18 Kwa kuwa hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
yeye aliyeumba mbingu,
ndiye Mungu;
yeye aliyeifanya dunia na kuiumba,
yeye ndiye aliiwekea misingi imara,
hakuiumba ili iwe tupu,
bali aliiumba ikaliwe na viumbe vyake.
Anasema:
“Mimi ndimi Mwenyezi Mungu,
wala hakuna mwingine.

19 Sijasema sirini,
kutoka mahali fulani katika nchi ya giza;
sijawaambia wazao wa Yakobo,
'Nitafuteni bure.'
Mimi, Mwenyezi Mungu, nasema kweli;
ninatangaza lililo sahihi.

20 "Kusanyikeni pamoja mje,
enyi wakimbizi kutoka mataifa.
Wale wabebao sanamu za mti ni watu wasio na akili,
wale waombao miungu isiyoweza kuokoa.
21 Tangazeni litakalokuwepo, lisemeni hilo;
wao na wafanye shauri pamoja.
Ni nani aliyetangulia kusema hili tangu zamani,
aliyelitangaza tangu zamani za kale?
Je, haikuwa Mimi, Mwenyezi Mungu?
Wala hapana Mungu mwingine
zaidi yangu mimi,
Mungu mwenye haki na Mwokozi;
hapana mwingine ila mimi.

22 "Nigeukieni mimi, nanyi mkaokolewe,
enyi miisho yote ya dunia;
kwa maana mimi ndimi Mungu,
wala hapana mwingine.
23 Nimeapa kwa nafsi yangu,
kinywa changu kimenena katika uadilifu wote
neno ambalo halitatanguka:
Kila goti litapigwa mbele zangu,
kwangu mimi kila ulimi utaapa.
24 Watasema kunihusu,

‘Katika Mwenyezi Mungu peke yake
ndiko kuna haki na nguvu.’ ”
Wote ambao wamemkasirikia Mungu
watamjia yeye, nao watatahayarika.
25 Lakini katika Mwenyezi Mungu wazao wote wa Israeli
wataonekana wenye haki na watashangilia.

# 46

*Miungu ya Babeli*

1 Beli anasujudu, Nebo anainama;
sanamu zao zabebwa na wanyama wa mizigo.
Vinyago hivi mnavyobeba kila mahali ni mzigo wa kulemea,
mzigo kwa waliochoka.
2 Vinyago pamoja na wale wanaovibeba wanainama chini;
hiyo miungu haiwezi kuwaokoa watu,
wote wanaenda utumwani pamoja.

3 “Nisikilizeni mimi, ee nyumba ya Yakobo,
ninyi nyote mliobaki wa nyumba ya Israeli,
ninyi ambao nimewategemeza tangu mlipotungwa mimba,
nami nimewabeba tangu kuzaliwa kwenu.
4 Hata wakati wa uzee wenu na mvi, Mimi ndiye,
Mimi ndiye nitakayewasaidia ninyi.
Nimewahuluku, nami nitawabeba,
nitawahudumia ninyi na kuwaokoa.

5 “Mtanilinganisha na nani,
au mtanihesabu kuwa sawa na nani?

Ni nani mtakayenifananisha naye
ili tuweze kulinganishwa?
6 Wengine humwaga dhahabu kutoka mifuko yao,
na kupima fedha kwenye mizani;
huajiri mfua dhahabu kutengeneza mungu,
kisha huisujudia na kuiabudu.
7 Huiinua mabegani na kuichukua;
huiweka mahali pake, papo hapo ndipo isimamapo.
Wala haiwezi kusogea kutoka mahali pale.
Ingawa mtu huililia, haimjibu;
haiwezi kumwokoa kwenye taabu zake.

8 “Kumbukeni hili, litieni akilini,
liwekeni moyoni, enyi waasi.
9 Kumbukeni mambo yaliyopita, yale ya zamani za kale;
mimi ndimi Mungu, wala hakuna mwingine;
mimi ndimi Mungu,
wala hakuna mwingine aliye kama mimi.
10 Ni mimi nitangazaye mwisho tangu mwanzo,
naam, tangu zamani za kale,
mambo ambayo hayajatendeka.
Ninasema: Kusudi langu ndilo litakalosimama,
nami nitatenda mapenzi yangu yote.
11 Kutoka mashariki ninaita ndege awindaye;
kutoka nchi ya mbali,
mtu atakayetimiza kusudi langu.
Lile ambalo nimelisema, ndilo nitakalolitimiza;
lile nililolipanga, ndilo nitakalolitenda.
12 Nisikilizeni, ninyi wenye mioyo migumu,
ninyi mlio mbali na haki.

13 Ninaleta haki yangu karibu,
haiko mbali;
wala wokovu wangu hautachelewa.
Nitawapa Sayuni wokovu,
Israeli utukufu wangu.

# 47

### *Anguko la Babeli*

1 “Shuka uketi mavumbini,
ee Bikira Binti Babeli;
keti chini pasipo na kiti cha utawala,
ee Binti wa Wakaldayo.
Hutaitwa tena mwororo wala wa kupendeza.
2 Chukua mawe ya kusagia, usage unga,
vua shela yako.
Pandisha mavazi yako, ondoa viatu vyako,
vuka vijito kwa shida.
3 Uchi wako utafunuliwa
na aibu yako itaonekana.
Nitalipa kisasi;
sitamhurumia hata mmoja.”

4 Mkombozi wetu: Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ndilo jina lake;
ndiye yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli.

5 “Keti kimya, ingia gizani,
Binti wa Wakaldayo,
hutaitwa tena malkia wa falme.
6 Niliwakasirikia watu wangu
na kuaibisha urithi wangu;
niliwatia mikononi mwako,
nawe hukuwaonea huruma.

Hata juu ya wazee
uliweka nira nzito sana.
7 Ukasema, ‘Nitaendelea
kuwa malkia milele!’
Lakini hukutafakari mambo haya
wala hukuwaza juu ya kile kingeweza kutokea.

8 “Sasa basi, sikiliza, ewe kiumbe mpenda anasa,
ukaaye mahali pako pa salama,
na kujiambia mwenyewe,
‘Mimi ndiye, wala hakuna mwingine zaidi yangu.
Kamwe sitakuwa mjane,
wala sitafiwa na watoto.’
9 Haya mawili yatakupata, kufumba na kufumbua,
katika siku moja:
kufiwa na watoto, na ujane.
Yote yatakupata kwa kipimo kikamilifu,
ijapokuwa uchawi wako ni mwingi,
na uaguzi wako ni mwingi.
10 Umeutegemea uovu wako,
nawe umesema, ‘Hakuna yeyote anionaye.’
Hekima yako na maarifa yako vinakupoteza
unapojiambia mwenyewe,
‘Mimi ndiye, wala hakuna mwingine zaidi yangu.’
11 Maafa yatakujia,
nawe hutaweza kuyaondoa kwa uaguzi.
Janga litakuangukia,
wala hutaweza kulikinga kwa fidia;
msiba mkuu usioweza kuutabiri
utakujia ghafula.

12 “Endelea basi na uaguzi wako,
na wingi wa uchawi wako,
ambao umeutumikia tangu utoto wako.
Labda utafanikiwa,
labda unaweza ukasababisha hofu kuu.
13 Ushauri wote uliopokea umekuchosha bure!
Wanajimu wako na waje mbele,
wale watazama nyota watabiriao mwezi baada ya mwezi,
wao na wawaokoe na lile linalokuja juu yenu.
14 Hakika wako kama mabua makavu;
moto utawateketeza.
Hawawezi hata kujiokoa wao wenyewe
kutokana na nguvu za mwali wa moto.
Hapa hakuna makaa ya kumtia mtu yeyote joto;
hapa hakuna moto wa kuota.
15 Hayo ndiyo yote wanayoweza kuwatendea ninyi,
hawa ambao umetaabika nao
na kufanya nao biashara tangu utoto.
Kila mmoja atatoroka;
hakuna yeyote awezaye kukuokoa.

# 48

*Israeli mkaidi*

1 “Sikilizeni hili, ee nyumba ya Yakobo,
ninyi mnaoitwa kwa jina la Israeli,
na mnaotoka katika ukoo wa Yuda,
ninyi mnaoapa kwa jina la Mwenyezi Mungu,
mnaomwomba Mungu wa Israeli,
lakini si katika kweli au kwa haki;
2 ninyi mnaojiita raia wa mji mtakatifu,

na kumtegemea Mungu wa Israeli,
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ndilo jina lake:
3 Nilitoa unabii mambo ya kwanza tangu zamani,
kinywa changu kiliyatangaza na kuyafanya yajulikane;
kisha ghafula nikayatenda, nayo yakatokea.
4 Kwa kuwa nalijua jinsi ulivyokuwa mkaidi;
mishipa ya shingo yako ilikuwa chuma,
paji la uso wako lilikuwa shaba.
5 Kwa hiyo nilikuambia mambo haya tangu zamani,
kabla hayajatokea nilikutangazia
ili usije ukasema,
'Sanamu zangu zilifanya hayo;
sanamu yangu ya mti, na mungu wangu wa chuma aliyaamuru.'
6 Umesikia mambo haya; yaangalie hayo yote.
Je, hutayakubali?

"Kuanzia sasa na kuendelea nitakueleza mambo mapya,
juu ya mambo yaliyofichika usiyoyajua.
7 Yameumbwa sasa, wala si tangu zamani;
hukupata kuyasikia kabla ya siku ya leo.
Hivyo huwezi kusema,
'Naam, niliyajua hayo.'
8 Hujayasikia wala kuyaelewa,
tangu zamani sikio lako halikufunguka.
Ninafahamu vyema jinsi ulivyo mdanganyifu,
uliitwa mwasi tangu kuzaliwa kwako.
9 Kwa ajili ya Jina langu mwenyewe
ninaichelewesha ghadhabu yangu,

kwa ajili ya sifa zangu nimeizuia isikupate,
ili nisije nikakukatilia mbali.
10 Tazama, nimekusafisha, ingawa si kama fedha,
nimekujaribu katika tanuru la mateso.
11 Kwa ajili yangu mwenyewe,
kwa ajili yangu mwenyewe, nafanya hili.
Jinsi gani niliache Jina langu lichafuliwe?
Sitautoa utukufu wangu kwa mwingine.

*Israeli anawekwa huru*

12 “Ee Yakobo, nisikilize mimi,
Israeli, ambaye nimekuita:
Mimi ndiye;
mimi ndimi mwanzo na mwisho.
13 Mkono wangu mwenyewe uliweka misingi ya dunia,
nao mkono wangu wa kuume umezitanda mbingu;
niziitapo, zote husimama pamoja.

14 “Kusanyikeni, ninyi nyote, msikilize:
Ni ipi miongoni mwa hizo sanamu
ambayo imetabiri vitu hivi?
Watu wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa na kuungana
watatimiza kusudi lake dhidi ya Babeli;
mkono wa Mungu utakuwa dhidi ya Wakaldayo.
15 Mimi, naam, Mimi, nimenena;
naam, nimemwita yeye.
Nitamleta,
naye atafanikiwa katika lile nililomtuma.
16 “Nikaribieni na msikilize hili:
“Tangu tangazo la kwanza sikusema kwa siri;

wakati litokeapo, nitakuwako hapo.”

Sasa Bwana Mungu Mwenyezi amenituma,
kwa Roho wake Mtakatifu.

17 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mkombozi wako, yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli:
“Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
nikufundishaye ili upate faida,
nikuongozaye katika njia ikupasayo kuiendea.
18 Laiti ungesikiliza kwa makini maagizo yangu,
amani yako ingekuwa kama mto,
haki yako kama mawimbi ya bahari.
19 Wazao wako wangekuwa kama mchanga,
watoto wako kama chembe zake zisizohesabika;
kamwe jina lao lisingefutiliwa mbali,
wala kuangamizwa kutoka mbele zangu.”

20 Tokeni huko Babeli,
kimbieni kutoka kwa Wakaldayo!
Tangazeni hili kwa kelele za shangwe
na kulihubiri.
Lipelekeni hadi miisho ya dunia;
semeni, “Mwenyezi Mungu amemkomboa
mtumishi wake Yakobo.”
21 Hawakuona kiu alipowaongoza kupita jangwani;
alifanya maji yatiririke kutoka mwamba kwa ajili yao;
akapasua mwamba
na maji yakatoka kwa nguvu.

22 “Hakuna amani kwa waovu,” asema Mwenyezi Mungu.

# 49

### *Mtumishi wa Mwenyezi Mungu*

1 Nisikilizeni, enyi visiwa, sikieni hili,
ninyi mataifa mlio mbali:
Kabla sijazaliwa, Mwenyezi Mungu aliniita,
tangu kuzaliwa kwangu, amelitaja jina langu.
2 Akafanya kinywa changu kuwa kama upanga ulionolewa,
katika uvuli wa mkono wake akanificha;
akanifanya kuwa mshale uliosuguliwa,
na kunificha katika podo lake.
3 Akaniambia, “Wewe u mtumishi wangu,
Israeli, ambaye ndani yake
nitaonesha utukufu wangu.”
4 Lakini nilisema, “Nimetumika bure,
nimetumia nguvu zangu bure bila faida.
Hata hivyo linalonistahili liko mkononi mwa Mwenyezi Mungu,
nao ujira wangu uko kwa Mungu wangu.”

5 Sasa Mwenyezi Mungu asema:
yeye aliyeniumba tumboni kuwa mtumishi wake,
kumrudisha tena Yakobo kwake
na kumkusanyia Israeli,
kwa maana nimepata heshima machoni pa Mwenyezi Mungu,
naye Mungu wangu amekuwa nguvu yangu;
6 yeye asema:

“Je, ni jambo dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu
ili kurejesha makabila ya Yakobo,
na kuwarudisha wale Waisraeli niliowahifadhi?
Pia nitakufanya uwe nuru kwa ajili ya watu wa Mataifa,
ili upate kuleta wokovu wangu hata miisho ya dunia.”

7 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
yeye Mkombozi na Aliye Mtakatifu wa Israeli,
kwake yeye aliyedharauliwa na kuchukiwa na taifa,
kwa mtumishi wa watawala:
“Wafalme watakuona na kusimama,
wakuu wataona na kuanguka kifudifudi,
kwa sababu ya Mwenyezi Mungu, aliye mwaminifu,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli, aliyekuchagua wewe.”

### *Kurejeshwa kwa Israeli*

8 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Wakati wangu uliokubalika nitakujibu,
nami katika siku ya wokovu nitakusaidia;
nitakuhifadhi, nami nitakufanya kuwa agano
kwa ajili ya watu,
ili kurudisha nchi
na kugawanyia urithi tena wale waliokuwa ukiwa,
9 kuwaambia mateka, ‘Tokeni nje,’
nao wale walio gizani, ‘Kuweni huru!’

"Watajilisha kando ya barabara
na kupata malisho yao juu ya kila kilima kilicho kitupu.
10 Hawataona njaa wala kuona kiu,
wala hari ya jangwani au jua halitawapiga.
Yeye mwenye huruma juu yao atawaonesha njia,
na kuwaongoza kando ya chemchemi za maji.
11 Nitaifanya milima yangu yote kuwa barabara,
na njia kuu zangu zitainuliwa.
12 Tazama, watakuja kutoka mbali:
wengine kutoka kaskazini, wengine kutoka magharibi,
wengine kutoka nchi ya Sinimu*."

13 Pigeni kelele kwa furaha, enyi mbingu;
furahi, ee dunia;
pazeni sauti kwa kuimba, enyi milima!
Kwa maana Mwenyezi Mungu anawafariji watu wake,
naye atakuwa na huruma kwa watu wake walioumizwa.

14 Lakini Sayuni alisema, "Mwenyezi Mungu ameniacha,
Bwana amenisahau."

15 "Je, mama aweza kumsahau mtoto
aliye matitini mwake akinyonya,
wala asiwe na huruma
juu ya mtoto aliyemzaa?
Ingawa anaweza kusahau,

* **49:12** au *Aswani*

mimi sitakusahau wewe!
16 Tazama, nimekuchora kama muhuri
katika vitanga vya mikono yangu,
kuta zako zi mbele yangu daima.
17 Wana wako wanaharakisha kurudi,
nao wale waliokuteka wanaondoka kwako.
18 Inua macho yako ukatazame pande zote:
wana wako wote wanakusanyika na kukujia.
Kwa hakika kama vile niishivyo,
utawavaa wote kama mapambo,
na kujifunga nao kama bibi arusi,"
asema Mwenyezi Mungu.

19 "Ingawa uliangamizwa na kufanywa ukiwa,
na nchi yako ikaharibiwa,
sasa nafasi itakuwa finyu kwa ajili ya watu wako,
nao wale waliokuangamiza watakuwa mbali sana.
20 Watoto waliozaliwa wakati wa msiba wako
bado watakuambia,
'Mahali hapa ni finyu sana kwetu,
tupe eneo kubwa zaidi la kuishi.'
21 Ndipo utasema moyoni mwako,
'Ni nani aliyenizalia hawa?
Nilikuwa nimefiwa, tena tasa;
nilikuwa nimehamishwa na kukataliwa.
Ni nani aliyewalea hawa?
Niliachwa peke yangu,
lakini hawa wametoka wapi?' "
22 Hili ndilo asemalo Bwana Mungu Mwenyezi:
"Tazama, nitawaashiria watu wa Mataifa,
nitainua bendera yangu kwa mataifa;
watawaleta wana wako mikononi yao,

na kuwabeba binti zenu juu ya mabega yao.
23 Wafalme watakuwa baba zenu wa kuwalea,
na malkia wao watakuwa mama zenu wa kuwalea.
Watasujudu mbele yako nyuso zao zikigusa chini;
wataramba mavumbi yaliyo miguuni mwako.
Ndipo utajua ya kuwa Mimi ndimi Mwenyezi Mungu;
wale wanaonitumaini mimi hawataaibika."

24 Je, nyara zaweza kuchukuliwa kutoka kwa mashujaa wa vita,
au mateka kuokolewa kutoka kwa watu wakali?
25 Lakini hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
"Naam, mateka watachukuliwa kutoka kwa mashujaa,
na nyara zitapokonywa kutoka kwa watu wakali.
Nitashindana na wale wanaoshindana nawe,
nami nitawaokoa watoto wako.
26 Nitawafanya wanaokudhulumu wale nyama yao wenyewe;
watalewa kwa damu yao wenyewe,
kama vile kwa mvinyo.
Ndipo wanadamu wote watajua
ya kuwa Mimi, Mwenyezi Mungu, ni Mwokozi wako,
Mkombozi wako, niliye Mwenye Nguvu wa Yakobo."

# 50

*Dhambi ya Israeli na utii wa mtumishi*

1 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Iko wapi hati ya talaka ya mama yako
ambayo kwayo niliachana naye?
Au nimewauza ninyi kwa nani
miongoni mwa watu wanaonidai?
Kwa ajili ya dhambi zenu mliuzwa,
kwa sababu ya makosa, mama yenu aliachwa.
2 Nilipokuja, kwa nini hapakuwa hata mtu mmoja?
Nilipoita, kwa nini hapakuwa hata mtu mmoja wa kujibu?
Je, mkono wangu ni mfupi mno hata nisiweze kuwakomboa?
Je, mimi sina nguvu za kukuokoa?
Kwa kukemea tu naikausha bahari,
naigeuza mito ya maji kuwa jangwa;
samaki wake wanaoza kwa kukosa maji
na kufa kwa ajili ya kiu.
3 Ninalivika anga weusi na kufanya gunia
kuwa kifuniko chake.”

4 Bwana Mungu Mwenyezi amenipa ulimi uliofundishwa,
ili kujua neno limtegemezalo aliyechoka.
Huniamsha asubuhi kwa asubuhi,
huamsha sikio langu lisikie kama mtu afundishwaye.
5 Bwana Mungu Mwenyezi amezibua masikio yangu,
nami sikuwa mwasi,
wala sikurudi nyuma.
6 Niliwapa mgongo wangu wale wanipigao,

mashavu yangu wale wang'oao ndevu zangu;
sikuuficha uso wangu kutokana na fedheha
na kutemewa mate.
7 Kwa sababu Bwana Mungu Mwenyezi ananisaidia,
sitatahayarika.
Kwa hiyo nimekaza uso wangu kama gumegume,
nami ninajua sitaaibika.
8 Yeye anipatiaye haki yangu yu karibu.
Ni nani basi atakayeleta mashtaka dhidi yangu?
Tukabiliane uso kwa uso!
Mshtaki wangu ni nani?
Ni nani aliye mshtaki wangu?
9 Ni Bwana Mungu Mwenyezi anisaidiaye mimi.
Ni nani huyo atakayenihukumu?
Wote watachakaa kama vazi,
nondo watawala wawamalize.

10 Ni nani miongoni mwenu amchaye Mwenyezi Mungu,
na kulitii neno la mtumishi wake?
Yeye atembeaye gizani,
yeye asiye na nuru,
na alitumainie jina la Mwenyezi Mungu,
na amtegemee Mungu wake.
11 Lakini sasa, ninyi nyote mnaowasha mioto,
na kupeana mienge iwakayo ninyi kwa ninyi,
nendeni, tembeeni katika nuru ya moto wenu
na ya mienge mliyoiwasha.
Hili ndilo mtakalolipokea kutoka mkononi mwangu:
Mtalala chini kwa mateso makali.

# 51

## *Wokovu wa milele kwa Sayuni*

1 “Nisikilizeni, ninyi mnaofuatia haki
na mnaomtafuta Mwenyezi Mungu:
Tazameni mwamba ambako mlichongwa,
na mahali pa kuvunjia mawe ambako mlichimbwa;
2 mwangalieni Ibrahimu, baba yenu,
na Sara, ambaye aliwazaa.
Wakati nilimwita alikuwa mmoja tu,
nami nikambariki na kumfanya kuwa wengi.
3 Hakika Mwenyezi Mungu ataifariji Sayuni,
naye atayaangalia kwa huruma magofu yake yote;
atayafanya majangwa yake yawe kama Edeni,
nazo sehemu zake zisizolimika ziwe kama bustani ya Mwenyezi Mungu.
Shangwe na furaha zitakuwa ndani yake,
shukrani na sauti za kuimba.

4 “Nisikilizeni, watu wangu;
nisikieni, taifa langu:
Torati itatoka kwangu;
haki yangu itakuwa nuru kwa mataifa.
5 Haki yangu inakaribia mbio,
wokovu wangu unakuja,
nao mkono wangu utaleta hukumu kwa mataifa.
Visiwa vitanitegemea
na kungojea mkono wangu kwa matumaini.
6 Inueni macho yenu mbinguni,
mkaitazame dunia chini;
mbingu zitatoweka kama moshi,

dunia itachakaa kama vazi,
na wakazi wake kufa kama inzi.
Bali wokovu wangu utadumu milele,
haki yangu haitakoma kamwe.

7 “Nisikieni, ninyi mnaojua lililo sawa,
ninyi watu ambao mna sheria yangu mioyoni mwenu:
Msiogope mashutumu ya wanadamu
wala msitiwe hofu na matukano yao.
8 Kwa maana nondo atawala kama vazi,
nao funza atawatafuna kama sufu.
Lakini haki yangu itadumu milele,
wokovu wangu kwa vizazi vyote.”

9 Amka, Amka! Jivike nguvu,
ewe mkono wa Mwenyezi Mungu,
Amka, kama siku zilizopita,
kama vile vizazi vya zamani.
Si ni wewe uliyemkata Rahabu vipande vipande,
uliyemchoma huyo mnyama mkubwa?
10 Si ni wewe uliyekausha bahari,
maji ya kilindi kikuu,
uliyefanya barabara katika vilindi vya bahari
ili waliokombolewa wapate kuvuka?
11 Wale waliolipiwa fidia na Mwenyezi Mungu watarudi.
Wataingia Sayuni wakiimba;
furaha ya milele itakuwa taji juu ya vichwa vyao.
Furaha na shangwe zitawapata,
huzuni na kulia kwa uchungu kutatoweka.

12 “Mimi, naam mimi,

ndimi niwafarijie ninyi.
Ninyi ni nani hata kuwaogopa
wanadamu wanaokufa,
wanadamu ambao ni majani tu,
13 kwamba mnamsahau Mwenyezi Mungu Muumba wenu,
aliyezitanda mbingu
na kuiweka misingi ya dunia,
kwamba mnaishi katika hofu siku zote
kwa sababu ya ghadhabu ya mdhalimu,
ambaye nia yake ni kuangamiza?
Iko wapi basi ghadhabu ya mdhalimu?
14 Wafungwa waliojikunyata kwa hofu
watawekwa huru karibuni;
hawatafia kwenye gereza lao,
wala hawatakosa chakula.
15 Kwa maana Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
ambaye huisukasuka bahari ili mawimbi yake yangurume:
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ndilo jina lake.
16 Nimeweka maneno yangu kinywani mwako
na kukufunika kwa uvuli wa mkono wangu:
Mimi niliyeweka mbingu mahali pake,
niliyeweka misingi ya dunia,
niwaambiaye Sayuni,
'Ninyi ni watu wangu.' "

### *Kikombe cha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu*

17 Amka, amka!
Simama, ee Yerusalemu,
wewe uliyekunywa kutoka mkono wa Mwenyezi Mungu

kikombe cha ghadhabu yake,
wewe uliyekunywa hata machujo yake,
kikombe kile cha kunywea
kiwafanyacho watu kuyumbayumba.
18 Kati ya wana wote aliowazaa
hapakuwa na hata mmoja wa kumwongoza;
kati ya wana wote aliowalea
hapakuwa hata mmoja wa kumshika mkono.
19 Majanga haya mawili yamekuja juu yako:
ni nani awezaye kukufariji?
Maangamizi, uharibifu, njaa na upanga:
ni nani awezaye kukutuliza?
20 Wana wako wamezimia,
wamelala kwenye mwanzo wa kila barabara,
kama swala aliyenaswa kwenye wavu.
Wamejazwa na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu
na makaripio ya Mungu wako.

21 Kwa hiyo sikiliza hili, wewe uliyeteswa,
uliyelewa, lakini si kwa mvinyo.
22 Hili ndilo asemalo Bwana Mungu Mwenyezi wako,
Mungu wako, yeye ambaye huwatetea watu wake:
"Tazama, nimeondoa mkononi mwako
kikombe kilichokufanya uyumbayumbe;
kutoka kikombe hicho,
kikombe cha kunywa cha ghadhabu yangu,
kamwe hutakunywa tena.
23 Nitakiweka mikononi mwa watesi wako,
wale waliokuambia,
'Anguka kifudifudi
ili tuweze kutembea juu yako.'

Ukaufanya mgongo wako kama ardhi,
kama njia yao ya kupita.”

# 52

1 Amka, amka, ee Sayuni,
jivike nguvu.
Vaa mavazi yako ya fahari,
ee Yerusalemu, mji mtakatifu.
Asiyetahiriwa na aliye najisi
hataingia kwako tena.
2 Jikung’ute mavumbi yako,
inuka, uketi kwenye kiti cha utawala, ee Yerusalemu.
Jifungue minyororo iliyo shingoni mwako,
ee Binti Sayuni uliye mateka.
3 Kwa kuwa hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Mliuzwa pasipo malipo,
nanyi mtakombolewa bila fedha.”
4 Kwa maana hili ndilo asemalo Bwana Mungu Mwenyezi:
“Hapo kwanza watu wangu walishuka Misri kuishi,
hatimaye, Ashuru wakawadhulumu.
5 “Basi sasa nina nini hapa?” asema Mwenyezi Mungu.
“Kwa kuwa watu wangu wamechukuliwa pasipo malipo,
nao wale wanaowatawala wanawadhihaki,”
asema Mwenyezi Mungu.
“Mchana kutwa

jina langu limetukanwa bila kikomo.
6 Kwa hiyo watu wangu watalijua Jina langu;
kwa hiyo katika siku ile watajua
kwamba ndimi niliyetangulia kulisema.
Naam, ni mimi."

7 Tazama jinsi miguu ya wale waletao habari njema
ilivyo mizuri juu ya milima,
wale wanaotangaza amani,
wanaoleta habari njema,
wanaotangaza wokovu,
wauambiao Sayuni,
"Mungu wako anatawala!"
8 Sikiliza! Walinzi wako wanapaza sauti zao,
pamoja wanapaza sauti zao kwa furaha.
Mwenyezi Mungu atakaporejea Sayuni,
wataliona kwa macho yao wenyewe.
9 Pazeni sauti ya nyimbo za furaha pamoja,
enyi magofu ya Yerusalemu,
kwa maana Mwenyezi Mungu amewafariji watu wake,
ameikomboa Yerusalemu.
10 Mkono mtakatifu wa Mwenyezi Mungu umefunuliwa
machoni pa mataifa yote,
nayo miisho yote ya dunia itaona
wokovu wa Mungu wetu.

11 Ondokeni, ondokeni, tokeni huko!
Msiguse kitu chochote kilicho najisi!
Tokeni kati yake mwe safi,

ninyi mchukuao vyombo vya Mwenyezi Mungu.
12 Lakini hamtaondoka kwa haraka,
wala hamtaenda kwa kukimbia;
kwa maana Mwenyezi Mungu atatangulia mbele yenu,
Mungu wa Israeli atakuwa mlinzi nyuma yenu.

### *Mateso na utukufu wa mtumishi*

13 Tazama, mtumishi wangu atatenda kwa hekima;
atatukuzwa, na kuinuliwa juu, na kukwezwa sana.
14 Kama walivyokuwa wengi
walioshangazwa naye,
kwani uso wake ulikuwa umeharibiwa sana
zaidi ya mtu yeyote
na umbo lake kuharibiwa
zaidi ya mfano wa mwanadamu:
15 hivyo atayashangaza mataifa mengi,
nao wafalme watafunga vinywa vyao kwa sababu yake.
Kwa kuwa yale ambayo hawakuambiwa, watayaona,
nayo yale wasiyoyasikia, watayafahamu.

# 53

1 Ni nani aliyeamini ujumbe wetu,
na mkono wa Mwenyezi Mungu umefunuliwa kwa nani?
2 Alikua mbele yake kama mche mwororo
na kama mzizi katika nchi kavu.

Hakuwa na uzuri wala utukufu wa kutuvutia kwake,
hakuwa na chochote katika sura yake cha kutufanya tumtamani.
3 Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu,
mtu wa huzuni nyingi, ajuaye mateso.
Kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao,
alidharauliwa, wala hatukumhesabu kuwa kitu.

4 Hakika alichukua udhaifu wetu
na akajitwika huzuni zetu;
tulidhania kuwa ameadhibiwa na Mungu,
naye akapigwa sana na kujeruhiwa.
5 Lakini alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu,
alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu;
adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake,
na kwa majeraha yake sisi tumepona.
6 Sisi sote, kama kondoo, tumepotea,
kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe,
naye Mwenyezi Mungu aliweka juu yake
maovu yetu sisi sote.

7 Alionewa na kuteswa,
hata hivyo hakufungua kinywa chake;
aliongozwa kama mwana-kondoo
apelekwaye machinjoni,
kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya wao wamkataye manyoya,
hivyo hakufungua kinywa chake.
8 Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa.
Nani awezaye kueleza kuhusu kizazi chake?

Kwa maana alikatiliwa mbali na nchi ya walio hai,
alipigwa kwa ajili ya makosa ya watu wangu.
9 Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu,
pamoja na matajiri katika kifo chake,
ingawa hakutenda jeuri,
wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

10 Lakini yalikuwa ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu
kumchubua na kumsababisha ateseke.
Ingawa Mwenyezi Mungu amefanya maisha yake
kuwa sadaka ya hatia,
ataona uzao wake na kuishi siku nyingi,
nayo mapenzi ya Mwenyezi Mungu
yatafanikiwa mkononi mwake.
11 Baada ya maumivu ya nafsi yake,
ataona nuru ya uzima na kuridhika;
kwa maarifa yake, mtumishi wangu mwenye haki
atawafanya wengi kuwa wenye haki,
naye atayachukua maovu yao.
12 Kwa hiyo nitamgawia sehemu miongoni mwa wakuu,
naye atagawana nyara pamoja na wenye nguvu,
kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti,
naye alihesabiwa pamoja na wakosaji.
Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi,
na kuwaombea wakosaji.

# 54

*Utukufu wa baadaye wa Sayuni*

1 “Imba, ewe mwanamke tasa,
wewe ambaye kamwe hukuzaa mtoto;
paza sauti kwa kuimba, piga kelele kwa furaha,
wewe ambaye kamwe hukupata uchungu;
kwa sababu watoto wa mwanamke aliyeachwa ukiwa ni wengi
kuliko wa mwanamke mwenye mume,”
asema Mwenyezi Mungu.
2 “Panua mahali pa hema lako,
tandaza mapazia ya hema lako uyaeneze mbali,
wala usiyazuie;
ongeza urefu wa kamba zako,
imarisha vigingi vyako.
3 Kwa maana utaenea upande wa kuume
na upande wa kushoto;
wazao wako watayamiliki mataifa
na kukaa katika miji yao iliyoachwa ukiwa.

4 “Usiogope, wewe hutaaibika.
Usiogope aibu, wewe hutaaibishwa.
Wewe utasahau aibu ya ujana wako,
wala hutakumbuka tena mashutumu ya ujane wako.
5 Kwa maana Muumba wako ndiye mume wako,
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ndilo jina lake,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli ni Mkombozi wako,
yeye anaitwa Mungu wa dunia yote.

6 Mwenyezi Mungu atakuita urudi
kana kwamba ulikuwa mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni;
kama mke aliyeolewa bado angali kijana
na kukataliwa," asema Mungu wako.
7 "Kwa kitambo kidogo nilikuacha,
lakini kwa huruma nyingi nitakurudisha.
8 Katika ukali wa hasira
nilikuficha uso wangu kwa kitambo,
lakini kwa fadhili za milele
nitakuwa na huruma juu yako,"
asema Mwenyezi Mungu Mkombozi wako.

9 "Kwangu mimi jambo hili ni kama siku za Nuhu,
nilipoapa kuwa maji ya Nuhu kamwe hayatafunika tena dunia.
Hivyo sasa nimeapa sitawakasirikia ninyi,
kamwe sitawakemea tena.
10 Ijapotikisika milima, na vilima viondolewe,
hata hivyo upendo wangu usiokoma kwenu hautatikisika,
wala agano langu la amani halitaondolewa,"
asema Mwenyezi Mungu, mwenye huruma juu yenu.

11 "Ewe mji uliyeteswa, uliyepigwa kwa dhoruba
na usiyetulizwa,
nitakujenga kwa almasi,
nitaweka misingi yako
kwa yakuti samawi.
12 Nitafanya minara yako ya akiki,
malango yako kwa vito ving'aavyo,
nazo kuta zako zote za vito vya thamani.

13 Watoto wako wote watafundishwa na Mwenyezi Mungu,
nayo amani ya watoto wako itakuwa kuu.
14 Kwa haki utathibitika:
Kuonewa kutakuwa mbali nawe;
hutaogopa chochote.
Hofu itakuwa mbali nawe;
haitakukaribia wewe.
15 Kama mtu yeyote akikushambulia,
haitakuwa kwa ruhusa yangu;
yeyote akushambuliaye
atajisalimisha kwako.

16 “Tazama, ni mimi niliyemuumba mhunzi,
yeye afukutaye makaa kuwa moto,
na kutengeneza silaha inayofaa kwa kazi yake.
Tena ni mimi niliyemwambia mharibu
kufanya uharibifu mwingi.
17 Hakuna silaha itakayofanyizwa dhidi yako
itakayofanikiwa,
nawe utauthibitisha kuwa mwongo
kila ulimi utakaokushtaki.
Huu ndio urithi wa watumishi wa Mwenyezi Mungu
na hii ndiyo haki yao inayotoka kwangu,”
asema Mwenyezi Mungu.

# 55

### *Mwaliko kwa wenye kiu*

1 “Haya! Njooni, ninyi nyote wenye kiu,
njooni kwenye maji;
nanyi ambao hamna fedha,

njooni, nunueni na mle!
Njooni, nunueni divai na maziwa
bila fedha na bila gharama.
2 Kwa nini kutumia fedha kwa kitu ambacho si chakula,
na kutaabikia kitu kisichoshibisha?
Sikilizeni, nisikilizeni mimi na mle kilicho kizuri,
nazo nafsi zenu zitafurahia utajiri wa unono.
3 Tegeni sikio mje kwangu,
nisikieni mimi, ili nafsi zenu zipate kuishi.
Nitafanya agano la milele nanyi,
pendo la uaminifu nililomwahidi Daudi.
4 Tazama, nimemfanya kuwa shahidi wa mataifa,
kiongozi na jemadari wa mataifa.
5 Hakika utaita mataifa usiyoyajua,
nayo mataifa yale yasiyokujua yataharakisha kukujia,
kwa sababu ya Mwenyezi Mungu, Mungu wako,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli,
kwa maana amekutukuza."

6 Mtafuteni Mwenyezi Mungu maadamu anapatikana;
mwiteni maadamu yu karibu.
7 Mtu mwovu na aiache njia yake,
na mtu mbaya na ayaache mawazo yake.
Yeye na amrudie Mwenyezi Mungu, naye atamrehemu,
arudi kwa Mungu wetu, kwa kuwa atamsamehe bure kabisa.

8 "Kwa kuwa mawazo yangu si mawazo yenu,
wala njia zenu si njia zangu,"
asema Mwenyezi Mungu.

9 “Kama vile mbingu zilivyo juu kuliko dunia,
ndivyo njia zangu zilivyo juu kuliko njia zenu
na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.
10 Kama vile mvua na theluji
ishukavyo kutoka mbinguni,
nayo hairudi tena huko
bila kunywesha dunia
na kuichipusha na kuistawisha,
ili itoe mbegu kwa mpanzi
na mkate kwa mlaji,
11 ndivyo lilivyo neno langu litokalo kinywani mwangu:
Halitanirudia tupu,
bali litatimiliza lile nililokusudia,
na litafanikiwa katika kusudi lile nililolituma.
12 Mtatoka nje kwa furaha
na kuongozwa kwa amani;
milima na vilima
vitapaza sauti kwa nyimbo mbele yenu,
nayo miti yote ya shambani
itapiga makofi.
13 Badala ya kichaka cha miiba
itaota miti ya misunobari,
na badala ya michongoma
utaota mhadasi.
Hili litakuwa jambo la kumpatia Mwenyezi Mungu jina,
kwa ajili ya ishara ya milele,
ambayo haitaharibiwa.”

# 56

*Wokovu kwa wengine*

1 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Dumisheni haki
na mkatende lile lililo sawa,
kwa maana wokovu wangu u karibu
na haki yangu itafunuliwa upesi.
2 Amebarikiwa mtu yule atendaye hili,
mtu yule alishikaye kwa uthabiti,
yeye ashikaye Sabato bila kuinajisi,
auzuiaye mkono wake usifanye uovu wowote.”

3 Usimwache mgeni aambatanaye na Mwenyezi Mungu aseme,
“Hakika Mwenyezi Mungu atanitenga na watu wake.”
Usimwache towashi yeyote alalamike akisema,
“Mimi ni mti mkavu tu.”
4 Kwa kuwa hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Kwa matowashi washikao Sabato zangu,
ambao huchagua kile kinachonipendeza
na kulishika sana agano langu:
5 hao nitawapa ndani ya Hekalu langu na kuta zake
kumbukumbu na jina bora
kuliko kuwa na watoto wa kiume na wa kike:
nitawapa jina lidumulo milele,
ambalo halitakatiliwa mbali.
6 Wageni wanaoambatana na Mwenyezi Mungu
ili kumtumikia,
kulipenda jina la Mwenyezi Mungu,
na kumwabudu yeye,
wote washikao Sabato bila kuinajisi
na ambao hushika sana agano langu:

7 hawa nitawaleta kwenye mlima wangu mtakatifu
na kuwapa furaha ndani ya nyumba yangu ya sala.
Sadaka zao za kuteketeza na dhabihu zao
zitakubalika juu ya madhabahu yangu;
kwa maana nyumba yangu itaitwa
nyumba ya sala kwa mataifa yote."
8 Bwana Mungu Mwenyezi asema, yeye awakusanyaye
Waisraeli waliohamishwa:
"Bado nitawakusanya wengine kwao
zaidi ya hao ambao wamekusanywa tayari."

### *Mashtaka ya Mwenyezi Mungu dhidi ya waovu*

9 Njooni, enyi wanyama wote wa kondeni,
njooni mle, ninyi wanyama wote wa mwituni!
10 Walinzi wa Israeli ni vipofu,
wote wamepungukiwa na maarifa;
wote ni mbwa walio bubu,
hawawezi kubweka;
hulala na kuota ndoto,
hupenda kulala.
11 Ni mbwa wenye tamaa kubwa,
kamwe hawatosheki.
Wao ni wachungaji waliopungukiwa na ufahamu;
wote wamegeukia njia yao wenyewe,
kila mmoja hutafuta faida yake mwenyewe.
12 Kila mmoja hulia, "Njooni, tupate mvinyo!
Tunywe kileo sana!
Kesho itakuwa kama leo,
au hata bora zaidi."

# 57

### *Ibada batili ya sanamu ya Israeli*

1 Mwenye haki hupotea,
wala hakuna hata mmoja awazaye hilo moy-oni mwake;
watu wanaomcha Mungu huondolewa,
wala hakuna hata mmoja anayeelewa
kuwa wenye haki wameondolewa
ili wasipatikane na maovu.
2 Wale wanaoenda kwa unyofu
huwa na amani;
hupata pumziko wanapolala mautini.

3 "Lakini ninyi:
Njooni hapa, ninyi wana wa wachawi,
ninyi wazao wa wazinzi na makahaba!
4 Mnamdhihaki nani?
Ni nani mnayemcheka kwa dharau,
na kumtolea ndimi zenu?
Je, ninyi si watoto wa waasi,
uzao wa waongo?
5 Mnawaka tamaa katikati ya mialoni
na chini ya kila mti uliotanda matawi;
mnawatoa kafara watoto wenu kwenye mabonde
na chini ya majabali yenye mianya.

6 "Sanamu zilizo kati ya mawe laini ya mabondeni ndizo fungu lenu;
hizo ndizo sehemu yenu.
Naam, kwa hizo mmemimina sadaka za vinywaji,
na kutoa sadaka za nafaka.
Katika haya yote,

niendelee kuona huruma?
7 Umeweka kitanda chako juu kwenye kilima
kirefu kilichoinuka,
huko ulienda kutoa dhabihu zako.
8 Nyuma ya milango yako na miimo yako
umeweka alama zako za kipagani.
Kwa kuniacha mimi, ulifunua kitanda chako,
umepanda juu yake na kukipanua sana;
ulifanya patano na wale ambao unapenda vitanda vyao,
nawe uliangalia uchi wao.
9 Ulienda kwa Moleki* ukiwa na mafuta ya
zeituni,
na ukaongeza manukato yako.
Ukawatuma wajumbe wako mbali sana,
ukashuka kwenye kaburi† lenyewe!
10 Ulikuwa umechoshwa na njia zako zote,
lakini hukusema, 'Hakuna tumaini.'
Ulipata uhuisho wa nguvu zako,
kwa sababu hiyo hukuzimia.

11 "Ni nani uliyemhofu hivyo na kumwogopa
hata ukawa mwongo kwangu,
wala hukunikumbuka
au kutafakari hili moyoni mwako?
Si ni kwa sababu nimekuwa kimya muda mrefu
hata huniogopi?
12 Nitaifunua haki yako na matendo yako,
nayo hayatakufaidi.
13 Utakapolia kwa kuhitaji msaada,
sanamu zako ulizojikusanyia na zikuokoe!

---

* **57:9** au *kwa mfalme* † **57:9** Kaburi hapa maana yake ni *Kuzimu*; kwa Kiebrania ni *Sheol.*

Upepo utazipeperusha zote,
pumzi peke yake itazipeperusha,
Lakini mtu atakayenifanya kimbilio lake,
atairithi nchi
na kuumiliki mlima wangu mtakatifu."

### *Faraja kwa wenye majuto*

14 Tena itasemwa:
"Jengeni, jengeni, itengenezeni njia!
Ondoeni vikwazo katika njia ya watu wangu."
15 Kwa maana hili ndilo asemalo Aliye juu,
yeye aliyeinuliwa sana,
yeye aishiye milele,
ambaye jina lake ni Mtakatifu:
"Ninaishi mahali palipoinuka
na patakatifu,
lakini pia pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu,
na mwenye roho ya unyenyekevu,
ili kuzihuisha roho za wanyenyekevu
na kuihuisha mioyo yao waliotubu.
16 Sitaendelea kulaumu milele,
wala sitakasirika siku zote,
kwa kuwa roho ya mwanadamu
ingezimia mbele zangu:
yaani pumzi ya mwanadamu niliyemuumba.
17 Nilighadhibika na tamaa yake ya dhambi;
nilimwadhibu, nikauficha uso wangu kwa hasira,
na bado aliendelea katika njia zake za tamaa.
18 Nimeziona njia zake, lakini nitamponya,
nitamwongoza na kumrudishia upya faraja,
19 nikiumba sifa midomoni ya waombolezaji
katika Israeli.

Amani, amani, kwa wale walio mbali
na kwa wale walio karibu,"
asema Mwenyezi Mungu. "Nami nitawaponya."
20 Bali waovu ni kama bahari ichafukayo,
ambayo haiwezi kutulia,
mawimbi yake hutupa takataka na matope.
21 Mungu wangu asema,
"Hakuna amani kwa waovu."

# 58

*Mfungo wa kweli*

1 "Piga kelele, usizuie.
Paza sauti yako kama tarumbeta.
Watangazieni watu wangu uasi wao,
na kwa nyumba ya Yakobo dhambi zao.
2 Kwa maana kila siku hunitafuta,
wanaonekana kutaka kujua njia zangu,
kana kwamba walikuwa taifa linalotenda lililo sawa,
na ambalo halijaziacha amri za Mungu wake.
Hutaka kwangu maamuzi ya haki,
nao hutamani Mungu awakaribie.
3 Wao husema, 'Mbona tumefunga, nawe hujaona?
Mbona tumejinyenyekeza, nawe huangalii?'

"Lakini katika siku ya kufunga kwenu, mnafanya mnavyotaka
na kuwadhulumu wafanyakazi wenu wote.
4 Kufunga kwenu huishia kwenye magomvi na mapigano,

na kupigana ninyi kwa ninyi kwa ngumi za uovu.
Hamwezi kufunga kama mnavyofanya leo
na kutazamia sauti zenu kusikiwa huko juu.
5 Je, hii ndiyo aina ya mfungo niliouchagua,
siku moja tu ya mtu kujinyenyekeza?
Je, ni kwa kuinamisha kichwa chini kama tete,
na kwa kujilaza juu ya gunia na majivu?
Je, huo ndio mnaouita mfungo,
siku iliyokubalika kwa Mwenyezi Mungu?

6 “Je, hii si ndiyo aina ya mfungo niliyoichagua:
kufungua minyororo ya udhalimu,
na kufungua kamba za nira,
kuwaweka huru waliodhulumiwa,
na kuvunja kila nira?
7 Je, sio kushirikiana chakula chako na wenye njaa
na kuwapatia maskini wasiokuwa na makao hifadhi,
unapomwona aliye uchi, umvike,
wala si kumkimbia mtu wa mwili wako
na damu yako mwenyewe?
8 Ndipo nuru yako itajitokeza kama mapambazuko
na uponyaji wako utatokea upesi;
ndipo haki yako itakapokutangulia mbele yako,
na utukufu wa Mwenyezi Mungu utakuwa mlinzi nyuma yako.
9 Ndipo utaita, naye Mwenyezi Mungu atajibu,
utalia kuomba msaada,
naye atasema: Mimi hapa.

“Ukiiondoa nira ya udhalimu,

na kunyoosha kidole na kuzungumza maovu,
10 nanyi mkimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi zenu
na kutosheleza mahitaji ya waliodhulumiwa,
ndipo nuru yenu itang'aa gizani,
nao usiku wenu utakuwa kama adhuhuri.
11 Mwenyezi Mungu atakuongoza siku zote,
atayatosheleza mahitaji yako katika nchi kame,
naye ataitia nguvu mifupa yako.
Utakuwa kama bustani iliyonyweshwa vizuri,
kama chemchemi ambayo maji yake hayakauki kamwe.
12 Watu wako watajenga tena magofu ya zamani
na kuinua misingi ya kale;
utaitwa Mwenye Kukarabati Kuta Zilizobomoka,
Mwenye Kurejesha Barabara za Makao.

13 "Ukitunza miguu yako isivunje Sabato,
na kutokufanya kama vile upendavyo katika siku yangu takatifu,
ukiita Sabato siku ya furaha
na siku takatifu ya Mwenyezi Mungu ya kuheshimiwa,
kama utaiheshimu kwa kutoenenda
katika njia zako mwenyewe,
na kutokufanya yakupendezayo
au kusema maneno ya upuzi,
14 ndipo utakapojipatia furaha yako katika Mwenyezi Mungu,
nami nitakufanya upande juu ya miinuko ya nchi

na kusherehekea urithi wa Yakobo baba yako."
Kinywa cha Mwenyezi Mungu kimenena haya.

# 59

*Dhambi, toba na ukombozi*

1 Hakika mkono wa Mwenyezi Mungu si mfupi hata usiweze kuokoa,
wala sikio lake si zito hata lisiweze kusikia.
2 Lakini maovu yenu yamewatenga
ninyi na Mungu wenu,
dhambi zenu zimewaficha ninyi uso wake,
ili asisikie.
3 Kwa maana mikono yenu imetiwa unajisi kwa damu,
na vidole vyenu kwa hatia.
Midomo yenu imenena uongo,
nazo ndimi zenu zimenong'ona mambo maovu.
4 Hakuna hata mmoja anayedai kwa haki;
hakuna hata mmoja anayetetea kwa haki.
Wanategemea mabishano matupu na kusema uongo,
huchukua mimba ya magomvi na kuzaa uovu.
5 Huangua mayai ya nyoka wenye sumu kali
na kutanda wavu wa buibui.
Yeyote alaye mayai yao atakufa,
nalo moja likianguliwa, nyoka hutoka humo.
6 Utando wao wa buibui haufai kwa mavazi;
hawawezi kujifunika kwa kile walichokitengeneza.
Matendo yao ni matendo maovu,
vitendo vya jeuri vipo mikononi mwao.

7 Miguu yao hukimbilia kwenye dhambi,
ni myepesi kumwaga damu isiyo na hatia.
Mawazo yao ni mawazo maovu;
uharibifu na maangamizi huonekana katika njia zao.
8 Hawajui njia ya amani,
hakuna haki katika mapito yao.
Wameyageuza kuwa njia za upotovu,
hakuna apitaye njia hizo atakayeifahamu amani.

9 Hivyo uadilifu uko mbali nasi,
nayo haki haitufikii.
Tunatazamia nuru, kumbe! Yote ni giza,
tunatazamia mwanga, lakini tunatembea katika giza nene.
10 Tunapapasa ukuta kama vipofu,
tunapapasa katika njia zetu kama watu wasio na macho.
Adhuhuri tunajikwaa kama wakati wa gizagiza;
kati ya wenye nguvu, tuko kama wafu.
11 Wote tunanguruma kama dubu;
tunalia kwa maombolezo kama hua.
Tunatafuta haki, kumbe hakuna kabisa;
tunatafuta wokovu, lakini uko mbali.

12 Kwa sababu makosa yetu ni mengi machoni pako,
na dhambi zetu zinashuhudia dhidi yetu.
Makosa yetu yako pamoja nasi daima,
nasi tunayatambua maovu yetu:
13 Uasi na udanganyifu dhidi ya Mwenyezi Mungu,

kumgeuzia Mungu wetu kisogo,
tukichochea udhalimu na maasi,
tukinena uongo ambao mioyo yetu imeuhifadhi.
14 Hivyo uadilifu umerudishwa nyuma,
nayo haki inasimama mbali,
kweli imejikwaa njiani,
uaminifu hauwezi kuingia.
15 Kweli haipatikani popote,
na yeyote aepukaye uovu huwa mawindo.

Mwenyezi Mungu alitazama, naye akachukizwa
kwamba hapakuwa na haki.
16 Aliona kuwa hapakuwa hata mtu mmoja,
akashangaa kwamba hapakuwa hata mtu mmoja wa kuingilia kati.
Hivyo mkono wake mwenyewe
ndio uliomfanyia wokovu,
nayo haki yake mwenyewe
ndiyo iliyomtegemeza.
17 Alivaa haki kama dirii kifuani mwake,
na chapeo ya wokovu kichwani mwake,
alivaa mavazi ya kisasi
naye akajifunga wivu kama joho.
18 Kulingana na kile walichokuwa wametenda,
ndivyo atakavyolipa
ghadhabu kwa watesi wake
na kisasi kwa adui zake,
atavilipa visiwa sawa na wanavyostahili.
19 Kuanzia magharibi, watu wataliogopa jina la Mwenyezi Mungu
na kuanzia mawio ya jua, watauheshimu utukufu wake.

Adui atakapokuja kama mafuriko,
Roho wa Mwenyezi Mungu atainua kiwango dhidi yake na kumshinda.

20 "Mkombozi atakuja Sayuni,
kwa wale wa Yakobo
wanaozitubu dhambi zao,"
asema Mwenyezi Mungu.
21 "Bali mimi, hili ndilo agano langu nao,"
asema Mwenyezi Mungu. "Roho wangu Mtakat-
ifu, aliye juu yenu, na maneno yangu niliy-
oyaweka vinywani vyenu, havitaondoka viny-
wani mwenu, wala kutoka vinywani mwa watoto
wenu, wala kutoka vinywani mwa wazao wao,
kuanzia sasa na hata milele," asema Mwenyezi
Mungu.

# 60

### *Utukufu wa Sayuni*

1 "Ondoka, angaza, kwa kuwa nuru yako imekuja
na utukufu wa Mwenyezi Mungu umezuka juu yako.
2 Tazama, giza litaifunika dunia,
na giza nene litayafunika mataifa,
lakini Mwenyezi Mungu atazuka juu yako
na utukufu wake utaonekana juu yako.
3 Mataifa watakuja kwenye nuru yako
na wafalme kwa mwanga wa mapambazuko yako.

4 "Inua macho yako na utazame pande zote:
Wote wanakusanyika na kukujia,
wana wako wanakuja toka mbali,

nao binti zako wanabebwa mikononi.
5 Ndipo utatazama na kutiwa nuru,
moyo wako utasisimka na kujaa furaha,
mali iliyo baharini italetwa kwako,
utajiri wa mataifa utakujilia.
6 Makundi ya ngamia yatajaa katika nchi yako,
ngamia vijana wa Midiani na Efa.
Nao watu wote wanaotoka Sheba watakuja,
wakichukua dhahabu na uvumba
na kutangaza sifa za Mwenyezi Mungu.
7 Makundi yote ya Kedari yatakusanyika kwako,
kondoo dume wa Nebayothi watakutumikia,
watakubalika kama sadaka juu ya madhabahu yangu,
nami nitalipamba Hekalu langu tukufu.

8 “Ni nani hawa warukao kama mawingu,
kama hua kuelekea kwenye viota vyao?
9 Hakika visiwa vinanitazama;
merikebu za Tarshishi* ndizo zinazotangulia,
zikiwaleta wana wenu kutoka mbali,
wakiwa na fedha na dhahabu zao,
kwa heshima ya Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli,
kwa maana amekujalia utukufu.

10 “Wageni watazijenga upya kuta zako,
na wafalme wao watakutumikia.
Ingawa katika hasira nilikupiga,

---

* **60:9** au: *za biashara*(taz. 1 Wafalme 10:22; 22:48; 2 Nyakati 9:21; 20:36; Isaya 2:16).

lakini katika upendeleo wangu
nitakuonesha huruma.
11 Malango yako yatakuwa wazi siku zote,
kamwe hayatafungwa, mchana wala usiku,
ili watu wapate kukuletea utajiri wa mataifa:
wafalme wao wakiongoza maandamano ya ushindi.
12 Kwa maana taifa au ufalme ule ambao hautakutumikia utaangamia;
utaharibiwa kabisa.

13 “Utukufu wa Lebanoni utakujilia,
msunobari, mvinje pamoja na mteashuri,
ili kupapamba mahali pangu patakatifu,
nami nitapatukuza mahali pa miguu yangu.
14 Wana wa wale waliokutesa watakuja wakisujudu mbele yako;
wote wanaokudharau watasujudu miguuni pako;
nao watakuita Mji wa Mwenyezi Mungu,
Sayuni ya Aliye Mtakatifu wa Israeli.

15 “Ingawa umeachwa na kuchukiwa,
bila yeyote anayesafiri ndani yako,
nitakufanya kuwa fahari ya milele,
na furaha ya vizazi vyote.
16 Utanyonya maziwa ya mataifa,
na kunyonyeshwa matiti ya wafalme.
Ndipo utakapojua kwamba Mimi, Mwenyezi Mungu,
ni Mwokozi wako, Mkombozi wako,
niliye Mwenye Nguvu wa Yakobo.
17 Badala ya shaba nitakuletea dhahabu,

na fedha badala ya chuma.
Badala ya mti nitakuletea shaba,
na chuma badala ya mawe.
Nitafanya amani kuwa mtawala wako,
na haki kuwa mfalme wako.
18 Jeuri hazitasikika tena katika nchi yako,
wala maangamizi au uharibifu
ndani ya mipaka yako,
lakini utaita kuta zako Wokovu,
na malango yako Sifa.
19 Jua halitakuwa tena nuru yako mchana,
wala mwangaza wa mwezi hautakuangazia,
kwa maana Mwenyezi Mungu atakuwa nuru yako ya milele,
naye Mungu wako atakuwa utukufu wako.
20 Jua lako halitazama tena,
nao mwezi wako hautafifia tena;
Mwenyezi Mungu atakuwa nuru yako milele,
nazo siku zako za huzuni zitakoma.
21 Ndipo watu wako wote watakuwa waadilifu,
nao wataimiliki nchi milele.
Wao ni chipukizi nililolipanda,
kazi ya mikono yangu,
ili kuonesha utukufu wangu.
22 Aliye mdogo kwenu atakuwa elfu,
mdogo kuliko wote atakuwa taifa lenye nguvu.
Mimi ndimi Mwenyezi Mungu;
katika wakati wake nitayatimiza haya upesi.”

# 61

## *Mwaka wa upendeleo wa Mwenyezi Mungu*

1 Roho wa Bwana Mungu Mwenyezi yu juu yangu,
kwa sababu Mwenyezi Mungu amenipaka mafuta
kuwahubiria maskini habari njema.
Amenituma kuwafariji waliovunjika moyo,
kuwatangazia mateka uhuru wao,
na hao waliofungwa
habari za kufunguliwa kwao;
2 kutangaza mwaka wa Mwenyezi Mungu uliokubaliwa,
na siku ya kisasi ya Mungu wetu,
kuwafariji wote wanaoomboleza,
3 na kuwapa mahitaji
wale wanaohuzunika katika Sayuni,
ili kuwapa taji za uzuri badala ya majivu,
mafuta ya furaha badala ya maombolezo,
vazi la sifa badala ya roho ya kukata tamaa.
Nao wataitwa mialoni ya haki,
pando la Mwenyezi Mungu,
ili kuonesha utukufu wake.

4 Watajenga upya magofu ya zamani
na kupatengeneza mahali palipoachwa ukiwa zamani;
watafanya upya miji iliyoharibiwa,
iliyoachwa ukiwa kwa vizazi vingi.
5 Wageni watayachunga makundi yenu,
wageni watafanya kazi katika mashamba yenu,
na kutunza mashamba yenu ya mizabibu.
6 Nanyi mtaitwa makuhani wa Mwenyezi Mungu,
mtaitwa watumishi wa Mungu wetu.

Mtakula utajiri wa mataifa,
nanyi katika utajiri wao mtajisifu.

7 Badala ya aibu yao
watu wangu watapokea sehemu maradufu,
na badala ya fedheha
watafurahia katika urithi wao;
hivyo watarithi sehemu maradufu katika nchi yao,
nayo furaha ya milele itakuwa yao.

8 "Kwa maana Mimi, Mwenyezi Mungu, napenda haki,
na ninachukia unyang'anyi na uovu.
Katika uaminifu wangu nitawapa malipo yao
na kufanya agano la milele nao.
9 Wazao wao watajulikana miongoni mwa mataifa,
na uzao wao miongoni mwa makabila ya watu.
Wale wote watakaowaona watatambua
kuwa ni taifa ambalo Mwenyezi Mungu amelibariki."

10 Ninafurahia sana katika Mwenyezi Mungu,
nafsi yangu inashangilia katika Mungu wangu.
Kwa maana amenivika mavazi ya wokovu,
na kunipamba kwa joho la haki,
kama vile bwana arusi apambavyo
kichwa chake kama kuhani,
na kama bibi arusi ajipambavyo
kwa vito vyake vya thamani.

11 Kwa maana kama vile ardhi ifanyavyo chipukizi kuota,
na bustani isababishavyo mbegu kuota,
ndivyo Bwana Mungu Mwenyezi atafanya haki na sifa
zichipuke mbele ya mataifa yote.

# 62

## *Jina jipya la Sayuni*

1 Kwa ajili ya Sayuni sitanyamaza,
kwa ajili ya Yerusalemu sitatulia,
hadi haki yake itakapoangaza kama mapambazuko,
wokovu wake kama mwanga wa moto.
2 Mataifa wataona haki yako,
nao wafalme wote wataona utukufu wako;
wewe utaitwa kwa jina jipya
lile ambalo kinywa cha Mwenyezi Mungu kitatamka.
3 Utakuwa taji la fahari mkononi mwa Mwenyezi Mungu,
taji la kifalme mkononi mwa Mungu wako.
4 Hawatakuita tena Aliyeachwa,
wala nchi yako kuiita Ukiwa.
Bali utaitwa Hefsiba*,
nayo nchi yako itaitwa Beula†,
kwa maana Mwenyezi Mungu atakufurahia,
nayo nchi yako itaolewa.
5 Kama vile kijana aoavyo mwanamwali,
ndivyo Mwashi wako atakavyokuoa‡;

---

* **62:4** maana yake *Yeye ninayemfurahia* † **62:4** maana yake *Aliyeolewa* ‡ **62:5** au *ndivyo wanao watakavyokuoa wewe*

kama bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi wake,
ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe.

6 Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, ee Yerusalemu,
hawatanyamaza mchana wala usiku.
Ninyi wenye kumwita Mwenyezi Mungu,
msitulie,
7 msimwache apumzike hadi atakapoufanya imara Yerusalemu
na kuufanya uwe sifa ya dunia.

8 Mwenyezi Mungu ameapa kwa mkono wake wa kuume
na kwa mkono wake wenye nguvu:
“Kamwe sitawapa tena adui zenu
nafaka zenu kama chakula chao;
kamwe wageni hawatakunywa tena
divai mpya ambayo mmeitaabikia,
9 lakini wale waivunao nafaka wataila
na kumsifu Mwenyezi Mungu,
nao wale wakusanyao zabibu watainywa divai yake
katika nyua za patakatifu pangu.”

10 Piteni, piteni katika malango!
Tengenezeni njia kwa ajili ya watu.
Jengeni, jengeni njia kuu!
Ondoeni mawe.
Inueni bendera kwa ajili ya mataifa.

11 Mwenyezi Mungu ametoa tangazo

hadi miisho ya dunia:
“Mwambie Binti Sayuni,
‘Tazama, mwokozi wako anakuja!
Tazama ujira wake uko pamoja naye,
na malipo yake yanafuatana naye!’ ”
12 Wataitwa Watu Watakatifu,
Waliokombolewa na Mwenyezi Mungu;
nawe utaitwa Aliyetafutwa,
Mji Usioachwa Tena.

# 63

*Siku ya Mwenyezi Mungu ya kisasi na ukombozi*

1 Ni nani huyu anayekuja kutoka Edomu,
kutoka Bosra, mwenye mavazi yaliyotiwa madoa mekundu?
Ni nani huyu, aliyevikwa joho la kifahari,
anayetembea kwa ukuu wa nguvu zake?

“Mimi ndimi, nisemaye katika haki,
mwenye nguvu wa kuokoa.”

2 Kwa nini mavazi yako ni mekundu,
kama ya yule akanyagaye shinikizo la zabibu?

3 “Nimekanyaga shinikizo la kukamulia zabibu peke yangu;
kutoka mataifa hakuna mtu aliyekuwa pamoja nami.
Nimewaponda kwa miguu katika hasira yangu
na kuwakanyaga chini katika ghadhabu yangu;

damu yao ilitia matone kwenye mavazi yangu,
na kutia madoa nguo zangu zote.
4 Kwa kuwa siku ya kisasi ilikuwa moyoni mwangu,
mwaka wa ukombozi wangu umefika.
5 Nilitazama, lakini hapakuwa yeyote wa kunisaidia,
nilishangaa kwa kuwa hapakuwa yeyote aliyetoa msaada;
hivyo mkono wangu wenyewe ndio ulionifanyia wokovu,
na ghadhabu yangu mwenyewe ndiyo iliyonitegemeza.
6 Nilikanyaga mataifa kwa miguu katika hasira yangu,
katika ghadhabu yangu niliwalewesha,
na kumwaga damu yao juu ya ardhi."

*Kusifu na kuomba*

7 Nitasimulia kuhusu wema wa Mwenyezi Mungu,
kwa matendo ambayo apaswa kusifiwa,
sawasawa na yote ambayo Mwenyezi Mungu ametenda kwa ajili yetu:
naam, mambo mengi mema aliyoyatenda
kwa ajili ya nyumba ya Israeli,
sawasawa na huruma zake
na wema wake mwingi.
8 Alisema, "Hakika wao ni watu wangu,
wana ambao hawatanidanganya";
hivyo akawa Mwokozi wao.
9 Katika taabu zao zote naye alitaabika,
na malaika wa uso wake akawaokoa.

Katika upendo wake na rehema zake aliwakomboa,
akawainua na kuwachukua siku zote zilizopita.
10 Lakini waliasi,
na kumhuzunisha Roho Mtakatifu wa Mungu.
Hivyo aligeuka na kuwa adui yao,
na yeye mwenyewe akapigana dhidi yao.

11 Ndipo watu wake wakazikumbuka siku zilizopita,
siku za Musa na watu wake:
yuko wapi yeye aliyewaleta kupitia katikati ya bahari,
pamoja na wachungaji wa kundi lake?
Yuko wapi yule aliyeweka
Roho wake Mtakatifu katikati yao,
12 aliyetuma mkono wake uliotukuka wenye nguvu
kuwa katika mkono wa kuume wa Musa,
aliyegawa maji ya bahari mbele yao,
ili kujipatia jina milele,
13 aliyewaongoza kupitia kwenye vilindi?
Kama farasi katika nchi iliyo wazi,
wao hawakujikwaa,
14 kama ng'ombe wanaoshuka bondeni,
walipewa pumziko na Roho wa Mwenyezi Mungu.
Hivi ndivyo ulivyowaongoza watu wako
ili kujipatia jina tukufu.

15 Tazama chini kutoka mbinguni ukaone
kutoka kiti chako cha enzi

kilichoinuliwa juu, kitakatifu na kitukufu.
Uko wapi wivu wako na uweza wako?
Umetuzuilia wema wako na huruma zako.
16 Lakini wewe ni Baba yetu,
ingawa Ibrahimu hatufahamu sisi
wala Israeli hatutambui;
wewe, Ee Mwenyezi Mungu, ndiwe Baba yetu,
Mkombozi wetu tangu zamani za kale ndilo jina lako.
17 Ee Mwenyezi Mungu, kwa nini unatuacha twende mbali na njia zako,
na kuifanya mioyo yetu migumu hata hatukukuheshimu?
Rudi kwa ajili ya watumishi wako,
yale makabila ambayo ni urithi wako.
18 Kwa maana kwa muda mfupi watu wako walimiliki mahali pako patakatifu,
lakini sasa adui zetu wamepakanyaga mahali patakatifu pako.
19 Sisi tumekuwa kama wale ambao hujawatawala kamwe,
kama wale ambao hawajaitwa kwa jina lako.

# 64

1 Laiti ungepasua mbingu na kushuka chini,
ili milima itetemeke mbele zako!
2 Kama vile moto unavyoteketeza vijiti
na kusababisha maji kuchemka,
shuka ukafanye jina lako lijulikane kwa adui zako,
na kusababisha mataifa yatetemeke mbele zako!

3 Kwa maana ulipofanya mambo ya kutisha ambayo hatukuyatazamia,
ulishuka, nayo milima ikatetemeka mbele zako.
4 Tangu nyakati za zamani hakuna yeyote aliyesikia,
hakuna sikio lililotambua,
hakuna jicho lililomwona Mungu mwingine ila wewe,
anayetenda mambo kwa ajili ya wale wamngojeao.
5 Uliwasaidia watu wale watendao yaliyo haki kwa furaha,
wale wazikumbukao njia zako.
Lakini wakati tulipoendelea kutenda dhambi kinyume na njia zako,
ulikasirika.
Tutawezaje basi kuokolewa?
6 Sisi sote tumekuwa kama mtu aliye najisi,
nayo matendo yetu yote ya uadilifu ni kama matambaa machafu;
sisi sote tunasinyaa kama jani,
na kama upepo maovu yetu hutupeperusha.
7 Hakuna yeyote anayeliitia jina lako
wala anayejitahidi kukushika,
kwa kuwa umetuficha uso wako
na kutuacha tudhoofike kwa sababu ya dhambi zetu.

8 Lakini, Ee Mwenyezi Mungu, wewe ndiwe Baba yetu.
Sisi ni udongo, na wewe ndiwe mfinyanzi;
sisi sote tu kazi ya mkono wako.
9 Ee Mwenyezi Mungu, usikasirike kupita kiasi,

usizikumbuke dhambi zetu milele.
Ee Bwana, utuangalie, twakuomba,
kwa kuwa sisi sote tu watu wako.
10 Miji yako mitakatifu imekuwa jangwa;
hata Sayuni ni jangwa, Yerusalemu ni ukiwa.
11 Hekalu letu takatifu na tukufu,
ambako baba zetu walikusifu wewe,
limechomwa kwa moto,
navyo vitu vyote tulivyovithamini
vimeharibika.
12 Ee Mwenyezi Mungu, baada ya haya yote, utajizuia?
Je, utanyamaza, na kutuadhibu kupita kiasi?

# 65

*Hukumu na wokovu*

1 "Nilijifunua kwa watu wale ambao hawakuniulizia.
Nimeonekana na watu wale ambao hawakunitafuta.
Kwa taifa lile ambalo halikuliita Jina langu,
nilisema, 'Niko hapa, niko hapa.'
2 Mchana kutwa nimeinyoosha mikono yangu
kwa watu wakaidi,
wanaoenda katika njia ambazo si nzuri,
wafuatao mawazo yao wenyewe:
3 taifa ambalo daima hunikasirisha
machoni pangu,
wakitoa dhabihu katika bustani
na kufukiza uvumba juu ya madhabahu za matofali;
4 watu waketio katika makaburi
na kukesha mahali pa siri,
walao nyama za nguruwe,

nazo sufuria zao zina mchuzi wa nyama
zilizo najisi,
5 wasemao, 'Kaa mbali; usinikaribie,
kwa maana mimi ni mtakatifu mno kwako!'
Watu wa aina hiyo ni moshi katika pua zangu,
ni moto uwakao mchana kutwa.

6 "Tazama, jambo hili hubakia limeandikwa
mbele zangu:
sitanyamaza, bali nitalipiza kwa ukamilifu;
nitalipiza mapajani mwao:
7 dhambi zenu na dhambi za baba zenu,"
asema Mwenyezi Mungu.
"Kwa sababu walitoa dhabihu za kuteketezwa juu
ya milima
na kunichokoza mimi juu ya vilima,
nitawapimia mapajani mwao
malipo makamilifu kwa matendo yao ya zamani."
8 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
"Kama vile divai mpya ingali bado inapatikana
katika kishada cha zabibu,
nao watu husema, 'Usikiharibu,
kwa kuwa bado kuna baraka ndani yake,'
hivyo ndivyo nitakavyofanya kwa ajili ya watumishi wangu;
sitawaangamiza wote.
9 Nitawaleta wazao kutoka kwa Yakobo,
na kutoka kwa Yuda watakaomiliki milima
yangu,
nao watu wangu wateule watairithi,
nako huko wataishi watumishi wangu.
10 Sharoni itakuwa malisho
kwa ajili ya makundi ya kondoo,

na Bonde la Akori mahali pa kupumzikia
kwa makundi ya ng'ombe,
kwa ajili ya watu wangu wanaonitafuta.

11 “Bali ninyi mnaomwacha Mwenyezi Mungu
na kuusahau mlima wangu mtakatifu,
ninyi mnaoandaa meza kwa ajili ya Bahati*,
na kujaza mabakuli ya mvinyo uliochanganywa
kwa ajili ya Ajali†,
12 nitawaagiza mfe kwa upanga,
nanyi nyote mtainama chini ili kuchinjwa;
kwa kuwa niliwaita lakini hamkuitika,
nilisema lakini hamkusikiliza.
Mlitenda maovu machoni pangu,
nanyi mkachagua mambo yale yanayonichukiza.”
13 Kwa hiyo hili ndilo asemalo Bwana Mungu Mwenyezi:
“Watumishi wangu watakula,
lakini ninyi mtaona njaa;
watumishi wangu watakunywa
lakini ninyi mtaona kiu;
watumishi wangu watafurahi,
lakini ninyi mtaona haya.
14 Watumishi wangu wataimba
kwa furaha ya mioyo yao,
lakini ninyi mtalia
kutokana na uchungu wa moyoni,
na kupiga yowe kwa sababu

* **65:11** mungu wa Wakaldayo wa bahati nzuri; pia alijulikana kama *Gadi* † **65:11** mungu wa Wakaldayo wa majaliwa; pia alijulikana kama *Meni*

ya uchungu wa roho zenu.
15 Mtaliacha jina lenu
kuwa laana kwa watu wangu waliochaguliwa;
Bwana Mungu Mwenyezi atawaua ninyi,
lakini watumishi wake atawapa jina jingine.
16 Yeye aombaye baraka katika nchi
atafanya hivyo kwa Mungu wa kweli;
yeye aapaye katika nchi
ataapa kwa Mungu wa kweli.
Kwa kuwa taabu za zamani zitasahaulika
na kufichwa kutoka machoni pangu.

### *Mbingu mpya na dunia mpya*

17 "Tazama, nitaumba
mbingu mpya na dunia mpya.
Mambo ya zamani hayatakumbukwa,
wala hayatakuja akilini.
18 Lakini furahini na kushangilia daima
katika hivi nitakavyoumba,
kwa kuwa nitaumba Yerusalemu uwe wa kupendeza,
nao watu wake wawe furaha.
19 Nami nitaifurahia Yerusalemu
na kuwafurahia watu wangu;
sauti ya maombolezo na ya kilio
haitasikika humo tena.

20 "Kamwe hapatakuwa tena ndani yake
mtoto mchanga atakayeishi siku chache tu,
au mzee ambaye hataishi akatimiza miaka yake.
Yeye atakayekufa akiwa na umri wa miaka mia moja

atahesabiwa kwamba ni kijana tu,
yeye ambaye hatafika miaka mia moja,
atahesabiwa kuwa amelaaniwa.
21 Watajenga nyumba na kuishi ndani yake;
watapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake.
22 Hawatajenga nyumba, nao watu wengine waishi ndani yake,
au kupanda mazao na wengine wale.
Kwa kuwa kama zilivyo siku za mti,
ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu,
wateule wangu watafurahia kwa siku nyingi
kazi za mikono yao.
23 Hawatajitaabisha kwa kazi bure,
wala hawatazaa watoto ili wapatwe na majanga,
kwa kuwa watakuwa taifa lililobarikiwa na Mwenyezi Mungu,
wao na wazao wao pamoja nao.
24 Kabla hawajaita, nitajibu,
nao wakiwa katika kunena, nitasikia.
25 Mbwa-mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja,
naye simba atakula nyasi kama maksai,
lakini mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka.
Hawatadhuru wala kuharibu
katika mlima wangu mtakatifu wote,"
asema Mwenyezi Mungu.

# 66

*Hukumu na matumaini*

1 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,

“Mbingu ni kiti changu cha enzi,
nayo dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu.
Iko wapi nyumba mtakayoijenga kwa ajili yangu?
Mahali pangu pa kupumzikia patakuwa wapi?
2 Je, mkono wangu haukuumba vitu hivi vyote,
hivyo vikapata kuwepo?”
asema Mwenyezi Mungu.

“Mtu huyu ndiye ninayemthamini:
yeye ambaye ni mnyenyekevu
na mwenye roho yenye toba,
atetemekaye asikiapo neno langu.
3 Lakini yeyote atoaye dhabihu ya fahali
ni kama yeye auaye mtu,
na yeyote atoaye sadaka ya mwana-kondoo,
ni kama yule avunjaye shingo ya mbwa.
Yeyote atoaye sadaka ya nafaka,
ni kama yule aletaye damu ya nguruwe,
na yeyote afukizaye uvumba wa kumbukumbu,
ni kama yule aabuduye sanamu.
Wamejichagulia njia zao wenyewe,
nazo nafsi zao zinafurahia machukizo yao.
4 Hivyo, mimi pia nitawachagulia mapigo makali,
nami nitaleta juu yao kile wanachokiogopa.
Kwa maana nilipoita, hakuna yeyote aliyejibu,
niliposema, hakuna yeyote aliyesikiliza.
Walifanya maovu machoni pangu
na kuchagua lile linalonichukiza.”

5 Sikieni neno la Mwenyezi Mungu,
ninyi mtetemekao kwa neno lake:

“Ndugu zenu wanaowachukia ninyi
na kuwatenga ninyi kwa sababu ya Jina langu, wamesema,
‘Mwenyezi Mungu na atukuzwe,
ili tupate kuona furaha yenu!’
Hata sasa wataaibika.
6 Sikieni hizo ghasia kutoka mjini,
sikieni hizo kelele kutoka hekaluni!
Ni sauti ya Mwenyezi Mungu ikiwalipa adui zake
yote wanayostahili.

7 “Kabla hajasikia uchungu, alizaa;
kabla hajapata maumivu,
alizaa mtoto wa kiume.
8 Ni nani amepata kusikia jambo kama hili?
Ni nani amepata kuona mambo kama haya?
Je, nchi yaweza kuzaliwa kwa siku moja,
au taifa laweza kutokea mara moja?
Mara Sayuni alipoona uchungu,
alizaa watoto wake.
9 Je, nilete mwana hadi wakati wa kuzaliwa
na nisizalishe?” asema Mwenyezi Mungu.
“Je, nifunge tumbo la uzazi
wakati mimi ndiye nizalishaye?”
asema Mungu wako.
10 “Shangilieni pamoja na Yerusalemu na mfurahi kwa ajili yake,
ninyi nyote mnaompenda,
shangilieni kwa nguvu pamoja naye,
ninyi nyote mnaoomboleza juu yake.
11 Kwa kuwa mtanyonya na kutosheka
katika faraja ya matiti yake;
mtakunywa sana,

na kuufurahia wingi wa mafuriko ya ustawi wake.”
12 Kwa kuwa hili ndilo asemalo Mwenyezi
Mungu:
“Nitamwongezea amani kama mto,
nao utajiri wa mataifa kama kijito kifurikacho;
utanyonya na kuchukuliwa mikononi mwake,
na kubembelezwa magotini pake.
13 Kama mama anavyomfariji mtoto wake,
ndivyo nitakavyokufariji wewe,
nawe utafarijiwa huko Yerusalemu.”

14 Mtakapoona jambo hili, mioyo yenu itashangilia,
nanyi mtastawi kama majani;
mkono wa Mwenyezi Mungu utajulikana kwa watumishi wake,
bali ghadhabu yake kali
itaoneshwa kwa adui zake.
15 Tazama, Mwenyezi Mungu anakuja na moto,
magari yake ya vita ni kama upepo wa kisulisuli,
atateremsha hasira yake kwa ghadhabu kali,
na karipio lake pamoja na miali ya moto.
16 Kwa maana kwa moto na kwa upanga wake
Mwenyezi Mungu atatekeleza hukumu juu ya watu wote,
nao wengi watakuwa ni wale waliouawa na Mwenyezi Mungu.
17 “Watu wote wanaojiweka wakfu na
kujitakasa wenyewe ili kwenda bustanini,
wakimfuata aliye katikati ya wale wanaokula

nyama za nguruwe na panya pamoja na vitu vingine vilivyo machukizo, watafikia mwisho wao pamoja," asema Mwenyezi Mungu.

18 "Nami, kwa sababu ya matendo yao na mawazo yao, niko karibu kuja na kukusanya mataifa yote na lugha zote, nao watakuja na kuuona utukufu wangu.

19 "Nitaweka ishara kati yao, nami nitapeleka baadhi ya hao walionusurika kwa mataifa, hadi Tarshishi, kwa Puli na Waludi (wanaojulikana kama wapiga upinde), kwa Tubali na Uyunani, hadi visiwa vya mbali ambavyo havijasikia kuhusu sifa zangu au kuuona utukufu wangu. Watatangaza utukufu wangu miongoni mwa mataifa.
20 Nao watawaleta ndugu zenu wote, kutoka mataifa yote, hadi mlima wangu mtakatifu huko Yerusalemu kama sadaka kwa Mwenyezi Mungu, juu ya farasi, katika magari ya vita na magari makubwa, juu ya nyumbu na ngamia," asema Mwenyezi Mungu. "Watawaleta, kama Waisraeli waletavyo sadaka zao za nafaka, katika Hekalu la Mwenyezi Mungu, katika vyombo vilivyotakaswa.
21 Nami nitachagua baadhi yao pia wawe makuhani na Walawi," asema Mwenyezi Mungu.

22 "Kama vile mbingu mpya na nchi mpya ninazozifanya zitakavyodumu mbele zangu," asema Mwenyezi Mungu, "ndivyo jina lenu na wazao wenu watakavyodumu.
23 Kutoka Mwezi Mpya hata mwingine, na kutoka Sabato hadi nyingine, wanadamu wote

watakuja na kusujudu mbele zangu," asema Mwenyezi Mungu.

24 "Nao watatoka nje na kuona maiti za wale walioniasi mimi. Funza wao hawatakufa, wala moto wao hautazimika, nao watakuwa kitu cha kuchukiza sana kwa wanadamu wote."

ccv

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: “Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible.”

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d